Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NANE

## KIKAO CHA NANE - TAREHE 10 FEBRUARI, 2005

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni taarifa fupi tu kuhusu Miswada. Nilipotoa taarifa ya Miswada tuliyoijadili katika Mkutano uliopita nilisema Miswada mitatu ilishapata kibali cha Rais, na kwamba Miswada mitatu ilikuwa bado haijapata kibali kwa sababu ilichelewa katika uchapishaji. Sasa leo napenda kuliarifu Bunge kwamba ile Miswada mitatu ambayo ilikuwa bado haijapata kibali cha Rais, sasa imeshapata kibali na itakuwa Sheria za nchi. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Baraza la Hifadhi ya Mazingira kwa Mwaka ulioishia Juni, 2004 *(The Annual Report and Accounts of the National Environment Management Council (NEMC) for the year ended June, 2004).*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Hesabu za Halmashauri za Miji na Wilaya kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2003. *(The Report of Controller and Auditor-General on Local Authority Accounts for the period Ended 31st December, 2003).*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 84

**_Couples_ Ndani ya Bunge**

**MHE. SALOME J. MBATIA** aliuliza:-

Kwa kuwa ni jambo jema kuwa na Waheshimiwa Wabunge mke na mume *(couple)* ndani ya Bunge lako Tukufu na kwa kuwa hadi sasa tayari ziko *couples* tatu ndani ya Bunge.

(a) Je, katika nchi wanachama wa *SADC* kuna Mabunge mangapi yenye Wabunge ambao ni mke na mume?

(b) Je, ni Mabunge mangapi yamebahatika kuwa na Spika na mkewe Wabunge?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haina takwimu za aina hiyo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameuliza. Serikali inavyojua ni kwamba kila raia mwenye sifa zinazohitajika anayo haki ya kugombea Ubunge bila kujali kama ni mke au ni mume wa mtu ambaye tayari ni Mbunge. Wote wawili wakipata bahati ya kuchaguliwa basi wanakuwa ni Wabunge. *(Makofi)*

(b) Kama nilivyosema katika jibu langu katika kifungu cha (a) Serikali haina takwimu za jambo hilo kwa upande wa Mabunge ya nchi nyingine.

Na. 85

**Madai mbalimbali ya Walimu na Waganga**

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Watumishi hususan walimu na waganga wamekuwa wakidai malimbikizo ya fedha za nyongeza za mishahara, malipo ya likizo na ya uhamisho.

(a) Je, Wilaya ya Geita ina walimu wangapi wanaodai Serikali kiasi gani cha fedha na je, Serikali ina mpango gani wa kuwalipa?

(b) Kwa kuwa Serikali imechelewesha sana malipo hayo na kama kweli ina upendo na kujali Watumishi wake itakuwa tayari kuwaongezea 10% kama riba kila mwezi kwa kuwa thamani ya fedha yetu inashuka kila siku?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ilifanya uhakiki wa madai mbalimbali ya walimu wake wakiwemo waganga na walimu mwezi Julai, 2004. Baada ya kukamilisha uhakika, malipo ya malimbikizo ya mishahara yanayotokana na upandishaji vyeo yameendelea kulipwa tangu mwezi Agosti, 2004 hadi Desemba, 2004 kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Geita ina walimu wapatao 796 kati ya walimu 2,491 wanaodai kiasi cha Shilingi 286,254,934/= kama ifuatavyo:-

- Uhamisho ni shilingi 226,685,900/=;
- Masomo ni shilingi 32,742,126/=;
- Matibabu ni shilingi 5,063,930/=;
- Waliofariki ni shilingi 2,627,424/=; na
- Likizo ni shilingi 9,097.20/=

Kuna madai ya mapunjo ya mishahara ya walimu yanayofikia shilingi 166,719,633.55/= ambayo hayajahakikiwa na Menejimenti ya Utumishi na Hazina. Pia watumishi wa Afya 244 wanayo madai yanayofikia shilingi 60,530,818/=.

Madai ya Halmashauri ya Geita yaliyowasilishwa Menejimenti ya Utumishi wa Umma yanaonekana na makosa mbalimbali. Kutokana na makosa hayo ambayo yasingeweza kusahihishwa Dar es Salaam, yalirejeshwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Geita. Mkurugenzi Mtendaji baada ya kusahihisha makosa hayo atayawasilisha tena Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Hazina ili malipo yaweze kufanyika.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taratibu zilizopo, hatuna utaratibu wa kulipa riba kwa mtumishi anayecheleweshewa maslahi yake. Isitoshe Kifungu Na. 195 cha Kanuni za fedha za Halmashauri ya mwaka 1997, hakijaidhinisha riba kwa madai yoyote ya mtumishi kwa mwajiri wake.

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniruhusu ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa tatizo la kuwalipa riba hawa watumishi ambao wanadai kwa muda mrefu ni Sheria.

(a) Je, Mheshimiwa Waziri anaonaje sasa ukileta hiyo Sheria tukaipitisha ili Serikali iwajibike kuona kwamba inalimbikiza madeni ya watu?*(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Serikali imekuwa ikiahidi tangu muda mrefu hadi leo na haitimizi wajibu wake na juzi Waziri Mkuu amepeleka Tume kwenda kuangalia madeni na ikaonekana kuna ubadhirifu mkubwa sana, je, Serikalini ni watendaji wangapi wamechukuliwa hatua ili matendo hayo yasiendelee?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hili la riba halimo kwa hivi sasa kwa mujibu wa Sheria tulizonazo. Lakini kama Waheshimiwa Wabunge wanaona ni busara kufanya hivyo, bado jambo hili linaweza kujadiliwa. Lakini nataka niseme tu kwamba Serikali hii ni yetu wote na kwa hiyo, tukifikia maamuzi kama hayo, basi tujue vile vile *implication* zake nini. Kwa sababu mambo mengine siyo ya makusudi yanatokana na mazingira fulani fulani ambayo hayakwepeki.

Lakini hili swali la pili, nashukuru tu kwamba amesema kwamba Tume iliundwa na ni kweli na taarifa ile bado inafanyiwa kazi. Nina hakika itakapokamilika, ziko hatua zitakazochukuliwa kwa watumishi wale wote watakaonekana ni wabadhirifu au wazembe kwa namna moja au nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu lifanye subira zoezi hilo likamilike ili tuweze kupata matokeo yake. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza. Tatizo hili la malimbikizo la malipo ya walimu na watumishi wengine wa Serikali, limetapakaa nchini nzima kwa kifupi Mwanza linatusumbua sana mpaka sasa walimu wanadai mishahara, fedha za uhamisho na mengine. Sasa katika taarifa ambayo inahusishwa na Waziri Mkuu, je, watu wa Mwanza imewahusisha kwa kiasi gani ili kwamba nao matatizo yao yaweze kutatuliwa mara moja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Stephen Kazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kwamba yapo malimbikizo mengi tu ambayo yamelimbikizwa ndani ya kipindi kirefu kidogo. Lakini wote nadhani tunafarijika kwamba baada ya Tume ile na kwa maagizo ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa, yako mambo ambayo itabidi yasitishwe au yakomeshwe ili kutuwezesha kuwa *up to date.* Sehemu uliyoongezea kuhusu Mwanza itaniwia vigumu kukupa maelezo ya uhakika labda mpaka baada ya kuwa tumejaribu utafiti kidogo ili tukuambie jambo la ukweli.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa malimbikizo ya

walimu na watumishi wengine yamekuwa ni makubwa sana, ningeomba tu kwamba kama Serikali inaweza kwa watumishi walioko vijijini wanapofika kufuata mishahara yao na kulala na kurudi.

Je, haya malipo yanaweze yakawa sehemu ya malimbikizo ya madeni kuliko wanapopata hasara ya kuja kufuata mishahara na hakuna mtu ambaye anaweza kuwalipa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Benedict Losurutia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama tulivyokwisha kusema wote tunakiri kwamba tatizo hili lipo na ni kubwa, lakini faraja ni kwamba linashughulikiwa sasa. Hii rai kwamba watumishi wanapokwenda kufuata mishahara yao, zile gharama za kulala pale na nauli zao ziingizwe katika utaratibu wa marejesho haukufidiwa na Serikali. Tulishawahi kulieleza hapa kwamba kwa sasa utaratibu huo haupo na hata kama mtaamua kufanya hivyo bado mtaamua bado tutazidi kujitwisha mzigo kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kwa sasa mishahara hii tuliamua kwamba ipitishwe kwenye Mabenki na ndio utaratibu hivi sasa sehemu nyingi unatumika. Kwa hiyo, kwa utaratibu huu tunaamini lile tatizo pengine la kukaa muda mrefu kama ilivyokuwa siku za awali utapunguza kwa kiasi kikubwa sana.

Na. 86

**Mpango wa Wananchi Kuishi Vijijini Nchini**

**MHE. NJELU E. M. KASAKA** aliuliza:-

Kwa kuwa mpango wa wananchi kuishi vijijini ni mzuri na umesifiwa sana na kwa kuwa kwa kipindi kirefu idadi ya vijiji imeendelea kutajwa kuwa ni 8,000.

(a) Je, hakuna vijiji vipya vilivyoanzishwa sasa?

(b) Je, kama mpango huu ni mzuri kama unavyosifiwa, kwa nini Serikali inaacha watu kutawanyika maeneo mbalimbali bila kuzingatia utaratibu wa sera ya vijiji?

(c) Je, ni vijiji vingapi viliandikishwa katika Mkoa wa Mbeya Kiwilaya katika kipindi cha mwaka 2001 hadi 2003?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, naomba tu kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa bado vijiji vinaendelea kuanzishwa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini kwa kuzingatia pale eneo husika linapotimiza masharti ya kuwa kijiji.

Aidha, kulingana na takwimu za mwezi Desemba, 2004 jumla ya vijiji vilivyokuwa vimeandikishwa ni 10,336. Lakini kati ya hivyo vijiji 528 vimefutwa kwa sababu kumeundwa Mamlaka za Miji midogo 90 ambayo zilizoanzishwa mwezi Oktoba, 2004 na baadhi ni inatokana na maeneo kama ya Manispaa kufutiwa vijiji ndani ya maeneo yao.

(b) Mheshimiwa Spika, vijiji vipo kwa mujibu wa Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 Kifungu cha 22 na pia hutawaliwa na Sheria ndogo mbalimbali zinazotawala matumizi bora ya Ardhi *(Land use Plan)* ambapo maeneo yanatengwa kwa ajili ya makazi, mifugo, kilimo, misitu, huduma za jamii na kadhalika. Katika mazingira hayo suala la watu kutawanyika linaweza likadhibitiwa kwa kiasi kikubwa

Mheshimiwa Spika, pamoja na mpango mzuri wa wananchi kuishi vijijini kumekuwepo na tatizo la uanzishwaji wa vijiji bila kufuata Sheria, Kanuni na taratibu. Serikali inasisitiza Halmashauri zote nchini kusimamia Sheria zinazotawala uanzishaji wa vijiji na matumizi bora ya ardhi ili vijiji viendelee kuwa mahali bora pa kuishi.

(c) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2001 hadi 2003 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, haikuandikisha vijiji vyovyote katika Halmashauri za Mkoa wa Mbeya. Zoezi la kuandikisha vijiji kwa nchi nzima lilifanyika mwaka 2004 na vijiji vya Mkoa wa Mbeya vilivyosajiliwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ileje vijiji 15, Kyela vijiji 22, Mbarali vijiji 12 na Rungwe vijiji 14.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kuuliza maswali mawili. Kwa kuwa siku hizi umezuka mtindo wa kuvipandisha hadhi vitongoji na kuwa vijiji.

(a) Je, Serikali huwa inaandaa mambo gani kabla ya kitongoji kukipandisha na kuwa kijiji? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa malengo ya awali ya kuanzisha vijiji ilikuwa ni pamoja na kusogeza huduma za jamii kama vile shule, hospitali, maji karibu na wananchi au wananchi kusogea karibu na huduma hizo. Je, mnapoandikisha vijiji vya sasa malengo haya yanazingatiwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, vitongoji ndivyo vinavyoongezewa hadhi na kuwa vijiji. Lakini vitongoji hivi kabla ya hapo vinakuwa ni sehemu ya kijiji husika. Kwa hiyo, linalotokea pale ni kwamba idadi ya watu imeongezeka na kuna *demand* sasa ili kurahisisha utawala kugawa kijiji hicho au vitongoji kadhaa katika kijiji kingine. Ndio maana tunavi-*separate* na kuanzisha kijiji kingine ndani ya kijiji hicho. Lakini msingi mkubwa ni kwamba unapoanzisha kijiji ni budi pawepo vitongoji angalau vinne au vitano katika eneo hilo.

Kwa hiyo, ndio msingi mkubwa sana ambao tunauzingatia pamoja na idadi ya watu na huduma mbalimbali ambazo zinakuwa ndani ya eneo hilo au matakwa ambayo yanahitaji, sasa huduma kutengwa na kuongezewa katika maeneo kama hayo.

Katika kujibu lile swali la pili, tunachoweza kusema ni kwamba suala la utoaji wa huduma kuwa karibu na wananchi katika maeneo husika linazingatiwa kwa kiasi kikubwa sana. Mara nyingi utakuta vitongoji hivyo vinavyodai kuwa Serikali ya Kijiji kwa kawaida utakuta vimeshapata huduma mbalimbali hasa shule za msingi na katika baadhi ya maeneo hasa Zahanati. Kwa hiyo, kwa msingi huo, jambo hili linazingatiwa kwa kiasi kikubwa sana.

**MHE. HENRY D SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi sana na nashukuru kwa kuniona.

Mimi nina swali moja la nyongeza, kwa kuwa utaratibu wa kuanzisha vijiji unaanzia katika ngazi ya kijiji chenyewe, Kata hadi Wilaya na mapendekezo yanaletwa kwenye Ofisi ya TAMISEMI. Viko vijiji ambavyo vimependekezwa katika utaratibu huo na vina sifa. Kwa mfano, Wilaya ya Lushoto tuliomba vijiji 50 lakini vijiji vilivyokubaliwa ni kumi na hii imeleta malalamiko.

Je, ni vigezo gani vinavyochukuliwa na TAMISEMI katika kukubali vijiji na kuacha vijiji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Henry Shekiffu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba taratibu zote za uanzishaji wa maeneo mbalimbali unaanzia katika ngazi ya chini kabisa yaani kwenye vijiji vinavyohusika. Sasa ukishawasilisha mapendekezo hayo TAMISEMI yako mambo mengi ambayo yanazingatiwa na kwa uhakika siwezi nikasema tulipoondoa vijiji vile 40 mlivyopendekeza kulikuwa na sababu zipi kwa sababu sikuwa nimejiandaa kwa jambo kama hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini ninaloweza kusisitiza ni kwamba bado unayo nafasi ya kuja TAMISEMI tukakupa maelezo kwa nini vijiji vile vingine 40 havikukubalika. Lakini kwa sababu sisi ndio tunasimamia taratibu hizi, kwa sehemu kubwa naamini

itakuwa vingi havikukidhi masharti ya uanzishaji. Lakini bado tunakukaribisha ili uweze kupata maelezo ya uhakika zaidi.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, sasa ni kipindi cha maswali na kwamba maswali yote Waheshimiwa Wabunge wanaleta kwako na wanategemea kujibiwa ndani ya Bunge hili. Jumatatu, nilikuwa na swali kuhusu watu wa Bariadi juu ya pamba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Mheshimiwa Mgana Msindai, ukasema maswali letu yatapangiwa siku nyingine.

**SPIKA:** Naomba uombe Mwongozo wa Spika, mwisho wa kipindi cha Maswali. Sasa hivi unatupotezea muda wa maswali.

Na. 87

**Programu za *TASAF***

**MHE. MARGARETH A. MKANGA** aliuliza:-

Kwa kuwa moja ya malengo ya *TASAF* ni kuanzisha programu za elimu ya watu wazima, watoto yatima, watu wenye ulemavu na wazee.

Je, ni programu ngapi na wapi zimeanzishwa tangu *TASAF* ianze?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ni programu ya Taifa iliyoanzishwa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kuunga mkono nguvu za wananchi katika kuimarisha miundombinu katika maeneo ya barabara, elimu, afya, maji na kadhalika.

*TASAF* haina lengo la moja kwa moja la kuanzisha programu ya elimu kwa watu wazima, watoto yatima, watu wenye ulemavu na wazee. Hata hivyo huko nyuma yake *TASAF* ilifanya majaribio katika Wilaya ya Bukoba, Shinyanga, Meatu na Kibaha kuhusu jinsi ya kuwasaidia watu wenye ulemavu, wajane, wazee, watoto yatima na masuala ya Ukimwi. Majaribio haya yamekuwa na mafanikio na hivyo *TASAF* mkupuo wa pili itakuwa na kitengo maalumu kwa ajili ya makundi haya kwa nchi nzima.

**MHE. MARGERETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza. Pamoja na jibu zuri la Mheshimiwa Waziri, nimeshtushwa kidogo kuambiwa kwamba *TASAF* haikuwa na lengo hili.

Je, vile vipeperushi mlivyotupa mwaka jana vikieleza malengo haya ya *TASAF* hili lengo lilikuwa ni la uongo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, ningependa kumjibu Mheshimiwa Margareth Mkanga, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa jinsi madhumuni ya *TASAF* yalivyo na vile vile kwa jinsi ilivyotekelezwa nchi nzima kwa ufanisi wa hali ya juu, haijawahi kufikiria na haitafikiria kufanya jambo lolote kwa ajili ya kuwadanganya wananchi. Nilichosema hapa ni kwamba maeneo hayo ambayo yatafanyiwa kazi katika awamu ya pili haya ya watu ambayo wanakuwa rahisi kuingia kwenye dimbwi la umaskini. Maeneo kama alivyoona kwenye vipeperushi, nimesema kwamba yalifanyiwa kama *pilot project* kwenye maeneo mbalimbali.

Kutokana na mafanikio haya sasa ndio tutakwenda moja kwa moja kwenye utekelezaji kwenye awamu ya pili ambayo inaanza muda wowote sasa. Kwa hiyo, haikuwa na nia wala hatujadanganya katika kuwaeleza nia hiyo wananchi. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba lengo kubwa la Mradi huu wa *TASAF* ni kuondoa umaskini na kupeleka miradi mbalimbali katika sehemu za nchi yetu ya Tanzania na kwa kuwa katika Jimbo langu la Wawi, toka ilipoanzishwa *TASAF* mpaka leo kila siku napiga kelele hapa na Bunge sijapata mradi hata moja wa *TASAF*. Naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri kila siku ananiambia Mradi wa *TASAF* utatolewa katika Jimbo la Wawi kuna kosa gani hasa mpaka leo Mradi wa *TASAF* haujafika katika Jimbo langu la Wawi? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, ningependa kumjibu Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitalijibu swali hili kwa kukumbusha Bunge lako Tukufu kuhusu utaratibu unaofuatwa na *TASAF*.

*TASAF* utekelezaji wake awamu ya kwanza ulihusisha Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba. Kwa upande wa Bara, miradi hii inasimamiwa na Ofisi ya Rais na vile vile wenyeviti wanaokubali maoni ya wananchi ya miradi hii ya *TASAF* wenyeviti wake ni Wakuu wa Wilaya.

Kwa upande wa Zanzibar, miradi hii inaratibiwa na Ofisi ya Waziri Kiongozi na Wakuu wa Wilaya miradi hii huipeleka mpaka kwa Waziri Kiongozi lakini ikipokelewa na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Waziri Kiongozi. Nimewahi kusema huko nyuma na

narudia hapa kwamba Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba fedha zinatolewa na Makao Makuu ya *TASAF* Dar es Salaam, lakini mradi gani utekelezwe lazima ipitie miradi hiyo kwenye Ofisi ya Waziri Kiongozi.

Kwa hiyo, pamoja na kufanya kazi na nini kwa maana ya kusimamia *TASAF* hapa Bungeni ningemshauri apitishe na aonane na Waziri mwenzangu upande wa Serikali ya Zanzibar ili kusudi kuoanisha nia yake ili kusudi nao Wawi wafaidike na mradi huu. Hata hivyo, namalizia kwa kusema kwamba tutazungumza tena na Waziri mwenzangu kwamba Wawi umeisikia Bungeni inalalamikiwa! *(Makofi)*

Na. 88

**Mfuko wa Kuondoa Umaskini kwa Wanawake na Vijana**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa wanawake na vijana wengi katika maeneo mengi nchini wakiwemo wale wa Singida wanaondokana na miradi midogo midogo na kuanzisha miradi mikubwa yenye kuhitaji mitaji mikubwa.

Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka kuboresha mfuko wa kuondokana na umaskini ili wanawake na vijana wengi waweze kunufaika nao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumkumbusha Mheshimiwa Diana Chilolo, pamoja na Bunge lako Tukufu kuwa umaskini uko katika sura na tabia nyingi. Kwa hiyo, hata juhudi za kupambana na umaskini ili kuleta matokeo bora zinatakiwa zilenge katika sura na tabia zote za umaskini.

Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali haioni mfuko mahususi wa kuondokana na umaskini badala yake imekuwa ikiandaa na kutekeleza mikakati na programu mbalimbali kupitia Wizara mbalimbali kwa lengo la kupambana na umaskini katika sura na tabia zake zote. Mkakati na programu ambayo Serikali imekuwa ikitekeleza unalenga kuimarisha miundombinu, huduma za jamii na kuiwezesha jamii pamoja na makundi maalum katika juhudi zake za kujiongezea kipato na uwezo wa kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kupunguza umaskini wa mwaka 2000 - 2003 ambao sasa umefanyiwa mapitio na kupitishwa na Serikali ulitazama sura na tabia za umaskini nchini na kuainisha maeneo mbalimbali ya kutekeleza. Katika kutekeleza mkakati huo programu na miradi mbalimbali imetekelezwa na Serikali, Wahisani, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na sekta binafsi. Serikali imekuwa ikitekeleza miradi

mbalimbali kupitia mfuko wa *TASAF* inayolenga kujenga uwezo wa jamii kwa kuweka miundombinu mbalimbali kama vile ujenzi wa shule, barabara, maji, majosho ya mifugo, mabwawa kwa ajili umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kusaidia juhudi za wanawake na vijana katika kutekeleza miradi yao ya kuinua kipato Serikali inatekeleza mradi wa *SELF* kama ambavyo nimekuwa nikieleza mara kwa mara labda hapa Bungeni unalenga kukuza uwezo wa taasisi za mikopo ili ziweze kuwafikia wananchi walio wengi zaidi hasa walio maskini wanawake kwa vijana. Mradi wa *SELF* ambao ulianza katika mikoa saba ukiwemo mkoa wa Singida, utaendelea kupanua shughuli zake mwaka hadi mwaka. Pamoja na mikoa ya awali, awamu ya pili ya mradi wa *SELF* imepanua shughuli zake katika mikoa mingine minane na ikiwemo Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mara, Mwanza, Iringa na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kufurahisha kuona kuwa wanawake na vijana sasa wanaanzisha miradi mikubwa inayohitaji mitaji mikubwa. Wanawake na vijana kote nchi na hususani wale wa Singida watakaokuwa na miradi ambayo inahitaji miradi isiyozidi shilingi milioni moja wanaweza kuendelea kufaidika na mifuko iliyopo kwani taasisi nyingi zinazopata mikopo kutoka *SELF* hutoa mikopo kati ya shilingi 50,000/= hadi shilingi milioni moja na baadhi ya taasisi chache hutoa mikopo inayofikia shilingi milioni tano.

Mheshimiwa Spika, mwisho ili kuwawezesha wanawake na vijana na wananchi kwa ujumla kutekeleza miradi yao yenye kuhitaji mitaji mikubwa Serikali inaandaa mpango maalum wa kuhusisha mali zote zisizotambulika rasmi kama vile nyumba zilizoko katika maeneo yasiyopimwa. Programu hii itaweka utaratibu mzuri wa kuthaminisha mali mbali mbali zisizo hamishika ili kurahisisha ubadilishanaji wa mali hizo.

Aidha, mpango huu mara ukamilikapo utawezesha kupatikana kwa taarifa za kila mwananchi mali zake pamoja na thamani zake. Kupatikana kwa taarifa sahihi za wananchi pamoja na mali zao kutawezesha wananchi kupata mikopo kutoka mabenki makubwa ambayo kwa sasa wa wananchi wengi hawafaidiki na mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kupatikana kwa mikopo kutoka mabenki makubwa kwa wananchi walio wengi tofauti na ilivyo sasa kutawezesha wanawake na vijana kuendesha miradi mikubwa yenye kuhitaji mitaji mikubwa kuliko ile itolewayo na taasisi mbalimbali ambazo zinafanya kazi kwa kushirikiana na *SELF.*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri. Pamoja na majibu mazuri napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mradi wa *SELF* umeonyesha kufaulu katika maeneo mengi ambako umefika. Je, Serikali haioni kwamba sasa kuna haja ya kuwapeleka waratibu kuweza kutoa elimu kwa wananchi ili wengi wa uelewe mradi huu ili waweze kujua ni njia gani ama taratibu gani za kufanya ili waweze kupata mkopo kupitia mradi huu wa *SELF? (Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMUWA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kazi mojawapo ya *SELF* ni kutoa elimu kwa walengwa, wale ambao wanataka kufaidika na mikopo kupitia *SACCOS* na vyama vingine vya ushirika. Kwa hiyo, kazi hiyo inafanyika, lakini hata hivyo kwa maana ya kupanua zaidi kila uwezo unapopatikana tutazingatia ushauri ambao ameutoa Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mpango huu wa mradi wa *SELF* sasa umeshaingia katika mkoa wa Ruvuma na kwa kuwa kwa muda sasa toka mradi huo umeingia *SACCOS* za wanawake katika Wilaya zote za mkoa wa Ruvuma zimekuwa zikihangaika sana kufanikiwa kupata mkopo ama uwezeshaji kutoka katika mradi huo na hazijafanikiwa mpaka sasa. Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuhakikisha kwamba *SACCOS* hizo zinawezeshwa kulingana na majibu yake aliyoyatoa kwamba zitapewa kipao mbele?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMUWA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza kwa kuwawezesha akinamama kupitia *SACCOS* mkoa wa Ruvuma kuhamasika kiwango hicho na kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu mwaka juzi Ofisi ya Makamu wa Rais ilimsaidia Mheshimiwa Jenista Mhagama, kupata fungu la fedha la kuhamasisha na kuwafunza akinamama namna ya kukopa. Nadhani hayo ndio matokeo.

Sasa kuhusu watapata lini, ni mwaka jana tu wakati wa Bajeti yetu hapa ndipo mkoa wa Ruvuma ulipoongezwa kwenye orodha ya mikoa ambayo inayofaidika na *SELF.* Kwa hiyo, ningemshauri Mheshimiwa Mbunge maadam sasa amekwishafika hatua ya *SACCOS* zake zimekwisha omba makao makuu basi kati ya sasa na pengine siku chache zijazo nitaulizia meneja wa *project,* suala hili limefikia wapi, na kwa sababu ninaelewa Mheshimiwa Mbunge hawezi kwenda Ruvuma au Songea bila kupitia Dar es Salaam, namkaribisha ofisini kwetu ili achukue majibu kabisa juu ya utekelezaji wa maombi hayo. *(Makofi)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika mradi wa *SELF* fedha za *SELF* zinapitia kwenye taasisi nyingine; na kwa kuwa kwa kufanya hivyo riba ambayo vikundi vya wanawake na vijana inadaiwa inaongezeka. Je, Serikali haioni kwamba muda umefika sasa *SELF* ikatoa mkopo moja kwa moja badala ya kupitia taasisi nyingine ili kuwapunguzia riba wanawake na vijana? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMUWA RAIS (MHE. EDGAR D. MAOKOLA-MAJOGO):** Mheshimiwa Spika, mkoa wa Lindi ni kati ya ile mikoa ya mwanzo ambayo *SELF* inafanya kazi na inaendelea kufanya kazi na mbali na *SACCOS* zilizopo huko lakini *SIDO* Lindi ni taasisi mojawapo ambayo inapata fedha za *SELF* na wao inawakopesha wateja moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, huu mradi *SELF* ni mkataba kati ya Benki ya Maendeleo ya Afrika na sharti mojawapo, ilikuwa ni kwamba *SELF* yenyewe menejimenti peke yake, haiwezi ikawafikia wananchi sehemu zote kutokana na udogo wa taasisi yenyewe. Ndio maana tukasema kwamba wao wawe ni kama taasisi ambayo inatoa kwa wale ambao wanawagusa walengwa moja kwa moja. Kwa hiyo, kadri ya uwezo wa taasisi ya *SELF* inavyopanuka jambo hili linaweza likafikiriwa. Lakini kwa sasa inabidi tuendelee kupitisha fedha hizo kwa hizo asasi jambo ambalo tumeliona linafaa. Lakini wazo la Mbunge linaweza likatiliwa maanani kadri ya uwezo wa *SELF* unavyozidi kupanuka.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu ya Rais, ningependa kutoa majibu ya nyongeza ya maswali yaliyoulizwa kama ifuatavyo:-

Serikali pamoja na mfuko wa *SELF* inamifuko mbalimbali ya kusaidia kuondoa umaskini. Mfuko mmoja ambao tumeutumia sana ni mfuko wa *NDF* ambao unapitia Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kupitia *SIDO.* Mfuko huu sasa hivi una mzunguko wa fedha zaidi ya bilioni nne na inazunguka katika kila mkoa. Tungependa tuwashauri Waheshimiwa Wabunge wawasaidie wananchi waweze kufuata mifuko hiyo katika mikoa yao. Kila mkoa una huo mfuko na fedha zipo.

Mheshimiwa Spika, tungependa kuongeza kwamba mfuko tulioutangaza hapa wakati wa Bajeti huo mfuko wa dhamana sasa uko tayari, taratibu zimekuwa tayari, ningewaomba Waheshimiwa Wabunge kwa miezi sita iliyobaki tuwasaidie wananchi waweze kutumia mfuko huu ambao una bilioni moja. Ahsante kushukuru. *(Makofi)*

Na. 89

**Ongezeko la Tembo Katika Hifadhi Zetu**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO** aliuliza:-

Kwa kuwa idadi ya Tembo/Ndovu imeongezeka katika Hifadhi za Wanyamapori, ikiwemo Hifadhi ya Liwale; na kwa kuwa wanyama hao wamekuwa wakiharibu mazao mbalimbali ya kilimo na kusababisha upungufu mkubwa wa chakula kwa wananchi wanaoishi karibu na hifadhi hizo wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Liwale:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuongeza idadi ya askari wanyamapori *(Games Scouts)* kwa kushirikiana na Halmashauri husika ili kukabiliana na ongezeko hilo la wanyama waharibifu na ni zipi sifa za *post* hiyo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa fidia kutokana na vifo vya wananchi vilivyosababishwa na wanyama waharibifu pamoja na fidia ya mali na mazao yao?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka utaratibu utakaowaruhusu wananchi wa Liwale husussan wa kijiji cha Kikulyungu kuvua samaki kwenye Ziwa Kihurumila lililopo ndani ya Hifadhi kwa ajili ya matumizi yao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, Mbunge wa Liwale, lenye sehemu (a), (b) na ( c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuongeza idadi ya askari wanyamapori yaani *Game Scouts,* Serikali inafanya mambo yafuatavyo:-

(a) Kujenga hoja kwenda Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma ya kuajiri askari waliomaliza kidato cha nne au cha sita. Askari hao watapangwa kwenye vituo mbalimbali kufanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja na hatimaye kupatiwa mafunzo kwenye vyuo vya Pasiansi na Mweka.

Kwa mwaka 2004/2005 Wizara yangu imepewa kibali kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma cha kuajiri watumishi 80 wenye sifa ya Stashahada ya Chuo cha Taalum ya Wanyamapori Mweka ambao pamoja na majukumu mengine watafanyakazi ya udhibiti wanyama wakali na waharifu.

(b) Kuishauri Halmashauri ya Wilaya ya Liwale kuajiri askari wanyamapori wa kutosha na wenye taaluma stahili ili kukabiliana na ongezeko la wanyama waharifu hususani tembo.

(c) Kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Liwale kutoa mafunzo kwa askari wa wanyamapori wa vijiji kuhusu mbinu za kudhibiti wanyama waharibifu kwa kuzingatia kanuni ya 57 ya maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya wanyamapori ya mwaka 2002.

(d) Kikosi dhidi ya ujangili Kanda ya Kusini kitaendelea kushirikiana na askari wanyamapori wa vijiji, askari wa Pori la Akiba la *Selous* na wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale katika kudhibiti wanyama waharibifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fidia, Wizara yangu haina utaratibu wa kutoa fidia kwa watu waliouawa na wanyamapori. Hata hivyo, Wizara imekuwa ikitoa kifuta machozi cha shilingi 50,000/= kwa kila familia ya Marehemu baada ya kupata taarifa sahihi kutoka kwenye Wilaya husika.

Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la *Selous* linahifadhiwa kwa mujibu wa Sheria ya kuhifadhi ya wanyamapori Na. 12 ya mwaka 1994. Kwa mujibu wa Sheria hiyo viumbe hai wote ndani ya pori hilo wakiwemo samaki vimehifadhiwa. Kwa hali hiyo, shughuli za uvuvi haziruhusiwi kwa mujibu wa Sheria hiyo.

**MHE. HASAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, je, inapotokea wanyama pori kufa ghafla kwa wingi kama tembo, twiga, simba, ujumbe wa Kiserikali mzito unatumwa mara moja kwenye sehemu ya

tukio. Inapotokea kwamba binadamu wameuawa na wanyama pori hakuna hatua inayofuatia ya haraka haraka kama hiyo, je, nani zaidi, wapiga kura au wanyama pori? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Endelea na swali la pili. Ahsante liko swali moja tu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, sote tunajua kwamba binadamu ni muhimu kuliko wanyama zaidi. Lakini niseme kwamba tunapozungumzia Serikali, tunazungumzia pamoja na Serikali katika ngazi ya Halmashauri, katika ngazi ya Wilaya, katika ngazi ya Mkoa na katika ngazi ya Taifa na kwa maana hiyo pale ambapo kwa kweli kumetokea na matatizo na wananchi kuuwawa katika ngazi za Halmashauri, katika ngazi za Wilaya ya Mkoa wamekuwa mstari wa mbele kabisa katika kutoa pole katika familia hizi na pia kuhudhuria hata mazishi katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nafikiri nimejibu swali la Mheshimiwa Mbunge, alikuwa na swali la pili lakini bahati mbaya hakuweza kuliuliza. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Ni mwaka wa Uchaguzi Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo, wote tutambue hivyo. *(Kicheko)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, mimi ningependa kuwauliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa tunakuwa na nyani wengi na ngedere ambao wanaharibu mazao ya binadamu na tunajua kwamba watanzania wengi wanategemea chakula chao kutoka mashambani.

Je, Wizara yake inamkakati gani wa kupunguza idadi kubwa ya nyani na ngedere wanaoharibu mazao ya binadamu kwa sababu sidhani kwamba kwa kweli wale nyani ambao wanaharibu ni kivutio cha utalii kama tunavyofikiri?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, tuna biashara ya wanyama hai kwenda nchi za nje na sehemu moja ni biashara ya hawa nyani na ngedere ambao kila mwaka tunatoa vibali na kwa Watanzania tu ambao kusafirisha nyani na ngedere kwenda nchi za nje. Mahali ambapo kunatokea na matatizo makubwa basi idara ya wanyamapori ikishirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, ina kuwa inahusika moja kwa moja.

**MHE. MATHEW TAKI OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali inapata fedha nyingi kutokana na uhifadhi wa wanyamapori, je, Serikali haioni kuwa kutolipa fidia kwa vifo vinavyosababishwa na wanyamapori haioni kwamba ni uonevu na ni kutokuthamini maisha ya binadamu hususani kwa eneo kama la Ngorongoro ambalo wanadamu na wanyama wana haki sawa ya kwenye eneo lile? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba Serikali inapata fedha nyingi kutokana na uhifadhi ikiwemo utalii. Lakini pia hapo hapo niseme kwamba Serikali pia inatumia fedha nyingi katika masuala haya ya uhifadhi na tunajua hapa kwamba kwa mfano katika utalii wa uwindaji asilimia 25 ya fedha zinazopatikana zinakwenda zote kwenye Halmashauri za Wilaya ambazo zinatumika katika maendeleo yao.

Lakini katika upande wa Ngorongoro kwa kweli ni kwamba utaratibu umekuwa kati ya hifadhi ya *Ngorongoro NSA* pamoja na wananchi wenyewe kuweza kuwashirikisha katika masuala mbalimbali. Kwa mfano, kuna utaratibu wa kuwashirikisha wafugaji wa Ngorongoro katika mikutano mbalimbali na katika Kamati mbalimbali za uhifadhi. Lakini hapo hapo kila mwaka Ngorongoro inatoa karibu shilingi milioni 600 kwa Halmashauri ya Ngorongoro ili kuweza kuendeleza sehemu hii. Pamoja na hayo inatoa utaratibu wa kutoa chakula kwa wananchi na familia mbalimbali za Ngorongoro. Kwa hiyo, niseme kwamba kwa upande wa Ngorongoro kwa kweli *NSA* kupitia bodi yake inajitahidi sana kusaidia wananchi wa Ngorongoro.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Chubi, ameondoa swali lake anasema ameshapata majibu ya maandishi na ameridhika nayo. Kwa hiyo, tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo.

Na. 91

**Mradi wa Maji Kasamwa**

**MHE. ERNEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa katika mji mdogo wa Kasamwa kuna mfumo wa maji ambao sasa hivi haufanyi kazi kabisa; na kwa kuwa baada ya kufuatilia mradi huo nimegundua kuwa mashine yake haina matatizo na yupo mlinzi anayelipwa na Halmashauri kuulinda mradi huo:-

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusu mradi huo?

(b) Kama kuna uchafuzi wa mfumo na usambazaji wa maji kwa kutolewa mabomba; je, Serikali itasaidia kurudisha mfumo huo katika hali yake ya kawaida?

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimwa Ernest Mabina, Mbunge wa Geita, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kuona kuwa miradi yote ya maji inafanyiwa ukarabati na kupata uendeshaji unaostahili kutoka kwa walengwa ili ifanye kazi ya kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yangu imeorodhesha miradi yote nchini isiyofanya kazi kwa lengo la kuifufua kulingana na upatikanaji wa fedha na Sera ya Maji ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wilaya imefanya zoezi la kuchagua miradi ambayo inaweza kujengwa na kuimarishwa kwa haraka, kwa fedha za Mradi wa Maji wa Vijijini unaofadhiliwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia. Mradi kama huu unaweza kunufaika iwapo utapendekezwa na Wilaya. Tatizo la uchafuzi wa vyanzo vya maji unatokana na makazi ya watu.

Mheshimiwa Spika, ni vema itolewe elimu ya kuwataka wanaofanya makazi kwenye vyanzo vya maji itolewe. Suala la maji katika mji mdogo wa Kasamwa Wizara yangu inalifahamu. Tunaishauri Wilaya Geita ama iuweke kwenye mapendekezo ya miradi itakayotekelezwa chini ya mradi wa maji na usafi wa mazingira unaofadhiliwa na mkopo wa Benki ya Dunia au ile inayotafutiwa kwa msaada wa Serikali ya Japan ambao utahusisha mikoa ya Mwanza na Mara.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa miradi hii imekuwa ni ya siku nyingi na haitekelezeki hasa mradi wa Kasamwa, mradi wa Nyamtukuza, mradi wa Nyahagomba pamoja na Geita Mjini kwa ujumla na watu wake wote wanakunywa maji ya visima, je, Waziri Edward Lowassa, anaweza akakubali kuja Geita na yeye tushirikiane kunywa maji ya visima? *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, kwanza mji wa Kasamwa ulikuwa unatumia maji kutoka Bwawa la Kasamwa lakini pampu ya Bwawa hilo imeharibika, kwa sababu imewekwa toka mwaka 1973.

Mheshimiwa Spika, pili maji wanayotumia maji ya visima maana yake si kama ni mabaya, tumejiridhisha kwamba maji yale yanafaa kutumika kwa matumizi ya binadamu na kuja kumthibitishia namhakikishia nitakuja Geita na mimi nitakunywa maji hayo hayo.

Na. 92

**Ujenzi wa Shule za Sekondari Serengeti**

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Serengeti wamejitolea na kufanikisha ujenzi wa Shule za Sekondari 19; na kwa kuwa shule hizo sasa zina upungufu mkubwa wa nyumba za walimu na madarasa:-

(a) Je, Serikali kwa kupitia *MMES* inatarajia kujenga madarasa mangapi na nyumba za walimu ngapi katika kipindi cha mwaka wa fedha 2004/2005 ili kutatua kero hiyo?

(b) Je, Serikali itazipatia walimu wangapi shule hizo katika kipindi hicho hicho ili kuondoa kabisa tatizo sugu la uhaba wa walimu katika shule hizo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Mnanka Wanyancha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kupitia mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari 2004 hadi 2009, Wilaya ya Serengeti imepangiwa fedha za ruzuku ya maendeleo ya ujenzi wa madarasa 2 mara shilingi milioni 7 jumla ni shilingi milioni 14 na nyumba za walimu 14, shilingi milioni 9 mara shilingi milioni 9 jumla ni shilingi milioni 126, jumla inakuwa shilingi milioni 140 kwa mwaka huu wa 2004/2005.

(b) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Serengeti inao upungufu wa walimu 33 wa shule za Sekondari. Mwaka 2004/2005 hadi sasa Wizara yangu imezipangia Shule za Sekondari za Serengeti jumla ya walimu 22, wakiwemo walimu 7 wa Stashahada ya Sayansi na walimu 15 wa Stashahada ya Sanaa. Serikali inaendelea na jitihada za kuzipatia shule hizo walimu zaidi ya kadri hali itakavyoruhuru.

Lakini napenda kuchukua nafasi hii kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa kwa kuwa ujenzi na uanzishaji wa shule katika Wilaya ya Serengeti ulijikita zaidi katika ujenzi wa madarasa bila nyumba za walimu za kutosha, walimu wengi tunaowapanga katika Wilaya hiyo hawaendi au wanaondoka na kwenda zao mara baada ya kuripoti na kukuta hakuna nyumba. Ndiyo maana katika Mpango wa Maendeleo ya Elimu Sekondari mwaka huu Wilaya ya Serengeti imepangiwa madarasa mawili tu lakini nyumba za walimu 14.

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, asante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali ya nyongeza mawili.

(a) Kwa kuwa nimekuwa kila mara natoa matatizo ya shule hizi za Serengeti na kumwomba Waziri aje sasa ni miaka mitano Waziri hajakanyaga wala Naibu Waziri katika hiyo Wilaya, je, sasa anaweza kuji-*commit* ni lini atakuja huko?

(b) Kwa sababu anajua moja kwa moja kwamba tuna matatizo ya madarasa, sasa madarasa mawili kweli yanatutosha lolote?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Kutokufika na ninaahidi naweza kuji-*commit* kufika lini, namshukuru sana kwa kunialika mara kwa mara na ni kweli sijapata nafasi, napenda kumhakikishia katika

kipindi hiki kilichobakia nitatoa umuhimu wa juu kutembelea Mkoa wa Mara kwa sababu sijafika katika Mkoa mzima. *(Makofi)*

Kuhusu shida ya madarasa nafahamu ipo isipokuwa tumeona shida ya walimu ni kubwa zaidi kuliko madarasa. Utaratibu uliotumika katika kupanga madarasa tumezingatia lengo la mwaka huu la kupeleka sekondari asilimia 35 ya wahitimu wa darasa la saba kwa kuwaongeza madarasa hayo mawili Wilaya Serengeti ukijumlisha na yale ambayo tayari walikwisha yajenga wanafikia lengo hilo la asilimia 35 bila wasi wasi.

Mheshimiwa Spika, napenda ifahamike kwamba hiyo ni mwaka huu kazi hii tutaendelea nayo kila mwaka mpaka mpango huu wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari wa miaka mitano tutakapoukamilisha.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali la nyongeza. Majibu ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri sana lakini nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa huu mgao wa *MMES* kama alivyojibu kwenye jibu lake la msingi unategemea zaidi, moja ya vigezo ni idadi ya wanafunzi waliomaliza darasa la saba bila kujali idadi za shule za sekondari zilizoko katika kila Wilaya. Je, Mheshimiwa Waziri haoni kwamba ni wakati muafaka kubadili kigezo hicho kwa sababu Wilaya nyingi zina shule nyingi, unapotoa madarasa mawili au madarasa matatu kama ilivyo kwenye Wilaya ya Mbarali, haileti uwiano sawa katika Wilaya zingine?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Estherina Kilasi, Mbunge wa Mbarali, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Naifahamu kabisa shida iliyotokea kwamba jumla ya madarasa tuliyopanga katika Wilaya ya Mbarali ukichukua na shule walizonazo, wakiyapanga yale madarasa zinabakia shule mbili au tatu. Hili tatizo nalifahamu, lakini napenda nirudie kigezo kinachotuongoza ni kupeleka sekondari asilimia 35 ya watahiniwa wa darasa la saba na kwa kigezo hiki nina hakika Mbarali itafikia. Sasa zile shule ambazo hazikupata madarasa tunawaachia wao katika Wilaya shule hizo wazipangie nyumba za walimu, katika zile nyumba za walimu zilizopangwa, basi kule ambako hakukwenda madarasa panga nyumba ya mwalimu.

Kwa vile tunafanya milioni tisa kwa kila nyumba ya mwalimu na sisi wote tunafahamu kwamba milioni tisa inaweza kufanya zaidi ya nyumba moja. Kwa hiyo, humo humo sisi tutadai ijengwe ile nyumba ya mwalimu iliyopangwa. Lakini ile *saving* ambayo inatoka na nguvu za wananchi kuongezwa, inaweza ikatumika kumalizia darasa pale ambapo alikuwa limepangwa darasa.

Na. 93

**Ujenzi wa Maabara - Sekondari ya Chalao**

**MHE. JOHN E. SINGO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilitoa msaada wa ujenzi wa maabara katika shule ya Sekondari ya Chalao, Wilayani Same, Mkoani Kilimanjaro kwa mfuko wa *ADB;* na kwa kuwa mradi huo mpaka sasa haujakamilika na mkandarasi ametoroka na kutekeleza lori lake hapa shuleni:-

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu mkandarasi huyo na ni hatua gani zimechukuliwa dhidi yake?

(b) Je, mradi huo ulianza lini na ni kwa nini Serikali imekaa kimya muda mrefu bila maelezo yoyote kuhusu kusimama kwa mradi huo?

(c) Je, mkandarasi huyo ameshakwambia miradi mingapi ya aina hiyo?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, inapenda nitoe ufafanuzi ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Maabara katika Sekondari ya Chalao ni sehemu ya mradi wa Ujenzi wa Maabara katika shule 36 nchini, kupitia Mradi wa pili wa Elimu *(Education II Project)* unaotekelezwa na Wizara yangu kwa fedha za Mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(African Development Bank).* Pamoja na ujenzi wa Maabara tatu kwa kila shule (Fizikia, Kemia na Baiolojia) pia inajengwa hosteli yenye uwezo wa kuchukua wasichana 20 na kuzipatia shule hizo vifaa vya maabara.

Mheshimiwa Spika, baada ya ufafanuzi huo napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 2001 Mkandarasi aitwaye *Tanzania Building Works (TBW)* alipewa kazi ya ujenzi wa Maabara katika shule za Sekondari saba za Chalao, Igunga, Kaliua, Oldonyosambu, King'ori, Matola na Kilangalanga. Mradi huu ulikisiwa kugharimu jumla ya shilingi 146,684,803/=. Bodi ya Zabuni ya Wizara yangu *(Elimu Tender Board)* ilimteua Mkandarasi huyo kwa taratibu zote sahihi za utoaji wa Zabuni baada ya kuridhika kuwa angekamilisha ujenzi huo baada ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni Mkandarasi huyo alionekana kuwa anauwezo wa kutosha kumudu kazi hiyo, lakini baadaye utendaji wake ulianza kuzorota na hatimaye kushindwa kabisa kuendelea na ujenzi. Serikali ilichukua hatua za kisheria kulingana ana Mkataba kati yake na Mkandarasi huyo, ikiwa ni pamoja na kumsimamisha rasmi

asiendelee na ujenzi na kusitishwa kwa Mkataba wake mwaka 2003. Wakati mkataba unasitishwa Mkandarasi huyo alikuwa amekwisha kulipwa jumla ya shilingi 18,311,971.68 na kutakiwa kurejea kiasi cha shilingi 2,189,755.02 ambazo ilionekana hajazifanyia kazi. Hatua za kisheria zinachukuliwa dhidi yake ili alipe deni analodaiwa na Serikali kwa kushindwa kumaliza kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali haijakaa kimya kuhusiana na kusimama kwa Mradi huo. Wizara yangu imeendelea kuwasiliana na Benki ya Maendeleo ya Afrika ili kuona uwezekano wa kumalizia ujenzi wa Maabara hizo. Aidha, Wizara yangu imekwisha kuwatuma Wahandisi katika shule zote saba ili kufanya tathmini ya gharama ya kumalizia ujenzi huo. Hivi sasa baada ya makubaliano na *ADB,* Zabuni zimetangazwa upya, ili kumpata Mkandarasi mwingine kwa lengo la kukamilisha ujenzi wa Maabara hizo kabla ya mwisho wa mwaka huu.

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwanza napenda niipongeze Serikali kwa hatua iliyochukua kumdhibiti Mkandarasi huyo ambaye ameitapeli Serikali.

Nina swali moja la nyongeza kuhusu wananchi ambao waliajiriwa na huyu Mkandarasi kule katika ile Shule ya Sekondari ya Chalao na Mkandarasi huyu alipotoroka wananchi wale walibaki bila malipo na wamekuwa wakidai Wizarani malipo yao. Je, sasa wananchi hao watalipwa na nani?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa John Singo, kwa pongezi alizozitoa kwa mradi huu.

Katika kujibu swali lake la nyongeza napenda nikubaliane nae kwamba, mradi huu umeingi katika matatizo. Sasa Serikali kama nilivyosema inamdai Mkandarasi shilingi milioni 2 na nina hakika hao wananchi nao wanaye mtu wanayemdai. Yeye mwenyewe amesema wanamdai yule Mkandarasi, kwa hiyo, cha kufanya ni sisi tunaomdai Mkandarasi ni kuunganika na kuendelea kumdai mpaka atapotulipa. Kwa sababu kila mtu anabeba mzigo wake, Serikali inamdai na wale wafanyakazi wanamdai, kama zile hela ambazo Serikali inamdai zinahusu wale wafanyakazi zitakavyopatikana tutaweka utaratibu wa kuwapa haki yao kama haki yao inatokana na zile ambazo Serikali inamdai huyo Mkandarasi.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa...

**SPIKA:** Samahani Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, kuna maelezo ya nyongeza kutoka Serikalini.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niongezee majibu mazuri kabisa ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, Makandarasi wote wanatawaliwa na Bodi ya Makandarasi na ningemwomba Mheshimiwa John Singo, aiombe Halmashauri husika kule ituandikie Wizara ya Ujenzi, ili tumkabili huyo Mkandarasi kupitia Bodi ya Makandarasi achukuliwe hatua. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na nyongeza iliyofanywa na Naibu Waziri wa Ujenzi, nina swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Waziri amekiri kwamba Mkandarasi huyu *Tanzania Building Works* ameshindwa kukamilisha kazi yake kwenye ujenzi wa Maabara kwenye hiyo shule iliyotajwa.

Je, kwa nini Serikali inaendelea kumkabidhi kazi zingine Mkandarasi huyu kwenye maeneo ya Serikali ikiwa ni pamoja na ujenzi katika Uwanja wa Songwe Mbeya, wakati wanajua hawezi kufanya kazi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu swali la nyongeza Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini. Lakini kabla sijamjibu napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi kwa maelezo ya ziada aliyoyatoa.

Katika kumjibu Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, napenda kusema kwamba tunamshukuru kwa taarifa aliyotupa na kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, Wakandarasi hawa wana chombo kinachowasimamia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, taarifa yake aliyotupa kwamba huyo *Tanzania Building Works* kapewa kazi nyingine huko Songwe, nina hakika wenzetu wanaowasimamia Wakandarasi Wizara ya Ujenzi nao wamesikia taarifa hii na tunashirikiana ndani ya Serikali kuona namna ya kumdhibiti Mkandarasi huyu.

Na. 94

**Ugonjwa wa Akili**

**MHE. JUMA S. KIDUNDA** aliuliza:-

Kwa kuwa ugonjwa wa akili *(Mental illness)* ni tatizo kubwa nchini na linaathiri uchumi na ustawi wa jamii kwa ujumla.

(a) Je, ugonjwa huo unasababishwa na nini?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimekuwa kikitengwa katika Bajeti kila mwaka kwenda kwenye kitengo hicho kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita?

(c) Je, ni mikakati gani imewekwa ili kuhakikisha kuwa wagonjwa wa akili wanapata huduma za tiba wanazostahili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Juma Kidunda, Mbunge wa Kilindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa akili *(Mental Illness)* unasababishwa na vyanzo vingi. Hata hivyo vyanzo hivyo vimegawanyika katika makundi matatu kama ifuatavyo:-

(i) Kurithi kutoka kwenye ukoo.

(ii) Matatizo yanayoathiri ubongo na mishipa ya fahamu:-

- Sumu mbalimbali mfano ulevi wa pombe uliokithiri, uvutaji bangi na utumiaji wa madawa ya kulevya.

- Maambukizo ya ubongo kwa virusi, bakteria na hata vijidudu vya malaria.

- Kuumia ubongo kwa kukosa hewa wakati wa moto anapozaliwa.

- Ajali mbalimbali zikiwemo za barabarani.

(iii) Matatizo ya kisaikolojia:-

- Mahusiano mabaya na watu muhimu mathalan muajiri, mke au familia.

- Wasiwasi wa usalama wa maisha au kutojiamini.

- Matatizo mengi humtokea mtu kwa wakati mmoja na kukosa mtu wa kumfariji.

(b) Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Afya ya Akili na Dawa za Kulevya Wizarani ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Mirembe na Lutindi Wilayani Korogwe, kwa miaka 2000/2001 hadi 2004/2005 zimepewa fedha kwa ujumla wake kama ifuatavyo:-

Mwaka 2000/2001 shilingi 90,687,000/=;
Mwaka 2001/2002 shilingi 129,048,780/=;
Mwaka 2002/2003 shilingi 350,881,600/=;
Mwaka 2003/2004 shilingi. 463,051,100/=; na
Mwaka 2004/2005 hadi Desemba 2004 shilingi 311,826,400/=.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina mikakati ya kuboresha Huduma za Afya ya Akili nchini. Mikakati hiyo inajumuisha mpango unaoendelea wa kufikisha huduma hizi kwenye ngazi ya msingi yaani Zahanati na Vituo vya Afya.

Mikoa ambayo tayari mpango huu umeanza kwa kushirikiana na Shirika la Uholanzi la *CORDAID* ni Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Manyara, Mwanza, Mtwara na Tanga. Mpango huu utaenezwa nchi nzima katika kipindi cha miaka mitatu ijayo. Aidha, Wizara yangu inashirikiana na Wizara nyingine za Elimu, Mambo ya Ndani, Sheria na Mambo ya Katiba na Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika mkakati huo.

Wizara yangu pia inashirikiana na Mashirika ya kujitolea kama Makanisa, Shirika la *Basic Needs* (Mtwara) na Chama cha Magonjwa ya Akili *(MEHATA)*. Wizara pia imeimarisha mafunzo ya watumishi wa fani hii ya magonjwa ya akili.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninalo swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hadhi ya magonjwa hujitokeza kwa wingi katika baadhi ya maeneo nchini, je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutueleza kwamba ugonjwa huu wa akili unajitokeza kwa wingi zaidi katika eneo gani la nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Kidunda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sina takwimu kamili za wapi magonjwa ya akili yanajitokeza kwa wingi zaidi katika nchi yetu. Lakini ambacho ninaweza kusema kwa sasa ni kwamba imeonekana kwenye Miji Mikuu ambapo dawa za kulevya zimekuwa ni tatizo kubwa, wagonjwa wa akili wamekuwa wakiongezeka kwa kasi hususan Miji kama Dar es Salaam.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina moja dogo la nyongeza la kuuliza. Kwa kuwa ugonjwa wa akili kama alivyosema unatokana na madawa ya kulevya na kwa kuwa vijana wengi wanaathirika sana na ugonjwa huu kutokana na kuvuta au kutumia dawa za kulevya.

Je, sasa inakuwaje Serikali ipo, *Anti-Corruption* ipo, dawa hizi za kulevya zinaingiaje?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, dawa za kulevya katika nchi yetu zimekuwa zikiingia kama ambavyo katika nchi nyingine zote. Isipokuwa Serikali imeweka mikakati madhubuti pamoja na kuanzisha Tume inayoratibu uthibiti wa dawa za kulevya. Tume hii imekuwa ikifanya kazi yake na inaendelea kupanga mikakati tofauti ya kuweza kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini kama unavyofahamu jambo lolote ambalo linaingiza kipato liwe la halali au la haramu, mara nyingi huwa linadumu katika jamii. Kwa hiyo, ni wajibu wetu sote katika jamii kuhakikisha kwamba tunatoa *report* kila tunapoona kwamba kuna dawa za kulevya zinaingia kupitia njia yoyote.

Na. 95

**Mahitaji ya Dawa - Kituo cha Afya cha Kabila**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA** aliuliza:-

Kwa kuwa kituo cha Afya cha Kabila kilichopo Wilayani Magu kinahudumia Tarafa nzima ya Ndagalu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza *kits* za dawa katika Zahanati hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu hutoa makasha ya dawa kwa Vituo vya Afya na Zahanati nchini kote. Hata hivyo utaratibu huu umeonekana kutokidhi mahitaji ya vituo hivi kulingana na aina ya magonjwa yaliyopo katika maeneo husika, kwani dawa za aina moja hutolewa kwa vituo vyote bila kujali mahitaji ya maeneo hayo.

Kwa kubaini upungufu huo, Wizara yangu imebuni utaratibu wa kuwawezesha wakuu wa vituo husika kuagiza dawa kulingana na mahitaji yao. Utaratibu huu unajulikana kama *indent system.*

Mheshimiwa Spika, kwa kuanzia Wizara yangu ilianza utaratibu huu kwa Wilaya zote za Mkoa wa Morogoro. Baada ya kuonyesha matokaeo mazuri, utaratibu huu utaenezwa nchi nzima. Hadi sasa Mikoa ambayo imepata mafunzo na kuanza utaratibu huu ni kama ifuatavyo:-

Kilimanjaro Wilaya zote, Arusha Wilaya zote, Manyara Wilaya zote, Mtwara Wilaya za Mtwara Vijijini, Tandahimba, Newala na Masasi,Pwani Wilaya ya Rufiji, Tabora Wilaya ya Igunga, Ruvuma Wilaya za Songea Mjini na Songea Vijijini, Iringa Wilaya za Iringa Vijijini na Mjini.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Mwanza, Kagera, Mara na Shinyanga iko katika hatua za mwisho za maandalizi ya kuanza utaratibu huu na Wilaya zote zitahusika. Maandalizi hayo ni pamoja na kutoa mafunzo kwa watumishi husika. Aidha, *MSD* tawi la Mwanza linakamilisha sehemu ya kuhifadhia dawa za nyongeza kutokana na utaratibu huu mpya.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Kituo cha Afya cha Kabila Wilayani Magu, kitafaidika na utaratibu huu mpya kwa kupatiwa dawa zinazokidhi mahitaji ya wananchi.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi tena ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa kituo hiki cha Kabila katika swali la msingi kinahudumia wananchi wengi wa kutoka Tarafa hii Ndagalu hasa wanawake na watoto, na kuwa kituo hiki ili kikamilishe kufanya kazi yake vizuri hakina mtaalam wa Maabara.

Je, Serikali sasa leo itanihakikishia vipi ili kukidhi haja ya kituo hichi cha Kabila inapelekewa mtaalam huyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Nyawazwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya hutoa Ikama ya Wataalam wanaohitajika katika vituo mbalimbali ikiwemo Zahanati, Vituo vya Afya, Hospitali za Wilaya, Hospitali za Mikoa na Hospitali za Rufaa. Kwa maana hiyo, Ikama ya Kituo cha Afya kinachozungumziwa hapa tayari ipo. Kinachohitajika sasa ni Halmashauri ya Wilaya husika kupeleka maombi yake moja kwa moja Ofisi ya Rais (Utumishi) ili waweze kupata kibali cha kumwajiri Mtaalam huyo.

Na. 96

**Uwanja wa Ndege Ibadakuli**

**MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE** aliuliza:-

Kwa kuwa ndege hutua mara mbili au tatu kwa siku katika Uwanja wa Ndege wa Ibadakuli Mkoani Shinyanga; na kwa kuwa uwanja huo hauna lami kabisa na wakati mwingine huwa na utelezi wakati mvua zinaponyesha na kusababisha ndege kuyumba:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuuwekea lami uwanja huo?

(b) Je, ni lini Serikali itaupanua uwanja huo ili ulingane na hadhi ya kutua ndege kubwa zinazochukua abiria wengi zaidi?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge wa Meatu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Kiwanja cha Ndege cha Ibadakuli kilijengwa miaka 1980 kwa ushirikiano wa Serikali na nguvu za Mkoa wa Shinyanga. Wakati huo kikiwa na ukubwa wa daraja la 2B

chenye uwezo wa kupokea ndege zenye ukubwa wa kubeba abiria wasiozidi 12. Uboreshaji wa Kiwanja hiki uliendelea hadi kufikia ukubwa wa daraja 2C ambapo ndege zenye uwezo wa kubeba abiria 19 zilihudumia kiwanja hicho.

Mheshimiwa Spika, sasa kina urefu wa mita 1600 na kiwanja hicho kina uwezo wa kupokea ndege kubwa ya aina ya *ATR 42* yenye uwezo wa kubeba abiria hadi 50. Hii ni ishara kuwa biashara ya usafiri wa anga Mkoani Shinyanga inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege ina mpango wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Katika kutekeleza mpango wa muda mfupi kiwanja cha Ibadakuli kiliwekwa tabaka la lami kwa urefu wa mita 200 katika eneo linalotumika kutua ndege *(touch down zone).*

Mheshimiwa Spika, mpango wa kuweka lami katika eneo lililobaki utaendelea kutekelezwa kwa awamu jinsi hali ya fedha itakavyoruhusu. Aidha, kiwanja cha ndege cha Ibadakuli kitaongezwa ukubwa jinsi hali ya soko la usafiri wa anga litakavyokuwa.

**SPIKA:** Hiki ni kiwanja cha Ibadakuli, mimi nafikiri mwenyewe ameridhika, inatosha.

Na. 97

**Watu Waliopata Ajali ya Treni/Meli**

**MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. JACOB D. SHIBILITI)** aliuliza:-

Kwa kuwa ajali ya treni na meli ni matukio mabaya sana ambayo ni vigumu kuyasahau kwa vile yaliuwa maelfu ya watu:-

(a) Je, Serikali ilitoa kifuta machozi cha kiasi gani kwa kila mwathirika au familia ya waliohusika kwa kila ajali yaani ile ya treni na ile ya meli?

(b) Je, Serikali imejifunza nini juu ya matukio hayo na imechukua hatua gani ili yasitokee tena?

(c) Kwa ajali za mabasi, magari, je, wahusika katika kulipa au kutoa vifuta machozi Serikali inasaidiaje inapotokea hasa kwa ajili kama ile ya basi liliotumbukia mtoni na kuua watu?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kwa ajili ya meli iliyotokea tarehe 21 Mei, 1996 katika Ziwa Victoria ya ajali *MV Bukoba,* Serikali ilitoa shilingi 500,000 kwa kila aliyefiwa na shilingi 200,000 kwa

kila aliyejeruhiwa. Aidha, kwa ajali ya treni iliyotokea tarehe 24 Juni, 2002 kati ya Stesheni ya Igandu na Msagali, Serikali ilitoa shilingi 500,000 kwa kila aliyefiwa na shilingi 100,000 kwa kila majeruhi, kama kifuta machozi.

Mheshimiwa Spika, bado tunawakumbuka wale wote waliopoteza maisha katika ajali hizo na nyingine. Tunaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema peponi roho za marehemu.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali imejifunza mengi kuhusu umuhimu wa kila wakati kujiweka tayari katika kukabiliana na majanga yatokanayo na ajali kama hizo kwa mambo yafuatayo: -

- Kuboresha na kukiimarisha Kitengo cha Maafa kilicho chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

- Kutoa mafunzo kwa watoa huduma za watumiaji wa huduma hizo kuhusu njia mbalimbali za kujiokoa na uokoaji pindi ajali zinapotokea.

- Kuelimisha umma nini cha kufanya pale matukio kama hayo yanapotokea.

- Umuhimu wa kuangalia na kuboresha Sheria zetu mbalimbali na Kanuni za uendeshaji ili zikidhi hali halisi ya leo.

- Kila wakati kuwa tayari kukabiliana na dharura.

- Kuangalia sifa za watoa huduma na ubora wa mitambo ya kutolea huduma.

- Kushughulikia malalamiko na mahitaji ya wafanyakazi kuhusu maslahi yao.

- Kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu usalama kwa wafanyakazi walio katika sehemu nyeti.

- Kuhariri vyeti vya watoa huduma wote ili kuona vinakidhi ubora kuhusu kazi wanayoifanya kutokana na ujuzi wao.

(c) Mheshimiwa Spika, ajali za barabarani zinasababisha pia maafa makubwa kwa raia pamoja na mali zao. Hivyo, kufuatana na sheria ya *Motor Insurance (Third Party) Ordinance Cap. 169,* mmiliki yeyote wa gari, wakiwemo wa mabasi ya abiria hulazimika wakati wowote kuwa na Bima ambayo itawapa haki abiria walioumia au kufariki kulipwa fidia kidogo au kifuta machozi, endapo basi walilosafiria litapata ajali. Kutokana na Sheria hii abiria waliolipia nauli ili kusafiri kwa mabasi wanakuwa na kinga ya Bima.

Hata hivyo, kwa kuwa makampuni ya Bima ndio yanayolipia fidia kwa niaba ya wamiliki wa mabasi ya abiria, sheria hii imefanya baadhi ya wamiliki wa mabasi kutokuwa waangalifu na makini kwa sababu hawawajibiki moja kwa moja kutoa fidia. Sheria hii inasimamiwa na Wizara ya Fedha. Serikali inaliangalia upya suala hili ili

kurekebisha au kuziboresha zaidi sheria husika kwa lengo zima la kupunguza ajali za barabarani.

Aidha, sheria ya Bima inashauri watu binafsi wajiwekee Bima ili kupata fidia ya kutosha pale ajali inapotokea.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa matukio haya makubwa makubwa wahanga wake wanapewa fidia na tukiangalia mwaka jana Wilaya ya Misungwi kulikuwa na ajali ya basi kutumbukia kwenye Mto Wami na zaidi ya watu 20 walifariki. Katika Wilaya ya Geita kuna watu walizama kwenye mitumbwi wakitoka Nkome kuelekea Visiwa vya Butwa na Isimacheli. Watu hao wote bado hawajalipwa fidia. Je, fidia hii inatolewa kwa vyombo vikubwa tu bila kuangalia hata vyombo hivi vidogo vidogo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri katika majibu yake ya msingi kwamba fidia inalipwa na aliyemiliki kile chombo kilichofanya ajali na hasa baada ya Mahakama kuthibitisha kwamba yule mwenye chombo ndiye aliyesababisha ajali. Ile hukumu ya Mahakama ndio inaambatishwa na madai ya yule ambaye anatakiwa alipwe fidia na madai yanafanywa na yule mwenyewe mhusika. Kwa hiyo, hawa ambao walipata ajali ya mabasi wanatakiwa wao wenyewe ndio wajaze *form* kudai fidia.

Kuhusu vyombo vidogo vidogo vile ambavyo havina Bima, sasa inakuwa ni vigumu sana kwa Bima kulipa fidia kwa mtu ambaye hana Bima. Mitumbwi na malori, hayana leseni za kubeba abiria, hivyo ajali ikitokea abiria hawawezi kudai fidia kwa vile walisafiri katika vyombo ambavyo havina leseni ya kubeba abiria. Kwa hiyo natoa tahadhari pale inapowezekana kuepuka kupanda vyombo ambavyo havina Bima wananchi wanashauriwa kuepuka.

Na. 98

**Rushwa Ndani ya Jeshi la Polisi**

**MHE. MARTHA M. WEJJA** aliuliza: -

Kwa kuwa rushwa ni tatizo katika Taifa letu na kwa bahati mbaya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ndiyo inalaumiwa kwa kupokea rushwa:-

(a) Je, kwa nini Wizara inapopewa taarifa kuwa askari fulani ni mla rushwa huwa anahamishiwa sehemu nyingine badala ya kuchukuliwa hatua?

(b) Je, Serikali itatumia njia gani za makusudi ili kupunguza au kuondoa kabisa tatizo hilo hasa katika kitengo cha *Traffic?*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Wejja, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa Wizara yangu ni miongoni mwa Taasisi za Umma zinazolalamikiwa na wananchi kuhusu suala la askari polisi kupokea rushwa. Hata hivyo si kweli kuwa Wizara inapopewa taarifa kuwa askari fulani ni mla rushwa huwa anahamishiwa sehemu nyingine badala ya kuchukuliwa hatua. Ukweli ni kwamba Wizara ikipata taarifa ya askari kujihusisha na vitendo vya rushwa uchunguzi wa kina hufanyika na akithibitika kujihusisha na vitendo vya rushwa huchukuliwa hatua za kinidhamu zinazostahili ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi jeshini na baadaye hufunguliwa mashtaka Mahakamani kujibu mashtaka ya jinai.

Aidha, malalamiko yanaposhindwa kuthibitishwa askari huyo pamoja na kuchukuliwa hatua zingine za kinidhamu, hubadilishwa kazi aliyokuwa anafanya awali na kupangiwa kazi nyingine ambayo haina vishawishi vingi vya rushwa na hivyo kupunguza malalamiko ya wananchi na kuongeza ufanisi wake katika kazi.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuondoa tatizo la kupokea rushwa katika vikosi vyote vya jeshi la polisi, ikiwa ni pamoja na Kikosi cha Usalama Barabarani *(Traffic)* Serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na hizi zifuatazo: -

(i) Kuelimisha umma wa Watanzania waelewe kuwa huduma za polisi hutolewa bure. Hivyo wasikubali kutozwa fedha. Elimu hiyo hutolewa kwa kupitia *radio, television* na kubandika mabango na vipeperushi mbalimbali kwenye vituo vya polisi.

(ii) Kuendesha semina na warsha mbalimbali kwa viongozi wa ngazi mbalimbali ndani ya Jeshi la Polisi juu ya kero ya rushwa, haki za binadamu na utawala bora. Elimu wanayopata viongozi hawa huwasaidia katika kuwafundisha askari walio chini yao katika mabaraza ili nao waweze kuelewa madhara ya rushwa na kujiepusha na maovu ya rushwa.

(iii) Kuboresha mazingira ya kazi ya askari Polisi, hasa kuwapatia vitendea kazi, hivyo kuachana na taratibu zinazoashiria rushwa za kuwadai wananchi watoe fedha za kuhudumia wahalifu kama usafiri, *stationaries,* chakula, matibabu, dhamana na kadhalika. Mkakati huu unatekelezwa kwa awamu kutegemea hali ya Bajeti yetu kila mwaka.

(iv) Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maeneo ya kazi ili kuwabaini mapema askari wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na kuwachukulia hatua mara moja.

(v) Kuwahamasisha wananchi ili watoe ushirikiano wa karibu kwa Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kuzuia Rushwa na vyombo vingine vya dola mara wanapohisi kuwa kuna vitendo vinavyoashiria kudaiwa rushwa ili askari wanaohusika wakamatwe mara moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba mapambano dhidi ya askari wala rushwa ndani ya Wizara yangu ni makali na hakuna huruma wala msamaha kwa wanaoendesha ufisadi wa aina hii.

Kati ya mwaka 2000 hadi 2004, askari 60 wamefukuzwa kazi na kufikishwa Mahakamani kwa tuhuma za rushwa. Mapambano haya yanaendelea na tunaomba wananchi wenye taarifa za askari wanaowasumbua kwa kudai rushwa watuletee taarifa zao na tunaahidi tutachukua hatua za haraka na kwa makini.

**MHE. MARTHA M. WEJJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ninaomba kuuliza swali moja au swali lifuatalo:-

Ni hivi karibuni alitoa tamko kwamba askari asimtereshe kondakta au dereva kuzungumza naye chini. Lakini hicho kitendo hakikuchukuliwa hatua na bado askari wafanyakazi ya kuteremsha wahusika chini na wanazungumza nao.

Je, Wizara yake inachukua hatua gani ili hicho kitendo kikomeshwe, maana yake nje ya hapo rushwa haitaisha, kwa sababu anapomteremsha konda na kondakta anatoka na gazeti lake chini ina maana ana honga. Hicho kitendo kitakomeshwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Wejja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Wizara yangu inatoa maelekezo kwa Askari wa Usalama Barabarani wafanye kazi kwa uwazi na uwazi maana yake ni kwamba anapolisimamisha basi barabarani ahojiane na dereva na kondakta pale pale ndani ya basi wakati watu wote wanasikia na wanaona, kama anamtoza adhabu ya papo kwa papo itolewe pale kila mtu anaona. Kitendo cha kuteremka na kwenda nyuma ya basi au kichakani tumepiga marufuku na mtu yeyote pamoja na Mheshimiwa Mbunge jambo kama hilo likitokea tupe taarifa na sisi tutaifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba Watanzania tusilalamike lalamike tu hebu fanyeni kweli, leteni taarifa za kweli na sisi tutafanya kweli.*(Makofi)*

Na. 99

**Magunia ya Kufungia Tumbaku**

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na utatanishi juu ya gharama za magunia ya kufungia tumbaku wanayotozwa wakulima kutoka kwa kampuni zinazonunua tumbaku ambapo kila mtumba hutozwa thamani inayolingana na kilo 2 bila kujali daraja la tumbaku iliyouzwa:-

(a) Je, kampuni zinazonunua tumbaku huwauzia wakulima magunia hayo kwa bei gani?

(b) Kwa kuwa kampuni hizo huchukua pamoja na magunia wanaponunua tumbaku, je, huko sio kumdhulumu mkulima maskini?

(c) Je, ni nini gharama halisi ya magunia hayo na mkulima anafaidika vipi na gharama hizo?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ufungashaji wa tumbaku kwa ajili ya mauzo hufanywa na wakulima kwa kutumia vitambaa maalumu vya magunia vyenye urefu wa mita tatu ambavyo hugawanywa katika vipande viwili vilivyo sawa. Vitambaa hivyo hutosha kufunga mtumba wa tumbaku wenye uzito wa kilo 50. Aidha, uzito wa vitambaa hivyo ni kilo moja na uzito huo hukatwa kwenye uzito wote wa mtumba wakati wa upimaji katika eneo la ununuzi ili kupata uzito halisi wa tumbaku anayeuza mkulima kwenye mtumba huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa gharama za vitambaa vya kufungashia tumbaku hutofautiana mwaka hadi mwaka, katika msimu wa mwaka 2003/2004 kwa mfano, bei ya mita moja ya kitambaa kipya ilikuwa shilingi 560/= ambapo mkulima alihitaji jumla ya shilingi 1,680/= kupata mita tatu za kitambaa kinachotosha kufungashia mtumba mmoja wa tumbaku wa kilo 50.

Aidha, kwa kuwa upo utaratibu uliokubalika hapa nchini wa kurudia kutumia vipande vya vitambaa hivyo kwa wastani wa misimu mitatu kabla havijachakaa kabisa, wanunuzi wa tumbaku huvirudisha vitambaa hivyo vya magunia kwa wakulima kupitia Vyama vyao vya Ushirika vya Msingi baada ya kuvifukizia dawa. Wakulima hutakiwa kuchangia gharama kidogo ya uchukuzi wakati wa kumrudisha vitambaa hivyo hadi kwenye Vyama vya Msingi. Gharama halisi ya vitambaa hivyo vilivyokwishatumika katika msimu uliopita wa 2003/2004 ilikuwa shilingi 200/= kwa vipande vyenye jumla ya mita tatu.

Gharama hizi za vitambaa vya magunia ya kufungashia tumbaku kama zilivyo gharama nyingine za uzalishaji ni moja ya vigezo muhimu ambavyo hutiliwa maanani katika Halmashauri ya Tumbaku yaani *Tobacco Council* wakati wa kujadiliana na kupanga bei ya mkulima kwa zo la tumbaku.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utaratibu huu nilioueleza, kampuni za ununuzi wa tumbaku hazichukui moja kwa moja vitambaa vya magunia ya kufungashia tumbaku kwa sababu vitambaa hivyo hurejeshwa kwa wakulima kusudi vitumike wakati wa msimu mwingine wa ununuzi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha kwa hiyo, tunaendelea na shughuli nyingine, Mheshimiwa Isaac Cheyo, ulitaka Mwongozo wa Spika, nafasi ndio hii sasa.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimeomba mwongozo wa Spika nikasema kwamba siku ya Jumatatu nilikuwa nimearifiwa kwamba swali langu litajibiwa siku ile. Lakini kwa sababu ya utaratibu wako ukasema kwamba muda hautoshi na hilo swali litajibiwa siku nyingine na siku nyingine nimeisubiri kwa muda mrefu sana. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haijafika.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Mheshimiwa mwenzangu pale yeye jibu lake likatoka kesho yake, nikavuta subira nikidhani kwamba jana lingetoka, halitoka na leo sijaliona.

Mheshimiwa Spika, lakini swali ambalo nataka kuuliza ni kwamba ulisema utalipangia...

**SPIKA:** Aaah, nimeshakuelewa.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Utalipangia siku na Mheshimiwa Waziri atalijibu, mpaka sasa hivi sijapata jibu lakini kwa kufuatana na vyombo vya habari hilo jibu limeshatoka, liko hapa. Sasa nashindwa kujua ni taratibu gani hizo tena ambazo zimeanza kutokea kwenye Ofisi yako kwamba Wabunge hawajajibiwa ndani ya Bunge swali linatoka kwenye vyombo vya habari na inaonekana Waziri kajibu kama ilivyoandikwa hapa.

**MBUNGE FULANI:** Duh!

**SPIKA:** Aaaah! Hata mimi siwezi kujua vyombo vya habari vimepata wapi majibu haya lakini mimi nilidhani ulitaka kumhoji Spika kwamba aliahidi kwamba atalipangia swali hilo siku nyingine na bado halijapangiwa.

**MHE. ISAAC M. CHEYO:** Ndiyo Mheshimiwa Spika.

**SPIKA:** Nadhani hiyo ndiyo inayonihusu. Basi napenda nikuhakikishie kwamba katika Ofisi ya Spika kuna Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge ndiye anayemsaidia Spika kupanga mambo haya yanayokuja kwenye *Order Paper.* Ulipouliza asubuhi ameniletea taarifa kwamba yeye Mkurugenzi wa Shughuli za Bunge swali la Mheshimiwa Isaac Cheyo amelipatia nafasi kwenye *Order Paper* ya kesho tarehe 11 Februari, 2005. Sasa huyo mhalifu aliyelipeleka kwenye magazeti tutasaidiana kumtafuta lakini bado litajibiwa tu ili lijulikane limetoka kwako. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Kwa kuwa hata siku ile Mheshimiwa Mgana Msindai, aliuliza vipi mbona maswali yetu hayakujibiwa, napenda niwasomee Kanuni namba 4(2) kinasema: "Spika ataongoza kila kikao cha Bunge na ndiye mwenye mamlaka ya kuamua mambo yanayoweza kuzungumzwa Bungeni."

Kwa hiyo, Spika akiamua kwamba muda wa maswali umekwisha ndio umekwisha au akisema maswali ya nyongeza yametosha ndio imetosha au akisema Muswada fulani hautaingia kwenye *Order Paper* mpaka mkutano ujao ndio itakuwa hivyo. Ni kama tunavyokuwa na Waziri wa *Management* ya Utumishi wa Umma, Spika ni mwenye dhamana ya *management* ya shughuli za Bunge lazima shughuli ziwe *managed* ili kusudi ziende vizuri kwa utaratibu unaotakiwa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, naomba tushirikiane na Spika katika *management* ya shughuli za Bunge. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Muda wa miongozo umekwisha, tunaendelea. *(Kicheko)*

Taarifa za vikao vya Kamati kwa siku ya leo, Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nchi za Nje, Mheshimiwa Dr. William Shija, anawaarifa wajumbe wa Kamati yake kwamba kutakuwa na kikao kuanzia saa tano asubuhi hii katika chumba namba 211, ghorofa ya pili.

Kamati nyingine ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, anawatangazia wajumbe wake kwamba kutakuwa na kikao mara tu baada ya kuahirishwa kwa kikao cha Bunge asubuhi hii katika Ukumbi wa Habari.

Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dr. John Malecela, anaomba wajumbe wake wakutane chumba namba 131, ghorofa ya kwanza mara baada ya kipindi hiki cha maswali.

Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anne Makinda, anawaomba wajumbe wa Kamati hii wakutane saa tano asubuhi hii kwenye ukumbi namba 231, ghorofa ya pili.

Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa William Shellukindo, anaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo Alhamisi tarehe 10 Februari, 2005 saa tano asubuhi, chumba namba 432, ghorofa ya nne.

Kamati ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Omar Kwaangw', anawatangazia wajumbe wake kwamba kutakuwa na kikao leo tarehe 10, saa tano asubuhi Ukumbi namba 227, ghorofa ya pili.

Matangazo ya Kamati yanaishia hapo lakini nimeombwa na Mheshimiwa Raphael Mlolwa, niwasomee ujumbe ufuatao kwamba kutakuwa na Misa ya kumwombea Marehemu Frank Michael Mussati, katika Kanisa Kuu la Katoliki hapa Dodoma

*(Cathedral)* kesho Ijumaa, tarehe 11 Februari, 2005, saa 12.30 asubuhi. Waheshimiwa Wabunge watakaokuwa na nafasi ya kuhudhuria ibada hiyo wanakaribishwa.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper.*

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa mwaka 2005
### *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria uitwao *The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005* pamoja na mabadiliko yaliyoambatishwa katika jedwali la orodha ya mabadiliko, sasa usomwe mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nianze kwa kuishukuru Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe kwa kuupitia na kuuchambua Muswada huu na kwa ushauri mzuri iliyotoa wa jinsi wa kuboresha maeneo mbalimbali wa Muswada huu. Ushauri huo umetusaidia sana katika kuuboresha na hivyo kuwezesha uwasilishwe mbele ya Bunge lako Tukufu asubuhi hii. Tunawashukuru kwa dhati wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kazi nzuri waliyofanya na kwa ushirikiano waliotupatia.

Mhehsimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kufanya marekebisho katika sheria sita mbalimbali zifuatazo:-

Sheria ya kwanza ni Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001 *(The Education Fund Act, 2001).* Sheria ya pili ni ya *The Merchandise Marks Act, 1963.* Sheria ya tatu ni Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 *(The Cooperative Societies Act, 2003).* Sheria ya nne ni Sheria ya Mwenendo wa Mashtaka ya Jinai ya mwaka 1985 *(The Criminal Procedure Act, 1985).* Sheria ya tano ni Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997 *(The Value Added Act ya 1997)* na Sheria ya sita ni Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 *(The Tanzania Investment Act, 1997).*

Mheshimiwa Spika, sheria ya kwanza inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Mfuko wa Elimu *(The Education Fund Act, 2001).* Sheria hii inafanyiwa marekebisho katika maeneo kadhaa ili kuondoa migongano na mwingiliano katika utekelezaji wake sambamba na Sheria ya Kodi ya Mapato ya mwaka 2004 ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wake na kuondoa upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yanayopendekezwa kufanywa katika Kifungu cha 6 ni ya kiuandishi tu kwa ajili ya kuondoa neno *objects* na badala yake kuweka neno *objectives* ambalo kimantiki na maudhui ndio neno lililokusudiwa katika sheria.

Mheshimiwa Spika, pili, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Kifungu cha 8(2) cha sheria hii kwa ajili ya kuipa Mamlaka ya Mfuko wa Elimu uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Imedhihirika kwamba haupo utaratibu unaoiwezesha Mamlaka ya Mfuko wa Elimu kutekeleza majukumu yake nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya kuongeza Aya ya (g) katika Kifungu cha 8(2) kutaiwezesha Mamlaka hiyo kuteua mawakala wa ukusanyaji michango *(collection agents).* Serikali inaamini mawakala hawa wataisadia Mamlaka kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa michango na hivyo kuwawezesha wachangiaji kuchangia Mfuko wa Elimu katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili litawapunguzia wachangiaji usumbufu wa kupeleka michango yao Makao Makuu ya Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu linalokusudiwa marekebisho linahusu uhusiano kati ya Mamlaka ya Mfuko wa Elimu na Mifuko ya Elimu iliyoundwa chini ya Serikali za Mitaa. Kama Waheshimiwa Wabunge watakavyokumbuka, madhumuni ya mfuko huu ni kuwafikia wananchi nchi nzima. Sheria hii ilivyo sasa haitoi fursa kwa Mamlaka ya Mfuko wa Elimu kushirikiana na Halmashauri za Mitaa. Kwa ajili hiyo, inapendekezwa kuongeza Kifungu kipya cha 10(a) ambacho kitaelezea ushirikiano kati ya mfuko na Halmashauri zetu katika ngazi zote kuanzia kusaidia Elimu ya Msingi, Elimu ya Sekondari na Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, eneo la nne linalopendekezwa kufanyiwa marekebisho katika sheria hii ni Kifungu cha 12 kwa ajili ya kupanua wigo wa michango. Inapendekezwa kuweka masharti mapya ya utoaji wa Hati za Wachangiaji *(Certificate of Education Appreciation)* pamoja na masharti mapya ya kupata nafuu ya kodi inayoendana na hati hiyo.

Kuhusu upanuaji wigo wa michango, inapendekezwa sasa iruhusiwe pia michango ya mashine na vifaa vingine kama vile mabati, *cement,* madawati na kadhalika badala ya michango ya fedha na mitambo peke yake inayotambuliwa sasa na sheria hii.

Mheshimiwa Spika, vile vile inapendekezwa kuwa michango inayotambuliwa ilengwe kwa wanafunzi wahitaji yaani wale ambao wazazi au walezi wao hawajiwezi ili mradi wasiwe na uhusiano wa damu na mchangiaji.

Aidha, inapendekezwa kuwekwa masharti mapya ya nafuu ya kodi ambazo sasa nafuu ya Ushuru wa Forodha inafutwa. Hata hivyo, napenda kusisitiza kwamba nafuu ya Kodi ya Mapato na nafuu ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* itaendelea kuwepo. Aidha, inapendekezwa kwamba endapo mchangiaji ataweka masharti katika mchango wake, Mamlaka itakuwa na uwezo kama itaona inafaa kutoa masharti kwa mchangiaji huyo kuhusu nafuu ya kodi atakayopata. Mathalani Mamlaka yaweza kumtaka mchangiaji huyo kuongeza kiwango cha mchango wake kabla ya kumpa mchangiaji huyo haki ya kupata nafuu ya kodi.

Mheshimiwa Spika, marekebisho mengine yanayopendekezwa kufanywa yanahusu Fungu la 12 ili lieleweke vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa. Inapendekezwa kufuta maneno yaliyomo katika sheria yanayosema *shall be deemed to have commit an act of default* na badala yake kutamka bayana kwamba matumizi mabaya ya *Certificate of Education Appreciation* litakuwa ni kosa la jina. Ilivyo sasa Kifungu hicho hakitamki kosa hilo kwa wazi.

Vile vile inapendekezwa kuweka utaratibu wa kiutawala wa kushughulikia kosa hili kwa kutumia Sheria za Kodi kwa kuzipatia mamlaka zinazohusika mamlaka ambayo tunaita *powers compound the offence* unaotekelezwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato pamoja na utaratibu wa kufuta haki zinazotokana na hati ambayo haijatumika ndani ya muda uliowekwa. Baada ya marekebisho haya kufanywa, inapendekezwa Kifungu cha sasa cha 7 kifutwe.

Mheshimiwa Spika, sheria ya pili, inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya *Merchandise Marks* ya mwaka 1963 kwa ajili ya kuongeza adhabu kwa kosa la kughushi alama za biashara zilizotolewa kwa mujibu wa sheria hiyo. Itakumbukwa kwamba katika Mkutano wake wa Kumi na Saba, Bunge hili lilipitisha marekebisho katika Sheria ya Alama za Biashara na Huduma *(Trade and Services Marks)* na Sheria Na.12 ya mwaka 1986 na pia katika Sheria ya Kanuni za Adhabu *(Penal Code)* na kuongeza adhabu kwa makosa ya kutumia udanganyifu alama za bidhaa na huduma.

Kwa vile Sheria ya *Merchandise Marks* ina makosa yanayofanana na makosa yaliyopo katika sheria zilizofanyiwa marekebisho ili kuondokana na adhabu zake ambazo ni hafifu, inapendekezwa kwamba sasa sheria hii nayo ifanyiwe marekebisho katika vifungu vya 3, 6 na 12(3) kwa kuongeza adhabu za makosa kama hayo.

Mheshimiwa Spika, pendekezo hili litazifanya adhabu hizo zifanane na zile zilizopo katika sheria nilizozitaja. Adhabu inayopendekezwa ni faini isiyozidi shilingi 50,000,000 na isiyopungua 10,000,000 au kifungo jela cha muda usiopungua miaka minne au usiozidi miaka 15 au adhabu zote mbili yaani faini na kifungo kwa pamoja. Hili ni kutokana na uzito wa makosa haya.

Mheshimiwa Spika, sheria ya tatu inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003. Sheria hii inafanyiwa marekebisho katika Fungu la 2 linalohusu tafsiri ya maneno yaliyotumika katika sheria hiyo.

Marekebisho haya yanafanywa ili kuzingatia masharti ya Kifungu cha 21(2) cha sheria hii kinachotoa fursa kwa Vyama vya Ushirika kuingia ubia na Mashirika binafsi au Mashirika ya umma pale ambapo inaonekana inafaa kwa ajili ya kuendesha biashara au shughuli za kiuchumi kwa ufanisi zinazohusisha vyama viwili vya ushirika au zaidi.

Mheshimiwa Spika, sheria ya nne inayopendekezwa kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997. Waheshimiwa Wabunge, watakumbuka kwamba katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2004 *(The Finance Act, 2004)*

Sheria ya Ushuru wa Forodha ilifanyiwa marekebisho ili kutoa msamaha wa kodi kwa vifaa vya aina ya *windmills.*

Uamuzi huo ulifikiwa baada ya Serikali kutambua umuhimu wa kutotoza kodi vifaa mbalimbali pamoja na *windmills* vinavyonunuliwa na wananchi kwa ajili ya miradi yao ya maendeleo. Sambamba na uamuzi huo, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997 nayo ilistahili ifanyiwe marekebisho katika Jedwali la Pili ili kutoa msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa *windmills* zinazokusudiwa kutumika katika miradi ya maji, kilimo cha umwagiliaji na ufugaji wa samaki, mifugo na kadhalika.

Mhehsimiwa Spika, hivyo ili kuondoa upungufu huo, inapendekezwa kuongeza Aya mpya ya 21 na 22 katika Jedwali la Pili na Aya mpya ya 24 katika Jedwali la Tatu la sheria hiyo. Pia inapendekezwa kuongeza Aya mpya ya 21 katika Jedwali la Pili ili kutoa nafuu ya kodi kwa *wind generators* na *liquid elevators.*

Mheshimiwa Spika, kwa madhumuni hayo hayo ya kutoa unafuu wa kodi kwa vifaa mbalimbali vinavyonunuliwa na wananchi kwa ajili ya kujiletea maendeleo, inapendekezwa kupitia Muswada huu kuifanyia marekebisho Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mwaka 1997 kwa kuongeza hiyo Aya ya 22 katika Jedwali la Pili la sheria hiyo ili kutoa msamaha wa Kodi ya *VAT* kwa vifaa vya umeme wa mionzi ya jua *(Solar Energy Gadgets). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vifaa vinavyopendekezwa kupatiwa nafuu ya Kodi ya *VAT* ni vingi ni kama vile *battery* za *solar,* taa za umeme wa *solar, pump* za maji zinazoendeshwa kwa *solar* na vifaa vingine vya kuendesha *pump* hizo zitakazotumika kwa ajili ya shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji wa samaki, ufugaji wa mifugo na hivyo kumwongezea kipato mkulima na mfugaji.

Aidha, inapendekezwa kufanya marekebisho katika Sheria ya Ushuru wa Forodha ya mwaka 1976 ili kuondoa Ushuru wa Forodha kwa vifaa hivyo vya *solar.* Hivi sasa *battery* za *solar* zinatozwa ushuru wa kiwango cha asilimia 25 na taa za umeme wa *solar* zinatozwa ushuru wa 10%.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo kutokana na Mkataba wa Ushuru wa Forodha wa Afrika Mashariki ulioanza kutumika tarehe 1 Januari, 2005, marekebisho haya yanapaswa kukubalika na washiriki wengine wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itachukua hatua ya kuwasiliana na washiriki hao ili tuweze kupata nafuu hiyo kwa manufaa ya wananchi wetu mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, lengo la msamaha huu ni kupunguza gharama za ununuzi wa vifaa hivi ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kupata huduma za nishati hasa wale wanaoishi katika maeneo ambayo kwa muda mrefu ujao gridi ya Taifa ya umeme haitafika.

Mheshimiwa Spika, naamini Bunge lako Tukufu litakubaliana na Serikali kwamba mapendekezo haya katika eneo hili la Muswada ni mwanzo mzuri wa kuweka mkakati wa uhakika katika kupambana na umaskini hasa ikizingatiwa kuwa nishati ni nyenzo muhimu katika maendeleo ya watu wetu na nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria ya mwisho lakini si kwa umuhimu wake ni Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997. Sheria hii inafanyiwa marekebisho katika Fungu la 19(2) na kuongeza Kifungu kipya cha tatu.

Mheshimiwa Spika, kwanza inapendekezwa kukifanyia marekebisho kifungu kidogo cha pili cha 19 kwa ajili ya kuweka sharti kwamba vivutio vinavyotolewa katika haki ya uwekezaji vitadumu kwa kipindi cha miaka mitano tu ili kuondoa tafsiri kwamba vivutio vyote ni vya kudumu na hivyo havina ukomo. Pili inapendekezwa kuongeza kifungu kipya cha tatu katika fungu la 19 kwa ajili ya kutoa fursa kwa mwekezaji anayepata nafuu ya kodi kutokana na hati ya uwekezaji kurejea kwenye mfumo wa kodi wa kawaida kama ataona kwamba mfumo huo wa kodi wa kawaida ni wa nafuu kwake. Kutokana na maboresho katika mfumo wa kodi yanayoendelea hapa nchini inawezekana mfumo wa kodi wa kawaida ukatoa nafuu zaidi kwa wawekezaji kuliko nafuu anayopewa mwekezaji chini ya hati ya uwekezaji aliyopewa.

Mheshimiwa Spika, ikitokea hali hiyo inapendekezwa ndani ya kipindi cha miaka mitano tangu hati ya uwekezaji itolewe mwekezaji huyo aweze kuchagua utaratibu ulio na nafuu zaidi kwake. Baada ya maelezo haya napenda kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii na kupitia kwako kuwashukuru Wabunge wote kwa kunisikiliza. Baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imetolewa na imeungwa mkono,wasemaji waliojiandikisha hadi sasa kwa Muswada huu ni wawili tu, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu na Mheshimiwa Omar S. Kwaangw'. Orodha bado iko wazi lakini kama kuna mawazo kwamba wanatosha basi tutaendelea hiyo. Sasa namuita msemaji wa Kamati iliyochambua Muswada huu na msemaji huyo ni Mheshimiwa Mwanne I. Mchemba. *(Makofi)*

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA (k.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako naomba nitoe salamu za rambirambi kwa niaba ya Kamati ya Sheria, Katiba na Utawala. Awali ya yote niungane na wenzangu waliotangulia na kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuchangia nitoe salamu za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Frank Mussati na familia ya Mheshimiwa Ntagazwa kwa kufiwa na mkewe. Pia nitoe salamu za rambirambi kwa wote waliopatwa na misiba kwa nyakati tofauti.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa salamu hizo naomba sasa nianze kutoa maoni ya Kamati ya Sheria, Katiba, Utawala kuhusu Muswada wa sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali.

Mheshimwa Spika, kwa mujibu wa kanuni namba 7(2) kanuni za Bunge toleo la 2004 naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria, Utawala kuhusu Muswada wa Sheria ya marekebisho ya sheria mbalimbali wa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, tarehe 25 Januari, 2005 Kamati ilikutana Dar es Salaam na kupokea maelezo ya Serikali kuhusu mapendekezo yaliyokusudiwa katika sheria hiyo, maelezo hayo yaliwasilishwa na Mwanasheria Andrew Chenge, Mbunge Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kama alivyozungumza mtoa hoja, Muswada huu ulilenga kufanya marekebisho katika sheria sita zilizotajwa hapo juu.

Mapendekezo ya marekebisho ya sheria ya uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997 *(Tanzania Investment Act 1997)* haya yalifikiriwa pamoja na mapendekezo ya sheria zilizoainishwa kwenye Muswada katika kikao cha Kamati.

Mheshimiwa Spika, katika sheria ya mwenendo wa mashitaka ya jinai ya mwaka 1985 kamati inashauri kuwa iwapo masharti ya vifungu 80 na 90 yataondolewa kuiwezesha ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka kuundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamahuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Serikali iangalie uwezekano wa kuwepo haki ya kuendesha mashitaka binafsi yaani *Private Prosecution.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ya ongezeko la kodi ya thamani ya mwaka 1997 *(The Value Added Tax 1997)* pamoja na dhana ya kupiga vita umaskini inayojitokeza katika marekebisho ya sheria hii Kamati inadhani kuwa utaratibu wa kumtaka mkulima anayenunua jenereta na pampu za maji kwa madhumuni ya kilimo cha umwagiliaji maji, uvuvi au ufugaji apate kwanza barua kutoka kwa Mkurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na kuiwakilisha Mamlaka ya Mapato Tanzania ikieleza matumizi ya vifaa hivyo ni utaratibu mgumu kiutekelezaji na utakuwa na usumbufu mkubwa kwa mkulima wa kawaida. Hivyo, Kamati inashauri kuwa Serikali isiweke vikwazo katika suala hili ili kuwawezesha wakulima wengi wajiendeleze kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001 pamoja na kamati yangu kukubaliana na mapendekezo yaliyokusudiwa ilibainika kuwa kuna Watanzania wengi wenye nia ya kuchangia katika maeneo mengine nje ya elimu kama ya Yatima, Walemavu na kadhalika. Kwa mantiki hiyo kamati inashauri kuwa ni vema Serikali iweke utaratibu mwingine wa kisheria kuwawezesha watu wa namna hiyo kuchangia maendeleo ya nchi katika kila uwanja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria ya alama za bidhaa ya mwaka 1963 yaani *The Merchandise Marks of 1963* Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali la kuongeza adhabu kwa makosa ya kutumia alama za bidhaa za udanganyifu. Hata hivyo kutokana na uzoefu uliopo wa wafanyabiashara kadhaa kujinufaisha kwa mtindo huo kama vile kusafirisha bangi kwa nembo ya majani ya chai Kamati inaona kuwa adhabu

iliyokusudiwa ni ndogo, hivyo inashauri iongezwe na kufikia ama kiwango cha miaka mitano au faini ya Shilingi 5,000,000 au vyote kwa pamoja na Mahakama ipewe uhuru wa kuamua adhabu itakayoona inafaa.

Mheshimiwa Spika, katika sheria ya uwekezaji Tanzania ya mwaka 1997 Kamati inashauri kuwa Serikali ikiandika vizuri kifungu kinachofanyiwa marekebisho ili dhana iliyoelezwa hapa kati ya mmiliki mali na mwekezaji zisijikanganye. Hizi ndizo sheria ambazo Kamati yangu ilizotolea ushauri, hata hivyo yale ambayo sikuyaongelea natumaini Wajumbe wa Kamati yangu watakao pata fursa ya kuchangia watajaribu kujazia upungufu huo.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nimalizie kwa kukushuru wewe na ofisi yako kwa ujumla kwa kufanikisha shughuli za Kamati kwa wakati uliyopangwa. Aidha napenda nimshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge, Mbunge Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wataalam wake wote kwa kushirikiana vema na kamati hii wakati wote tulipojadili Muswada huu. Kipekee naomba niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kujituma wakati wote na kutoa michango yao ya kina ambayo imesaidia sana kuboresha Muswada huu. Naomba niwatambue kwa kuwataja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Athumani S.M. Janguo, Mbunge Mwenyekiti, Mheshimiwa George Malima Lubeleje Mbunge Mwenyekiti, Kingunge Ngombale Mwiru Mbunge, Mjumbe, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mbunge Mjumbe, Mheshimiwa Rosemary Nyerere, Mbunge Mjumbe, Mheshimiwa Zahor Juma Khamis, Mbunge Mjumbe, Mheshimiwa Khamis Salum Ali, Mbunge Mjumbe, Mheshimiwa Ramadhani Khalfan Mbunge Mjumbe, Mheshimiwa Juma S. Nh'unga, Mbunge, Mheshimwa Ruth Msafiri, Mbunge, Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mbunge, Mheshimiwa Chifu Abdallah Said Fundikira, Mbunge, Dr. Willbrod Slaa Mbunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama Mbunge, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge na ndiyo mimi ninayesoma, Mheshimiwa George F. Mlawa Mbunge, Mheshimiwa Raynard Mrope, Mjumbe, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mbunge, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, Mbunge, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mbunge, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mbunge na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mbunge.

Napenda pia niwashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ernest Zulu, Charles Mloka na Aggrey Nzowa, kwa kuihudumia Kamati hii wakati wote wa vikao vyake na kutayarisha maoni ya Kamati mapema.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na ninaomba kuwasilisha kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GRACE S. KIWELU (k.n.y. MHE. DR. WILLBROD P. SLAA - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA):** Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa *Written Laws Miscellaneous Amendment Act* ya 2005 yaani Muswada wa Marekebisho ya Sheria mbalimbali za mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kukushukuru kwa nafasi kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa kanuni na kifungu cha 43(5) (b) na 81 toleo la 2004 kuhusu Muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali wa mwaka 2005 ulioko mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, madhumuni ya Muswada huu ni kufanya mabadiliko katika vifungu vya sheria mbalimbali ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hizo Kambi ya Upinzani ingelipenda kutoa maoni yake katika baadhi ya marekebisho ya sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Mfuko wa Elimu yaani *The Education Fund Act 2001.* Elimu ni ufunguo wa kila kitu katika maisha ya mwanadamu, elimu pia ndiyo nguzo na mhimili mkubwa katika maendeleo ya Taifa lolote, Taifa ambalo wananchi wake wana elimu ya kutosha wana uwezo wa kuhimili mikikimikiki ya maisha iwe katika masuala ya kijamii na ya kisiasa na ya kiuchumi hivyo Kambi ya Upinzani kimsingi haina tatizo kabisa na juhudi mbalimbali za kuimarisha elimu ya Tanzania ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfuko wa elimu ulioundwa na Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika hata hivyo Kambi ya Upinzani inapenda kutoa maoni yake maeneo yafuatayo:- Kambi ya Upinzani haina tatizo kutoa Mamlaka kwa mfuko kuteua mawakala wa mfuko, tunasisitiza kuwa ni lazima vigezo vya uteuzi vya wazi na visivyo na mizengwe ni lazima viwekwe ili kuhakikisha kuwa mawakala waaminifu wanapatikana. Watanzania wengi wako tayari kuchangia maendeleo yao lakini wanakatishwa tamaa baada ya muda mfupi kutokana na fedha zao kuangukia katika mikono ya watu wasio waaminifu ambao wanakusanya lakini kinachokusanywa aidha hakifiki chote au sehemu yake kwenye malengo yanayokusudiwa. Ni muhimu sana kuwa na mawakala wazuri toka mwanzo ili kujenga imani ya wachangiaji mbalimbali wakubwa kwa wadogo.

Ni muhimu pia mfuko huu kuunda *Tools and Instruments* yaani Mbinu ya kufuatilia kila kinachochangwa na wachangiaji, tusisahau kuwa huku nyuma tulishakuwa na Mfuko wa Elimu uliochangiwa na wafadhili kutoka nje lakini ulikufa kifo cha mende kutokana na kutokusimamiwa vizuri na fedha kuishia kusikopangwa. Mfuko huu ujifunze kutoka uzoefu ule na tusiingie kwenye matatizo ya aina hiyo ambayo yameendelea kudumaza daima elimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kuanzisha uhusiano na ushirikiano na Halmashauri za Wilaya mfuko ni lazima uweke vigezo vilivyo wazi, mikataba na Halmashauri ni lazima iwe wazi na yenye kuhakikisha usalama wa fedha zinazochangwa na zinazorudishwa Wilayani kwa ajili ya manufaa ya elimu Wilayani. Halmashauri ndiyo watakuwa *beneficiaries* yaani wanufaika namba moja kwani shule kimsingi zitasimamiwa na Mamlaka za Wilaya.

Kwa maoni ya Kambi ya Upinzani marekebisho haya kwa peke yake hayatoshi kutoa guarantee zitakazotakiwa katika kulinda fedha zinazotolewa na wachangiaji

mbalimbali. Tungependa kuona vigezo vya uhakika na *tools* za *monitoring* zitakazotoa uhakika kwa wachangiaji na usalama wa fedha zao.

Mheshimiwa Spika, katika sheria tunayoirekebisha kifungu cha 12(2) sasa kimefutwa. Kambi ya Upinzani inadhani hatua hiyo siyo sahihi na kifungu hicho kirudishwe wachangiaji wa ndani wa nje ndiyo wafalme na lazima tuheshimu matakwa yao iwapo tunataka kufanikisha mfuko huu.

Kuna wafadhili au wachangiaji wangependa kutoa fedha taslim na wengine wanapenda kutoa vifaa vya ujenzi au vya masomo lakini wapo pia ambao wangelipenda kulipia gharama ya shule yoyote au sehemu kwa ajili ya watoto ambao wazazi wao hawana uwezo au hata akaamua kulipia mathalani watoto wenye vipaji maalum kwa vigezo anavyoweka. Hayo yote ni kuchangia mfuko wa elimu kila mmoja anapochangia ana sababu iliyoko kwenye dhamira yake na lazima tuheshimu dhamira hiyo ama sivyo tunawakatisha tamaa. Hivyo Kambi ya Upinzani inashauri kwa nguvu kabisa kuwa kifungu hicho kirejeshwe kama ilivyo kwenye sheria tunayoirekebisha.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani hatuna tatizo na kuundwa kwa mfuko huu tunaona hatari ya kuunda mifuko mingi ya aina hii, watu mbalimbali wanaopenda kuchangia maendeleo na huduma ya jamii wangelipenda kuchangia mambo tofauti, wengine wangelipenda kuchangia huduma ya afya, wengine huduma ya maji kwa sababu mbalimbali badala ya kuunda mifuko kwa ajili kila sekta Kambi ya Upinzani ingelidhani kuwe na utaratibu unaofanana wa kuwawezesha wachangiaji wanaopenda kutoa asilimia ya biashara yao kabla ya kodi kwa ajili huduma za jamii wapate nafasi ya kufanya hivyo na wapate pia nafuu inayofanana popote pale wanapotoa.

Kambi ya Upinzani ingelipenda Serikali izingatie jambo hili na iandae utaratibu utakaowezesha watu hao kuchangia maendeleo katika eneo lolote wanalochagua kwa hiari yao na kutokana na dhamira zao. Kwa sasa sheria ya kodi ya mapato inatoa uwezekano huu lakini inaelekea maafisa wa hazina hawaelewi vizuri sheria hii na hivyo hawatoi ufafanuzi wa kina kwa wale wanaotaka na hivyo wananchi wengi wanashindwa kuchangia.

Tunaitaka Serikali iandae haraka utaratibu ulio wazi na usio na vikwazo visivyo vya lazima, mtu anayechangia hapendi tena asisumbuliwesumbuliwe kwani usumbufu ukiwa mkubwa au taratibu zisizokuwa wazi watu hawatajitokeza.

Mheshimiwa Spika, sheria nyingine inayobadilishwa na ambayo tungelipenda kutoa mchango wetu ni sheria ya ongezeko la thamani yaani *Value Added Tax Act 1997.* Mabadiliko yanayopendekezwa katika sheria hii yanahusu ongezeko la *VAT* kadhaa katika orodha inayosamehewa *VAT* kutokana na umuhimu wake kwa wananchi wetu hasa katika kukuza kilimo na uvuvi.

Kambi ya Upinzani tunaunga jitihada hizo na hata hivyo Kambi ya Upinzani haioni mantiki ya kutoa msamaha wa jenereta ya umeme au pampu ya maji kwa ajili ya shughuli za kilimo na ufugaji tu. Kambi ya Upinzani tunadhani kuwa jenereta ya umeme

popote na yeyote anayeweka iwe ni kwa ajili matumizi ya kilimo cha umwagiliaji au kuendesha vyombo vya moto vinavyotumika katika uvuvi au kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya umeme wa nyumbani ni muhimu ipate msamaha wa *VAT* na Ushuru wa Forodha kwa ujumla hii ni kwa sababu msingi wetu wa dhana ni kumkwamua Mtanzania katika kupiga vita umaskini. Yeyote anayeweza kununua jenereta akaitumia kwa ajili ya umeme wa nyumbani kwa kiwango kikubwa atakuwa ametusaidia kupunguza uharibifu wa mazingira.

Ni ukweli usiopingika kuwa Watanzania wengi tu wanatumia kuni na mkaa kwa kupika mambo ambayo yanaleta uharibifu mkubwa wa mazingira katika nchi yetu mathalani ukataji holela wa miti. Kutoa msamaha wa *VAT* na Ushuru wa Forodha utawashawishi wengi hasa katika maeneo ya mjini kununua jenereta kutumia kwa matumizi ya nyumbani. Isitoshe kwa maeneo ya vijijini jenereta hizo itakuwa kichocheo cha viwanda vidogo vidogo ambavyo ajira kwa vijana na kusaidia upatikanaji wa huduma muhimu katika ulimwengu huu wa ushindani.

Mheshimiwa Spika, tuwe wepesi kuondoa vikwazo kuliko kujenga vikwazo hata pale tu jenereta itakapotumika na watu wakaweza kutazama luninga ni mchango mkuwa katika kuelimisha jamii ambayo vinginevyo kwa muda mrefu uja watabaki kusikia tu habari ya luninga mijini. Kuwa na na jenereta siyo jambo la luxury tena tunayopaswa kuzuia kwa kuwa na kodi kubwa kubwa. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufuta kodi na ushuru huo mara moja ili kuwanufaisha wananchi wengi vijijini watakonufaika na huduma hizo. Kambi ya Upinzani inaunga mkono na inapenda jambo hilo litekelezwe mara moja.

Lakini tunaenda mbele zaidi pale ambapo wananchi wamejitahidi kubuni miradi yao iwe ya maji, iwe ya afya, elimu na wakapata msaada ya kutoka nje ya nchi au hata ndani ya nchi Serikali iwe tayari kuwaunga mkono kwa kuondoa kodi na ushuru wowote utakao takiwa kulipwa katika miradi yote ya wananchi.

Kambi ya Upinzani inadhani leo tunaondoa kodi na ushuru kwenye *wild meals* lakini hatuwezi kurekebisha kila siku hali hiyo inapotoke, tuna imani kabisa kuwa Serikali ikitaka na ikiwa na maofisa waaminifu inaweza kudhibiti wale wachache wanaotumia vibaya fursa hizo. Si jambo la busara kuwaadhibu wananchi walio wengi na kuwawekea mlolongo mgumu wa utaratibu wa kufuata ilhali mengi ya matatizo hayasababishwi na wananchi bali na watumishi wachache wa Serikali wasio waaminifu.

Mhehimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono Kambi ya Upinzani inasisitiza kukumbusha kuwa kuna sheria nyingine nyingi zenye kuguza maslahi ya watu walio wengi lakini Serikali imekaa kimya. Mfano halisi ni sheria ya matunzo ya watoto waliozaliwa nje ya ndoa ya mwaka 1949 ambayo hadi leo haijafanyiwa marekebisho na inataka Shilingi mia ndiyo iwe matunzo ya mtoto, sheria hii inawaguza watu wa chini kabisa na wako wengi.

Kambi ya Upinzani inadhani Serikali inafanya mabadiliko tu kwenye zile sheria ambazo zinainufaisha Serikali yenyewe moja kwa moja lakini zinazogusa maisha ya jamii hazipewi kipaumbele. Sheria nyingine ya namna hiyo ni sheria inayotoa tafsiri ya mtoto kwani tuna sheria nyingi zenye kukinzana kuhusu maslahi mbalimbali ya watoto.

Mheshimiwa Spika, ni imani yetu kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atatoa majibu yake na maelezo ya kina ni kitu gani kimeshindikana kuleta mabadiliko haya iwapo sheria ya 2001 inarekebishwa ni kwa nini sheria ya mwaka 1949 isirekebishwe? Bunge hili lingependa kupata maelezo ya kina kuhusu utaratibu wa kufanyia mabadiliko sheria hizi zinazogusa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni imani yetu kuwa hoja hizi zitazingatiwa na Serikali kwa nia ya kuleta manufaa makubwa zaidi kwa nchi yetu, Kambi ya Upinzani kimsingi haina matatizo na mapendekezo ya mabadiliko katika sheria nyingine zote zilizopendekezwa kufanyiwa mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, narudia tena kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani na namna ya pekee sana nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha *(Makofi)*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kwanza kuchangia pia vilevile nimshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao kwa kweli ni mzuri na ninapenda nianze kwa kusema naunga mkono asilimia mia moja.

Nitakayoyazungumza kikubwa ni kuboresha na pengine kuongeza mawazo yangu pale ninapoona kwamba sheria ingeboreka zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia si kwa kufuata umuhimu na jinsi Serikali ilivyopanga kuleta mabadiliko haya au marekebisho haya lakini nitachangia kufuatana na nilivyojielekeza katika umuhimu wa mambo ninayoona yachangiwe.

Kwanza nitaanza na mabadiliko yale au mapendekezo yale ya mwisho ya sheria ya ongezeko la thamani ya mwaka 1997 kwa kuongeza aya mpya ya 24. Napenda kuipongeza Serikali kwa nia na shabaha ya kuwasaidia wananchi, kama Mwanasheria Mkuu wa Serikali alivyosema, alisema kwamba kwa kweli lengo la mabadiliko haya au mapendekezo haya ni kupunguza gharama za watumiaji na ametaja maeneo ya pembejeo na nishati lakini mimi sina ugomvi nakubaliana na mapendekezo yote.

Mheshimiwa Spika, pengine wasiwasi wangu ni nini, Serikali ina nia nzuri sana ya kupunguza au kuondoa mizigo kwa wananchi wake hasa katika hili eneo la kupunguzwa kwa kodi kwa mfano katika suala hili ni nafuu ya kodi katika upande wa *VAT* lakini mimi wasiwasi wangu ni jinsi nafuu hizi zinavyowafikia wananchi. Mara nyingi Serikali ina nia lakini utaratibu ule wa nafuu haimfikii mwananchi.

Kwa mfano juzi tumetoa nafuu kwa upande wa mbolea lakini lilikuja swali hapa kwamba mbona mbolea imeendelea kupanda bei na nafuu haionekani? Sasa mimi ninashauri ni kweli kwamba tuko katika uchumi wa soko yaani soko huria.

Si vizuri kuweka vikwazo katika biashara za soko huria lakini tufike mahali ambapo inapofika Serikali ina adhma ya kumfikia mlaji wa mwisho.

Basi viwekwe vipengele vya sheria ambavyo vitambana muuzaji ili ifike mahali muuzaji anapoleta vifaa hivi kutoka nje kwa sababu bei zinatambulika na zinajulikana na siku hizi mawasiliano ni rahisi sana. Basi ni vizuri bei zipangwe, kuwepo na chombo cha kusimamia maeneo yote ambayo Serikali inasamehe kodi ili mwananchi wa mwisho apate unafuu.

Haisaidii sana unaposema mwananchi aweze kununua chombo cha umeme kinachotumia mwanga wa jua wakati yule mnunuzi anapokileta anaweka faida anayoitaka yeye na mara nyingi wanaweka asilimia 200, 300 na kwa sababu anasamehewa kodi tangu pale mwanzoni basi usipomdhibiti yeye atatafuta faida zaidi.

Mheshimiwa Spika, mimi hili nalisisitiza kwa sababu yapo maeneo mengi ambayo Serikali imesamehe kodi lakini wanaonufaika siyo wananchi, wanaonufaika ni wachuuzi au wale wafanyabiashara wanaofanya biashara hizo.

Lingine ambalo ningeomba nichangie ni suala la marekebisho ya mfuko wa elimu, nashukuru sana Serikali kwa kulitambua hilo. Pengine mimi nitoe pongezi kwa mwanzo mzuri wa mfuko wa elimu, mfuko wa elimu umeanza vizuri na kwa kweli matunda yake yanaonekana, misaada inayotolewa katika vyuo vyetu, misaada inayotolewa katika nyanja mbalimbali za elimu.

Napenda kuipongeza Serikali kwa kuamua sasa kuunganisha nguvu za mfuko wa elimu kufikia ngazi za wilaya, sasa pengine hapa ndiyo mahali ambapo ningeomba nitoe pendekezo. Kwa sababu mifuko ya elimu katika ngazi ya wilaya ni mingi na mfuko huu wa elimu ndiyo kwa kweli kiongozi kusimamia utaratibu mzima wa kusaidia elimu.

Mimi ningeshauri kwamba pengine sheria ingeboreshwa na ikafika mahali kwamba siyo tu kuweka uhusiano ambao siyo bayana lakini uwepo uhusiano wa bayana na ikiwezekana hii mifuko ya Wilaya ya elimu basi ikabidhiwe kwenye huu mfuko wa elimu mkuu na usimamiwe kwa kanuni pamoja na kwamba kila wilaya itachanga.

Lakini kuwepo na mtiririko pia wa msaada unaotoka katika mfuko wa elimu kwenda mpaka katika wilaya siyo kwamba kila wilaya iombe tu kufuatana na umuhimu lakini utolewe umuhimu kwamba uhusiano wa mfuko huu kitaifa uwe na uhusiano wa moja kwa moja na mifuko ya wilaya hii ingesaidia katika ku-*monitor* na kutoa elimu kwa wale wasimamizi wa mifuko ya elimu ya Wilaya kwa sababu hamasa hii kule Wilayani wakati mwingine haitoshi lakini hamasa ya kitaifa inapata fedha nyingi na Serikali inatenga fedha. Kwa hiyo, kuwepo na *direct relationship* na mifuko ya wilaya. Pengine la kuongeza hapo ni kwamba kwa kuipa umuhimu mifuko hii ya elimu ya wilaya mimi

ningeishauri Serikali kwa sasa hivi ina utaratibu wa kutoa msaada katika kila wilaya kwa wanafunzi ambao wazazi wao hawajiwezi kabisa.

Mimi ningeshauri kwamba badala ya fedha hizi kupelekwa moja kwa moja kwa Afisa Elimu fedha hizi zingepelekwa kwenye mifuko kwa sababu mifuko tayari ina uzoefu na inajua ni wakina nani ambao wana matatizo ya kusaidiwa katika elimu. Basi ingesimamiwa vizuri kuliko kusimamiwa na Halmashauri na wakati mwingine inachelesha. Taarifa zinachelewa kutoka kwa hiyo mara nyingi unakuta mategemeo ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wale ambao mfano watoto yatima au familia ambazo hazina uwezo kabisa mpaka kufikiwa inachukua muda na wakati mwingine hawafikiwi na wakati mwingine wanachukuliwa watu ambao hawakulengwa.

Kwa hiyo, kwa sababu ndiyo nimeanza kujenga uzoefu na tuna chombo hiki kikubwa cha mfuko wa elimu mimi ningeshauri kwamba basi hata fedha hizi zinapotoka wizarani zipelekwe katika mifuko sawa zisimamiwe na Halmashauri lakini zidhibitiwe na kuangaliwa na utaratibu mzima wa kuzigawa uende katika mifuko. Inaweza ikafanyiwa utafiti zaidi na kutolewa mapendekezo zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo lingine ambalo ni muhimu katika mabadiliko ya Marekebisho. Kuna eneo linahitaji kuongeza jina la *Director General.*

Mimi sijui maana yake, bahati mbaya sina ile sheria yenyewe, hivi ni kwa nini tunaweka *Commissioner* halafu tunaongeza *Director General.* Kwa nini, pengine asiitwe *Director General* kabisa badala ya kuweka *Commissioner* halafu unaongeza *Director General,* kwa nini tumpe mtu majina mawili au kwa nini tukipe cheo majina mawili. Hilo ni wazo langu na pengine Mwanasheria Mkuu anaweza kulitolea ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni muhimu ni la hawa *Collection Agents.* Mimi nashauri sana Shirika la Bima limepoteza fedha nyingi sana kwa kuweka hawa *agents* wa kukusanya kwa niaba. Tuwe waangalifu sana katika kuwateua hawa na kama kwa kweli watateuliwa wababaishaji hizi fedha zinaweza kupotea nyingi. Kwa hiyo, ni muhimu sana utaratibu huu wa kupata *Collection Agents* ufanyike, lakini tuangalie na tuwe waangalifu sana katika kuteua watu hao ambao watakusanya kwa niaba ya Mfuko.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningeomba kutoa mawazo yangu kidogo ni suala la Vyama vya Ushirika kuingia katika ubia. Mimi nakubali hili ni wazo zuri na kwa kweli ni kupanua wigo na kuvisaidia vyama viwe *partners* na watu ambao wana uzoefu. Lakini pia ni vizuri tukaelewa kwamba uzoefu wa huko nyuma umeonyesha kwamba wale walioingia ubia au mikataba na watu ambao wana elimu ya juu zaidi au ni wajanja zaidi, wanapata matatizo. Ni vizuri hili liangaliwe sana wakati tunaingia katika mikataba na Vyama pengine vipewe msaada na waonywe kabisa na Wizara kwamba ni vizuri wanapoingia katika mikataba ya ubia wawe waangalifu. Wanaweza kabisa kutapeliwa, wakaingia katika makubaliano ya ajabu ajabu, wakapoteza haki zao.

Kwa hiyo, hili napenda tu kulisisitiza na ni wazo zuri. Hili linaendana na elimu na kuwa na viongozi wenye uwezo katika Vyama vya Ushirika. Hilo ni la msingi sana, kule kuchagua tu, huyu ni mtoto wa mjomba awe Katibu, huyu ni nani awe Katiba iachwe. Tutafute watu walio na uwezo wa kielimu na upeo mkubwa wa elimu ili waweze kuongoza Vyama vya Ushirika ambavyo vinaingia katika Mikataba hii, vinginevyo watu wetu watatapeliwa na ushirika hautakomaa, siku zote tutauuza kwa watu ambao ni wajanja.

Mheshimiwa Spika, mimi nimeona nichangie hivyo katika hilo. Katika eneo la vivutio kwa wawekezaji, mimi nakubaliana na mabadiliko yale yaliyopendekezwa. Pengine la msingi tu ni la ujumla kwamba wawekezaji wanapokuja nchini wengine ni wajanja sana na kama inavyosisitizwa na kama inavyoonekana sasa Serikali inajaribu kubana ili ile mipenyo ambayo wawekezaji wanaitumia kuingia nchini, kuwekeza kwa muda mfupi, wakishapata wanaondoka waiondoe. Hili ni muhimu, lakini kama ilivyopendekezwa ni vizuri kuwa waangalifu na wawekezaji. Tuwe wakali na wapole, tusiwe wakali sana kwani tutawafukuza na tusiwe wapole sana tukawa wajinga wakatuchukulia hela zetu. Kwa hiyo suala la kusisitiza ni kuangalia sheria hizi mara kwa mara, ni vipi tupunguze na ni vipi tuongeze.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri sana suala la wawekezaji ni muhimu lakini ni vizuri kuwa waangalifu sana katika kuwakaribisha wawekezaji. Wawekezaji wengi hasa hawa wanaokuja na *handbag* za mifukoni bila ofisi na bila kuwaelewa wanakotoka wametuyumbisha sana. Kwa hiyo ni vizuri tuwe na uhakika na kila mwekezaji anapokuja achujwe. Asipewe hivi vivutio, baada ya muda akivipata anaondoka, amekwishachukua hela zake. Hebu angalia mabadiliko yanayotokea katika wawekezaji, mwekezaji anakuja leo, baadaye kidogo anamwuzia mwingine. Kwa hiyo, ni vizuri kuwaangalia hawa je, wanakuja na dhamira ya kweli.

Mheshimiwa Spika, katika hili mimi ningesisitiza kuwepo na chombo cha kuangalia mikataba iliyowekwa na utekelezaji wake ili wale wote ambao hawakutekeleza mikataba ambayo wameweka basi wachukuliwe hatua, tukiachia suala hili lisimamiwe na Wizara kama ilivyo sasa utakuta wawekezaji wengi hawatekelezi mikataba kama walivyoahidi na matokeo yake Taifa linakosa mapato. Mtu amekuja awekeze katika Kiwanda cha Matunda, badala ya kuwekeza katika Kiwanda cha Matunda anatengeneza *Flavours Juice* ambapo sisi tulitaka tuwanufaishe wakulima waweze kununuliwa matunda yao, lakini huyu anapokuja anatumia rangi na maji anatengeneza *juice.* Sasa nia yetu haikuwa hiyo, kwa hiyo hawa wabanwe kwa kwenda kinyume na ile mikataba inavyosema.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nitumie nafasi hii kukushukuru ili na mimi niweze kuchangia machache kwenye marekebisho ya Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2005. Lakini kabla sijafanya hivyo naomba niseme kwamba, kwa niaba ya wananchi wangu wa Babati

Mashariki nami mwenyewe niungane na wenzangu wote katika kutoa rambirambi kwa wananchi wa Kasulu Mashariki kwa kufiwa na mpendwa wao Mheshimiwa Frank Mussati ambaye kwa kweli alikuwa mkimya na mtaratibu sana. Kwa kweli tunamkumbuka sana na Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nitumie nafasi hii kuwapa pole wale wote ambao katika kipindi chote hiki wameweza kupata misiba mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Muswada huu mimi nakubaliana kabisa na marekebisho ambayo yameletwa, sina tatizo kabisa na niseme kabisa kwamba naunga mkono asilimia mia moja marekebisho ya Muswada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nimeguswa zaidi na eneo hili la Mfuko wa Elimu. Katika Sheria ya Mfuko wa Elimu ya Mwaka, 2001, kwanza niseme kwamba wote tunafahamu kwamba elimu ni nyenzo na hasa katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na vile vile katika kuboresha maisha ya binadamu na hakuna mkakati wowote wa Kitaifa utakaofanikiwa bila kuhusisha elimu. Hili ni jambo muhimu sana na kwa kweli elimu ndiyo inamwezesha binadamu au mtu yeyote kupambana na wale maadui wawili yaani umaskini na maradhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama nilivyosema nimeguswa kidogo na marekebisho katika Mfuko huu wa Elimu. Lakini kwanza niseme Mfuko huu wa Elimu tangu uundwe kwa kweli inaonekana kwamba kazi zake zinaridhisha sana kwa sababu ukiangalia taarifa za Mfuko huu chache ambazo nimeweza kuziangalia, utakuta kwamba Mfuko huu umeweza kuchangia vyuo ishirini na saba ikiwa ni pamoja na Vyuo vya Kati mpaka Vyuo Vikuu na mimi nimepata bahati ya kupita katika Vyuo Vikuu na katika Vyuo vingine na nimeona jinsi ambavyo Mfuko huu umeweza kuchangia fedha nyingi sana. Vile vile umeweza kuchangia karibu shule kumi na nane zikiwa ni pamoja na shule za sekondari. Kwa hiyo, Mfuko huu kwa kweli unafanya kazi kubwa sana na hasa katika zile fedha ambazo mara nyingi zinasaidia watoto yatima ambazo zinapelekwa kwenye Halmashauri za Wilaya zetu. Vile vile Mfuko huu umefanya kazi kubwa ya kuisaidia Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba watoto hao kweli wanasaidiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo napenda nijikite kidogo katika eneo hili tu la mamlaka ya Mfuko wa Elimu. Katika marekebisho sina tatizo kabisa na kifungu kile cha 5(2) ambacho kwa kweli kinaupa mamlaka Mfuko wa Elimu ya kutekeleza majukumu yake kwa njia ambayo mamlaka inaona kwamba italeta ufanisi na kwa kweli inafaa. Vile vile katika kifungu kile cha 8(2), kwa ajili ya kuteua wakala wa kukusanya fedha na kama walivyosema wenzangu ni muhimu katika eneo hili Mawakala ambao wanateuliwa, kitu muhimu ni kuhakikisha kwamba kwa kweli kunakuwa na ufuatiliaji mzuri kabisa na taarifa za utendaji wa hawa watu ambao watakuwa ni mawakala zinatakiwa zifuatiliwe sana kwa sababu wote tunafahamu kwamba michango mingi ambayo imekuwepo ya elimu katika Wilaya zetu na katika maeneo mbalimbali mara nyingi tumesikia ubadhirifu wa hapa na pale. Sasa katika kuimarisha hili mimi naungana kabisa na marekebisho haya na muhimu nikazie tu hapo katika ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika fungu la 10(a) linalokusudia kujenga mahusiano baina ya mamlaka ya Mfuko wa Elimu na Mifuko ya Elimu iliyopo katika Serikali za Mitaa, kwa kweli jambo hili ni muhimu sana na hili litaunganisha mtiririko mzuri wa namna ya kuchangia elimu. Sasa wakati Serikali inafanya marekebisho nilidhani kwamba ni vizuri vile vile Serikali ikawa inaangalia sheria yote kwa ujumla kwa sababu ninavyoona lipo eneo ambalo mimi nadhani ni muhimu sana na ambalo pengine halijafanyiwa marekebisho katika sheria hii. Katika kifungu cha 13(a) kifungu hicho tulikisemea sana katika bajeti na katika taarifa mbalimbali kwamba kifungu hiki kwa kweli tunadhani bado kina utata wa namna moja au nyingine. Kwanza kinasema hivi, naomba naomba kunukuu: "Serikali itatoa kutoka bajeti yake asilimia isiyozidi mbili baada ya kutoa madeni ya Taifa kama ruzuku kwa ajili ya Mfuko huu".

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki kina utata na kwa kweli hakiweki uzito wa kutosha kwa mahitaji ya Mfuko wa Elimu, kwani inaposemwa kiasi kisichozidi asilimia mbili, maana yake hata asilimia sifuri haijazidi mbili. Kwa hiyo, Serikali inaweza ikaamua kutoa kiasi chochote. Kwa hiyo ilitakiwa kwamba angalau kile kiwango cha chini kingewekwa. Sasa mimi labda nitoe tu mifano michache jinsi ambavyo Serikali imechangia Mfuko huu wa Elimu katika eneo hilo tangu mwaka 2001/2002. Katika mwaka 2001/2002, kiasi ambacho kingetarajiwa cha asilimia mbili ya matumizi ya kawaida ya bajeti ya Serikali kingepaswa kutengwa 21.59bn/=, lakini kiasi ambacho kimetengwa na Hazina na ambacho ndio kimetolewa katika mwaka 2001/2002 ni asilimia 0.45 ambayo ni sawa na 4.9bn/= kwa fedha za kugharamia maendeleo, fedha za matumizi ya kawaida ambazo zimetengwa ambazo kwa mwaka huo Serikali katika matumizi ya kawaida ilikuwa imetenga sh. 1079.9bn/=.

Katika mwaka 2002/2003, Serikali ilipaswa kutenga asilimia hiyo mbili ambayo ni 23.51bn/=, lakini kiasi kilichotengwa katika bajeti ni asilimia 0.4, kinazidi kwa kweli kuteremka ambacho ni sawa na 4.9bn/= ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi. Mwaka 2003/2004, fedha ambazo zingepaswa kwenda kwenye Mfuko huu ni Sh. 27.82bn/=, lakini Serikali imetenga asilimia 0.39, inazidi kupungua ili kwenda kwenye hiyo sifuri ninayosema ambayo kwa fedha zile ilikuwa kama sh. 5.4bn/=. Mwaka 2004/2005, ilitarajiwa kwamba kutokana na asilimia mbili ya matumizi ya kawaida ya bajeti ya Serikali, Serikali ingepaswa kutenga 35.20bn/=, lakini sasa hapa ndio imekuwa chini zaidi. Kitu cha kushangaza Serikali imetenga asilimia 0.23 ambayo ni sawa na sh. 4.4bn/=.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa mtiririko huu utaona kwamba kwa kweli kuna utata kidogo na mimi nimeona sheria nyingi tunapotunga hapa unaweza ukasema kwamba mtu anatozwa faini ya elfu hamsini lakini isiyozidi laki moja. Lakini katika sheria hii tumesema kiasi kisichozidi asilimia mbili. Sasa kiasi cha chini kiko wapi. Tunaomba Serikali ilete marekebisho, itamke kiasi cha chini maana vinginevyo kuna mwaka Serikali itafika itaamua kutokutoa kabisa fedha kwenye Mfuko huu.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwamba basi katika marekebisho ni vema Serikali ikaliangalia hili ijaribu kuleta basi hata kile kima cha chini ambacho chenyewe kinaweza kutokana na uwezo wake ili tufike mahali tujue kwamba huu Mfuko ambao ni muhimu

sana katika kusaidia elimu unatusaidia sana na kwamba tungeweza kupambana katika malengo yale manane ya maendeleo ya *millennium.* Katika malengo manane ya *millennium* elimu ipo kwenye nafasi ya pili. Kwa hiyo, ni jambo muhimu sana. Sasa naomba Serikali ione umuhimu wa kurekebisha Muswada huu katika kifungu kile cha 13(a).

Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kwamba baada ya maelezo haya Serikali itaona wakati ujao umuhimu wa jambo hili la Mfuko huu wa Elimu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL E. KIPOLE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika Muswada huu wa mabadiliko ya sheria. Kwanza niseme kwamba ninaunga mkono hoja hii ya mabadiliko kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama ili ikae kwenye rekodi kwamba niliunga mkono hoja hii kwa kuzungumza. Mchango wangu nitauelekeza kwenye hili eneo la (d) kwenye mabadiliko ya sheria ya *VAT.* Kwa kweli niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kuona kwamba sasa hivi vyombo vya nishati ya jua vinahitajika kwa wananchi. Kwetu sisi tunaotoka kwenye maeneo ya Vijijini na ambapo kwa kweli ni sehemu chache mno ambazo wanapata umeme, hii ni faraja kubwa kwetu. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Msalala ambao wanahitaji sana huu umeme wa jua kwa sababu bado hatujaweza kuwapelekea umeme wa aina nyingine.

Mheshimiwa Spika, pengine itakuwa changamoto kwa Serikali kuangalia pia maeneo mengine ambayo yana vikwazo vya kodi ambavyo wanashindwa kutumiwa na wananchi kwa sababu ya kukwazwa na kodi. Kama tunavyofahamu kodi kwa upande mwingine huwa ni kichocheo cha kuzuia matumizi ya jambo fulani. Nitatoa mfano, kwa mfano, kama nchi itaamua kitu fulani kisitumike sana katika nchi, inaweza kuongeza kodi kwenye eneo hilo. Sasa kitu kama hiki cha *solar* Serikali ilikuwa imeacha kodi ikawekwa pale, imewa-*discourage* wananchi kutumia vyombo hivyo, lakini sasa tunafikiri wataweza kuvitumia na ninasema kwamba ijaribu pia kuangalia maeneo mengine ambayo yana vikwazo vya kodi iweze kujiondoa pia.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi sana nilikuwa naomba nitoe mapendekezo katika hii Ibara ya 24 kwamba yamewekwa masharti ili mtu aweze kupata huo msamaha lazima apitie kwa *Director then* aende kwa *TRA.* Nafikiri sasa hii inaweza kupunguza au kuondoa dhana na azma nzima ya kupeleka huo unafuu. Hapa kutajitokeza urasimu usiokuwa wa lazima. Utakuwepo mlolongo mrefu ambao pengine hata utakatisha tamaa tena na kwa sababu tunawalenga wananchi wa Vijijini ambao kwa kweli utakapompelekea mambo ya karatasi nyingi nyingi na maombi mengi mengi tayari unamvunja moyo na unamkatisha tamaa.

Kwa hiyo, atabaki hivyo hivyo bila kutaka kutumia. Pengine tuangalie utaratibu au pengine labda Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali atakapokuwa ana-*wind up*

atatwambia ni kwa nini wanafikiri ni lazima kuwepo na mlolongo mzima wa kupita kwa *Director then* ukapeleke, nafikiri italeta urasimu ambao utawakatisha tamaa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hapa lingine ninalopenda kuongeza ni kwamba yametajwa maeneo hapa ambayo yataruhusiwa. Naomba ninukuu kwamba: *"The Director of Local Government Authority but such generator or water pump shall be used for the purpose of irrigation, fishing and keeping livestock".* Nafikiri tunaweza kuongeza maeneo hapa ninakotoka mimi tuna wachimbaji wadogo wadogo, miongoni mwa nyenzo muhimu wanazozihitaji ni *generator* pamoja na *water pump* kwa ajili ya ku-pump maji kuyatoa mashimoni ili waweze kuendelea kuchimba, lakini pia wanazihitaji hizi *generator* kwa ajili ya kupata mwanga wakati wa shughuli zao. Nilidhani kwamba tuongeze sekta ya wachimbaji wadogo wadogo. Wanavihitaji sana vifaa hivi na sisi tunataka kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo tunafahamu jinsi wanavyofanya shughuli zao. Nilikuwa naomba kwa dhati kabisa Serikali iweze kupokea ombi langu ili iongezwe hiyo sekta ya wachimbaji wadogo wadogo katika vifaa vya *water pump* pamoja na *generator.*

Mheshimiwa Spika, vile vile na watumiaji wa majumbani. Naona hapa wameenguliwa sijui ni kwa sababu gani lakini nafikiri wanahitaji *generator* ili waweze kujipatia umeme katika Vijiji ambavyo havina huu umeme. Kwa hiyo, nilikuwa naomba haya maeneo mawili yaongezwe watumiaji wa nyumbani na watumiaji katika migodi ya wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. LEONARD M. SHANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nichangie kidogo katika Muswada huu. Awali ya yote kwa niaba ya wananchi, wapiga kura wangu wa Iramba Magharibi nami naungana na wenzangu kutoa salam za rambirambi kwa familia ya mwenzetu Mheshimiwa Mussati pia na Waheshimiwa Wabunge wengine ambao wamepata matatizo haya ya kufiwa.

Mheshimiwa Spika, mimi nitachangia katika maeneo mawili. Kwanza kabisa naunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilichonifurahisha zaidi ni kuona kuwa Muswada huu umeleta marekebisho kuhusu *The Education Fund Act, 2001,* lakini mimi naona kuwa Mfuko huu kwa kweli ungepanuliwa zaidi na kwa sababu elimu sasa hivi tunavyoona mahitaji yake ni makubwa sana, shule zinajengwa, watu binafsi wanajenga shule, Serikali inaendelea kujenga shule za msingi, sekondari na vyuo.

Sasa katika Muswada huu kwa kuwa hii ni sheria, ningeomba mambo ambayo yatahusika hapa na marekebisho yawe kamili kabisa yaani orodha kamili ya vitu ambavyo vitanufaika na marekebisho haya. Ni kweli Muswada unazungumzia kuwa kutakuwa na kusamehewa au kupunguziwa kodi mbalimbali kwa wale ambao watajihusisha katika kuwekeza katika sekta ya elimu. Labda hapa mimi ningeomba tu ufafanuzi. Je, wenzetu ambao sasa wamechukua nafasi kubwa sana katika kusaidia sekta ya elimu ambao wanajenga shule binafsi, wanajenga kwa gharama kubwa sana kwa

sababu vifaa na vitu wanavyovitumia katika ujenzi lazima waende kwenye maduka ya kawaida. Sasa ningeomba hawa kwa njia moja au nyingine wao pia wapate unafuu kwa kupitia sheria hii.

Mheshimiwa Spika, pili, Mfuko huu pia ujihusishe zaidi katika kusaidia wale watoto ambao wazazi wao au walezi wao hawapo (watoto yatima) ambao hawatapata nafasi kabisa ya kuendelea kwa sababu ya kukosa uwezo wa fedha za kulipia gharama zinazotakiwa. Sasa ningeomba hapa suala la kupewa *scholarships* kusudi wale wanaokwenda kwenye shule za binafsi ambazo ni za gharama kubwa wapewe pia *scholarship* au misaada ya kifedha kusudi wawezeshwe kwa sababu sasa hivi ukitazama shule hizi zinachukua tu wale wenye uwezo na wale ambao hawana uwezo wanabaki. Kwa sasa hivi tunajua kwamba watoto wanaomaliza darasa la saba asilimia kubwa kabisa hawaendelei na sekondari kwa sababu nafasi hakuna au hawana uwezo wa kulipia gharama kwenye shule binafsi. Kwa hiyo, huu Mfuko ungejihusisha kusaidia katika kuhakikisha kwamba shule binafsi pia zinachukua wale watoto ambao hawatakuwa na uwezo wa kulipa gharama kamili.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuongelea suala la Ushirika, *The Cooperative Societies Act.* Hapa marekebisho yameorodhesha vitu fulani fulani hasa ukitazama ile Ibara ya 24 ambayo imerekebishwa na imeorodhesha vitu ambavyo vitahusishwa na kunufaika na punguzo au kuondolewa kodi. Sasa mimi ningeomba au ningeshauri kuwa tuone ushirika ni kama dhana mojawapo ya kupunguza umaskini kwa wananchi wetu Vijijini na Mijini. Sasa ukitazama mambo yaliyoorodheshwa hapa mimi ningeomba yaongezewe yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kilimo cha wakulima wadogo wadogo, vifaa vyote vinavyotumika katika kilimo kile viondolewe kodi. Pia ningeomba kuna magari kama *pick-ups* sasa ama wewe mwanaushirika una mazao yako utayapelekaje hayo mazao yako sokoni kama *pick-ups* kodi yake ni kubwa. Kwa hiyo, ipunguzwe kusudi kukidhi matakwa ya wanaushirika na kwa kuwa tumesema kuwa watapitia katika Halmashauri zao, watapewa barua wanaponunua au kuagiza vifaa kama hivi kusudi wapunguziwe kodi katika magari ya namna hii.

Mheshimiwa Spika, pia kuna vifaa vingine kama *generator* vimetajwa hapa lakini kuna vifaa kama vya *biogas, windmill equipment and solar equipment.* Hivi vyote ni vifaa muhimu sana kwa maeneo ya Vijijini. Sasa ningeomba iwekwe wazi kuwa vinufaike katika kuondolewa kodi. Kwa kufanya hivyo siyo tu kwa wananchi waliopo Vijijini wataboresha maisha yao lakini pia watasaidia katika kuboresha mazingira. Suala la kuendelea kukata miti, kufyeka vichaka kwa sababu ya kupata kuni na mikaa vitapungua.

Mimi mfano mzuri nyumbani kwangu pale Kijijini nina *biogas,* katika Mkoa wote wa Singida ni peke yangu nina *biogas* na juzi hata Wizara ya Nishati ilipeleka wataalam wake kwenda kutazama na matumizi ya kuni hayapo tena. Kwa hiyo, ningeomba wakulima na wafugaji wasaidiwe katika kupata au kujenga mitambo hii midogo midogo kusudi watumie kama nishati ya kupikia na taa.

Sasa ningeomba kwa kweli Muswada huu kwa kuwa ni sheria sio suala la kuwa tunaongelea hivi hivi, vifaa hivyo vyote ambavyo havipo hapo viwekwe wazi, viorodheshwe kusudi mtu anapoomba msamaha aonekane kuwa na yeye *covered by this law.*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa mimi ninachoogopa, Muswada huu ni mzuri, marekebisho tutayapitisha, lakini utekelezaji wake unakuwa na matata. Kwanza, kuna urasimu ambao umejengwa humu humu katika sheria hii. Hivi wakulima au wananchi kutoka Kijijini waanze kupitia Halmashauri, baadaye ndio waende kukomboa vifaa vyao labda bandarini au wapi. *(Makofi)*

Hili suala la milolongo kwa kweli itawakatisha tamaa wananchi. Mimi ningeomba hivi vifaa vinaletwa na wafanyabiashara visamehewe kodi na ule msamaha utakuwa *pass over to the beneficiaries.* Sasa hili suala la kuleta urasimu kama huu wakati mwingine ndiyo inakuwa mwanya wa rushwa. Kwa sababu unapokwenda kutafuta barua fulani ndiyo unaanza kuombwa chochote.

Kwa hiyo, kodi kama hizi zingekuwa moja kwa moja zinatolewa maagizo kuwa wafanyabiashara wanaoingiza vifaa hivi wawe wameondolewa kodi na Halmashauri isimamie kuhakikisha kuwa wasije wakauza kwa bei mbaya kwa kisingizio kuwa wamelipia kodi.

Mheshimiwa Spika, pia ningeomba suala la viwanda vidogo vidogo *food processing* kama mashine za kusaga, mashine za kukamua mafuta ya alizeti na kwa upande wa mijini mashine za kutengeneza vyakula vya mifugo na hivi vifaa vyao vyote vingeondolewa kodi. Kwa sababu kama mjini watu wanaonufaika zaidi na ufugaji wa kuku au ng’ombe ni akinamama na watu ambao hali yao siyo nzuri hasa wastaafu ndiyo miradi yao.

Sasa ningeomba pia orodha hii iongezeke ya vifaa vinavyotumika katika viwanda vidogo vidogo vya kusaga kwa mfano kama mashine za kusaga au kukamua mafuta na vingine vya kutengeneza vyakula vya mifugo na vile vinufaike katika msamaha huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nasema tu kuwa Muswada huu ni mzuri. Lakini utekelezaji wake sasa uangaliwe sana kwa sababu utaleta matatizo haya ya urasimu wa *bureaucracy.* Kwa kweli tunahitaji elimu maalum kusisitiza kuwa wale wanaotaka kunufaika kutoka vijijini wasifuate mlolongo ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, narudi tena kusema kuwa ninaunga mkono Muswada huu mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wasemaji wote waliojiandikisha kuchangia Muswada huu wamemalizika. Kwa hiyo, Mheshimiwa mtoa hoja jiandae kuhitimisha

hoja yako. Wakati unafanya hivyo namwomba Mheshimiwa Naibu Spika, anipokee kiti. *(Makofi)*

*Hapa Naibu Spika, (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia kiti*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuhitimisha hoja yangu. Nianze kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja hii nikianza na Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Grace Kiwelu, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Emmanuel Kipole na mwisho Mheshimiwa Leonard Shango. Nawashukuru sana kwa michango yenu mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza kwa haraka haraka tu na maeneo muhimu yaliyosemwa nadhani ni hili sharti ambalo linawekwa na Serikali kupitia Muswada huu wa kumtaka mwananchi ambaye ana pampu au vifaa vya *solar* ambavyo anataka vimsaidie katika shughuli zake za maendeleo kwa nini tuweke njia ya urasimu, yawezekana yote haya ni kuwakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tusisahau kwamba moja ya kazi ya jukumu la Serikali ni kuhakikisha kwamba vifaa vinavyoingia nchini vinalipiwa ushuru, na maendeleo ya nchi hii na kama ilivyo kwa nchi yoyote yanategemea makusanyo ya kodi halali kutoka kwa wananchi. Usipoweka utaratibu mzuri ujue unajitumbukiza katika lindi la mapato ya Taifa kuvunja kwa kutumiwa vibaya. Binadamu ndivyo tulivyozaliwa, akipata mwanya kidogo anataka alalie hapo hapo.

Lakini tunaamini utaratibu huu siyo mgeni. Napenda tu nilikumbushe Bunge lako Tukufu kwamba ukiangalia jedwali la 3 la sheria hii ya Kodi ya Ongezeko la Thamani yaani *VAT* utakuta katika Ibara ya 9(2) sharti hili lipo. Ningelipenda sana Waheshimiwa Wabunge waiambie Serikali kwamba tangu Bunge liweke sharti hili pamekuwa na tatizo gani? Maana tumeona tuendelee kutumia utaratibu huo ambao upo na wananchi wetu wamekuwa wakiutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa hapa hapa niseme kwa hoja nzuri aliyosema Mheshimiwa Leonard Shango kwamba hawa wananchi ambao wanachangia sana katika ujenzi wa shule na hii ilikuwa hoja tangu mwanzo kwamba jamani tunatambua elimu kama ndiyo kichocheo cha maendeleo hasa tusipoweza tukaisaidia katika kupunguza kodi katika maeneo mbalimbali hasa hii ya *VAT* tutakuwa hatufanyi lolote la maana.

Ndiyo maana Serikali ikaja hapa Bungeni na tukapata idhini yenu, ukiangalia jedwali la 3 kwenye eneo hilo hilo na jedwali la 2 utakuta maeneo haya tayari yameshughulikiwa kwa hiyo tunakwenda vizuri. Ni pale ambapo tunaona kwamba kuna hoja imejengwa hebu tuiangalie ndiyo tunasema na hili tulichukue. Lakini maendeleo yatakuja kwa nguvu za wananchi lakini pia kwa kodi za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vifungu vya kwenye eneo la sheria ya uwekezaji tulivyoenda navyo mbele ya Kamati, ukiangalia marekebisho haya yanayopendekezwa naamini kimeandikwa vizuri. Mimi Kiingereza siyo lugha ya kwanza, lakini tumejitahidi kinatiririka vizuri. Hoja hapa ni kwamba unapewa nafuu hiyo ya kodi. Kule zimetajwa tu maana maeneo makubwa ya kodi ni kodi ya mapato, kodi ya ushuru wa forodha na kodi ya ongezeko la thamani. *Exercise Duty* ni mara chache tunafika huko. Lakini maeneo hayo ndiyo tunasema cheti chako kile umeshapewa cha unafuu. Nafuu hiyo ni ya miaka 5 tangu cheti hicho kitolewe tofauti na ilivyokuwa inasema tangu uanze shughuli zako.

Sasa shughuli zako unaweza ukawa na *line* moja ya uzalishaji tuseme katika kiwanda cha bia, leo una *line* moja unafunga hapa, kesho unafunga nyingine sasa unasema *operation* zako zimeanza lini? Sasa tunaondokana na utata huo ni kwamba *you have* miaka mitano tumia hiyo fursa yako. Lakini tunaendelea kusema kwamba iwapo kutokana na maboresho haya yanayoendelea katika Mfumo wa Kodi katika kipindi cha miaka mitano itaonekana kwamba umewekwa unafuu mzuri wa kodi, basi mwekezaji huyo apate fursa ya kuingia katika utaratibu wa kawaida wa ulipaji kodi. Tunaamini lengo ni hilo hilo nchi yetu itajengwa na Watanzania wenyewe wawekezaji wa ndani, lakini pia kwa muda mrefu ujao kwa kushirikiana na wawekezaji wa kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la Mfuko wa Elimu nadhani hili limesemewa vizuri tu. Kwanza, nikubaliane kabisa na hoja ya Mheshimiwa Grace Kiwelu kwa upande wa hawa Mawakala wa kukusanya michango hii. Naamini kabisa uongozi wa Mfuko huu utazingatia katika kuhakikisha kwamba wanaweka watu waadilifu wanaoaminika na sio matapeli ambao watakimbia na michango ya wananchi. Ukiona *scheme* ya sheria yenyewe ilivyo kwa hawa Mawakala kwa sababu wenyewe wanafanya kwa niaba ya Mfuko, ukifanya manzaga utaratibu wa kuwashughulikia upo. Lakini ni hoja nzuri nadhani na wao wameisikia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilipendekezwa kwamba turejeshe kile kifungu cha (12)(1). Sisi tulisikia hoja kwenye Kamati na ndiyo maana tumekiandika upya. Ukiangalia *schedule of amendments* kina sura ile ile isipokuwa tumepanua kidogo sasa maana kule kulikuwa na restriction ya shule ya Sekondari na Chuo Kikuu. Sasa sisi tumeacha wazi kwa sababu Mfuko huu unashughulikia tangu *Primary, Secondary* na Chuo Kikuu. Tunachosema tu ni kwamba tuyafanye hayo unaweza kuwa ni ku-*sponsor* kusoma hapa au nje, tunachosema tu ni kwamba huyu unayem-*sponsor* msiwe na uhusiano wa damu. Maana wewe una jukumu la kusomesha ndugu yangu kama una uwezo, sasa usije ukaja na ujanja huo ukasema unachangia kuja kupata *relief* ya kodi, hiyo tunasema hapana bwana. Ndiyo hoja yetu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *generator* na yote haya yameingizwa bila ushuru. Nimeeleza nia ni nzuri lakini haiwezekani. Kwa kundi ndogo lile la wachimbaji wadogo wadogo niseme tu kwa hoja ya Mheshimiwa Emmanuel Kipole ni nzuri. Lakini kama mlivyosikia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amesema Serikali inaangalia sekta hiyo ya wachimbaji wadogo wadogo itakavyoweza kuwasaidiwa na hasa kwenye

eneo la *generatots* na *water pump* kwa sababu kwenda chini huku kunahitaji vifaa hivyo. Lakini kwa eneo hili tulikuwa tumesema kwa sasa tusijitumbukize katika mapendekezo yaliyopo mbele ya Muswada huu yasubiri utaratibu unaokuja. Naamini wakati utakapowadia eneo hili na lenyewe litaangaliwa kwa makini na Serikali na kuletewa mapendekezo mazuri tu. Pale ambapo wananchi wamejikusanya wanapata msaada kutoka nje kwa nini wasisaidiwe. Mara nyingi ndivyo inavyotokea kama kuna hoja nzuri na sheria inaruhusu kikundi kimejiunga wamepata misaada wanaenda kwa Waziri wa Fedha wanajenga hoja wanaona kama hili linawezekana, basi Waziri anashauriwa anatoa kupitia *GN* hiyo nafuu ya kodi kwa vifaa *specific* ambavyo vinaenda kwa shughuli za maendeleo.

Hoja ya Mheshimiwa Henry Shekiffu, uhusiano wa Mfuko huu na ile Mifuko mingine hii ndiyo shabaha kubwa kwa sababu Sheria ya sasa ilikuwa haiweki utaratibu wa jinsi watakavyokuwa na mahusiano hayo. Sasa ni jinsi gani hayo mahusiano na mawasiliano yawe, ndiyo tunataka wao waketi kitako Mfuko huu na ile ya Halmashauri zetu waweze kuweka utaratibu *the model superintend* ambayo itakayowezesha shughuli hizi kufanyika kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Director General* wa Mamlaka hii pamoja na *Commissioner General* wa *TRA* hawa ni viongozi wakuu wa vyombo hivi viwili. Tunawaweka katika namna hiyo kwa sababu ni wadau muhimu kama Sheria inavyowataka. Kile cheti unachomtunuku mwananchi aliyechangia katika Mfuko huu utakuta wote wawili wanaweka saini zao kama aina ya utambulisho. Lakini kubwa zaidi kwa *TRA* ni kwa sababu huyu anayechangia ndiye anapata zile *Tax benefits* ile relief kwa muda gani. Sasa watapima hawa upewe nini.

Lakini katika eneo hili tulisema pale ambapo inaonekana sasa kuna matumizi mabaya ya nafuu hizi *trigger mechanism* ambayo inapendekezwa kupitia *schedule of amendments* ni kuanzia kwa *Director General* maana yeye ndiye anawafahamu kule walikochangia wamechangia nini na muda hasa ndiyo tunapendekeza kwamba iwapo patakuwa na tatizo la namna hiyo hizo nafuu za kodi ziweze kusitishwa, sasa yeye ndiye ana *trigger* hiyo kumjulisha *Commissioner General,* ndiyo dhana hiyo iliyomo na *Commissioner General* akiridhika kwa mujibu wa Sheria yake ndiyo tumependekeza, kwa sababu yule anafuja utaratibu huu akiweza kusema ndiyo kweli nimefuja na ndiyo kuna *option* ya ku-*compound* ile *offence.* Halafu mambo mengine yanafuata kama ilivyopendekezwa katika Ibara ndogo ya (8) ya ukurasa wa pili pale juu wa marekebisho hayo. Kwa hiyo, ndiyo *role* hizo mbili za nafasi za viongozi hawa wawili.

Mheshimiwa Omar Kwaangw' ameleta hiyo hoja na ni hoja nzuri na kama mnavyosema kila wakati Waheshimiwa Wabunge hii ilikuwa ni nafasi nzuri Mfuko huu ukatunishwa na Serikali ikachangia kupitia bajeti yake na ikaonekana inachangia. Lakini kwa Sheria hatuwezi kusema kwamba sasa tunakiuka sheria. Sheria iko wazi kabisa kiasi cha mchango kisichozidi asilimia 2 ya vigezo vilivyowekwa, na ni kweli kwa kutegemea ile *formula* inaweza kama kwa *figure* alizokuwa anazitoa Mheshimiwa Omar Kwaangw' ni kweli. Lakini hiyo haimaanishi kwamba kuna ukiukwaji wa sheria, ila ni

eneo ambalo linaweza kuangaliwa, na *formula* hii ndiyo tunayoitumia kama mnavyokumbuka katika utoaji wa ruzuku kwa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mimi naamini kama Watanzania tunajituma tukafanya kazi kwa bidii na maarifa tukaibua uchumi suala hili ndiyo jibu kwa hoja ambayo Omar Kwaangw' amekuwa anaitoa. Bajeti ya Serikali inakuja hapa na wote mnaiona na nyie ndiyo mnaoidhinisha. Sasa hatuna njia nyingine isipokuwa kule kuchochea jitihada za maendeleo na uchumi wetu ukakua na kuimarika haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa hayo machache, nimalizie kwa kukushukuru wewe na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza na ninaomba kabisa tusaidieni kama tulivyosaidiana tangu wiki iliyopita na sehemu hii ya Muswada katika ngazi hii Serikali iweze kuungwa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2005**
***(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005)***

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge Muswada huu una vifungu viwili tu.

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa mwaka 2005**
***(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya

Kurekebisha Sheria Mbalimbali wa mwaka 2005 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2005* na imeukubali pamoja na mabadiliko yake. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara Tatu na Kupitishwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niliwaomba waliopo kwenye Kamati warudi kwa sababu tulikuwa wachache kwenye mjadala na kama mnavyofahamu kifungu cha 63(1) kinataka wakati tunafanya maamuzi tuwe zaidi ya nusu na sasa nimeridhika kwamba tuko zaidi ya nusu. Kwa hiyo, maamuzi mmeyapitisha mkiwa mmetimia.

Sasa baada ya maelezo hayo, ningependa pia kuwakumbusha kwamba tunaweka jiwe la msingi mchana huu saa 8.00. Kwa hiyo, wote tuwepo pale hii ni shughuli yetu inatuhusu wote.

Kwa hiyo, wote tuwepo pale wakati jiwe la msingi linawekwa. Baada ya tangazo hilo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.27 Mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

**Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuzuia, Kudhibiti na Kupunguza Silaha Ndogo ndogo na Nyepesi Katika Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika *(The Nairobi Protocol on Prevention, Control and Reduction of Small Arms and Light Weapons in the Great Lakes and the Horn of Africa).***

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha Azimio la kuridhia itifaki ya kuzuia, kudhibiti na kupunguza silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika, naomba kwa ruhusa yako nitoe salamu za rambirambi kwa Familia na

wananchi wa Kasulu Mashariki kwa kufiwa na Mbunge wao Marehemu Frank Mussati. Vile vile kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali waliofiwa na wapendwa wao hivi karibuni, tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze mahali pema peponi roho za marehemu hao. Amen.

Naomba nitoe shukrani kwa Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa uchambuzi, ushauri na ushirikiano mkubwa waliotupa katika kuandaa Azimio hili. Naishukuru pia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na watendaji wake wote kwa msaada waliyotupatia katika kuandaa Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo napenda kutoa maelezo machache kuhusiana na mkataba huu. Tatizo la kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo na nyepesi katika ukanda wa nchi za Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika ikiwemo Tanzania ni kubwa na kwa kiwango kikubwa limesabishwa na migogoro ya kisiasa na kukosekana kwa amani katika baadhi ya nchi hizo.

Migogoro hiyo imesababisha mapigano ya wenyewe kwa wenyewe, na imezalisha wakimbizi hasa katika nchi za Rwanda, *Congo DRC* na Burundi. Vile vile imesababisha ujambazi wa kutumia silaha kuwa mwingi, mauaji na kuongezeka kwa vitendo mbalimbali vya uhalifu wa kutumia silaha.

Aidha kukosekana kwa Serikali nchini Somalia nako kumechangia kwa kiasi kikubwa kuzagaa silaha ndogo ndogo na nyepesi katika eneo lote la Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika. Kwa kutambua hali hiyo tarehe 20 Aprili mwaka 2004 yaani mwaka jana ulifanyika mkutano wa Mawaziri wa Nchi za Nje na wa Mambo ya Ndani wa Nchi za Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika mjini Nairobi. Mkutano huo ulihudhuriwa na wajumbe kutoka nchi 11 ikiwemo Tanzania. Kwa pamoja nchi hizo zilikubaliana kutia saini mkataba wa kushirikiana katika kuzuia, kudhibiti na kupunguza silaha ndogo ndogo na nyepesi katika ukanda wa nchi za Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika, na hivyo kulifanya eneo hili kuwa la amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa Nairobi wa kuzuia, kudhibiti na kupunguza ueneaji wa silaha ndogo ndogo na nyepesi una vipengele muhimu vifuatavyo:

1. Wajibu wa nchi wanachama kutunga sheria zinazokataza utengenezaji, uuzaji na umiliki wa silaha haramu.

2. Kuanzisha utaratibu wa kutunza kumbukumbu za silaha zote ndogo ndogo na nyepesi zinazomilikiwa na Serikali na pia kuwa na kumbukumbu na uratibu wa kuzifuatilia silaha zilizotolewa na Serikali.

3. Kuwa na utaratibu wa pamoja wa nchi wanachama kufanya *operation* za kuzisaka, kuzikamata na kuziteketeza silaha haramu.

4. Kuwa na utaratibu wa vibali au mamlaka ambayo itadhibiti uingizaji na usafirishaji wa silaha ndogo ndogo.

5. Kutoa elimu na kuhamasisha jamii au umma ili wasaidie katika harakati za kupambana na biashara haramu ya silaha ndogo ndogo na nyepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imewasiliana na wadau wengi ambao walikubaliana na maudhui yaliyomo katika mkataba huu. Wadau hao ni pamoja na Wizara na Idara zinazo wakilishwa katika Baraza la Ulinzi na Usalama na zingine zilizoshirikishwa katika kuunda Kamati ya Taifa ya Kuratibu na Kudhibiti silaha nchini. Wajumbe wa Kamati hiyo ni kutoka katika Idara ya Polisi, Uhamiaji, Wakimbizi, Usalama wa Taifa, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais Zanzibar, Ofisi ya Waziri Kiongozi Zanzibar, Wizara ya Sheria na Katiba, Jeshi la Wananchi, Mahakama Kuu, Idara ya Ushuru na Forodha, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Wizara ya Nishati na Madini na Idara ya Wanyama Pori.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo faida nyingi zitakazo patikana kutokana na Bunge lako Tukufu kuridhia mkataba huu wa ushirikiano. Miongoni mwa faida hizo ni kama ifuatavyo: -

1. Ujambazi wa kutumia silaha utapungua na amani katika nchi yetu itaimarika na hivyo kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na hivyo kukuza uchumi wa nchi yetu.

2. Kutakuwa na ubadilishanaji wa taarifa baina ya nchi wanachama kuhusu biashara, utengenezaji na umiliki wa silaha haramu.

3. Nchi zote ambazo zinakubali kutia saini mkataba huu zitakuwa tayari kushirikiana na nchi yetu katika kuzuia na kukabiliana na tatizo la uzagaaji wa silaha ndogo ndogo.

4. Kutunga sheria mpya au kurekebisha baadhi ya sheria zetu ili kuhakikisha kwamba zinazingatia matakwa ya mkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari nchi yetu imeridhia mkataba wa umoja wa *SADC* juu ya Usambazaji wa silaha ndogo ndogo na ule wa Umoja wa Nchi za Afrika pamoja na Umoja wa Mataifa juu ya ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia haya yote Bunge lako Tukufu linaombwa likubali kuridhia mkataba wa Nairobi wa kuzuia, kudhibiti na kupunguza uzagaaji wa silaha ndogo ndogo na nyepesi katika ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika *(The Nairobi Protocol on Prevention, Control and Reduction of Small Arms and Light Weapons in the Great Lakes Region and the Horn of Africa).*

Ibara ya 22 na 23 za mkataba huo zinazitaka nchi wanachama kuridhia makubaliano hayo. Bunge lako Tukufu linaombwa likubali kutungwa kwa sheria mpya au kurekebisha kwa baadhi ya sheria zetu ili kuhakikisha kwamba zinazingatia matakwa ya mkataba.

Baada ya maelezo haya sasa kwa ruhusa yako naomba nisome Azimio lenyewe kama ifuatavyo: Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuzuia, Kudhibiti na Kupunguza Silaha ndogo ndogo na Nyepesi Katika Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika *(The Nairobi Protocol on Prevention, Control and Reduction of Small Arms and Light Weapons in the Great Lakes and the Horn of Africa).*

KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni moja kati ya nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika;

NA KWA KUWA, lengo kuu la itifaki hii ni Kuzuia, Kudhibiti na Kupunguza silaha ndogo ndogo na Nyepesi hivyo kufanya eneo la Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika kuwa ya amani;

NA KWA KUWA, nchi zote ambazo zimekubali kutia saini mkataba huu zitakuwa tayari kushirikiana na nchi yetu katika kuzuia na kukabiliana na tatizo la uzagaaji wa silaha ndogo ndogo na nyepesi;

NA KWA KUWA, kutakuwa na ubadilishanaji wa taarifa kuhusu biashara, utengenezaji na umiliki wa silaha kinyume cha sheria;

NA KWA KUWA, amani katika nchi yetu itaimarika na hivyo kuweka mazingira mazuri ya maendeleo na uwekezaji rasilimali ambao itasaidia kukua kwa uchumi;

NA KWA KUWA, nchi yetu pamoja na nchi nyingine ambazo ni wanachama zitanufaika katika kuratibu programu za kutoa elimu na kuhamasisha wajamii ili kushirikisha umma katika harakati za kukabiliana na uzagaaji wa silaha haramu;

NA KWA KUWA, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado haijaridhia mkataba huu. Kwa hiyo basi, kwa kuzingatia umuhimu na manufaa ya itifaki hii na kwa mujibu wa Ibara ya 63 kifungu kidogo cha 3(e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Bunge hili katika Mkutano wake wa 18 sasa linaazimia kuridhia itifaki ya kuanzishwa kwa itifaki ya Kuzuia, Kudhibiti na Kupunguza Silaha ndogo ndogo na Nyepesi katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika (*The Nairobi Protocol on Prevention, Control and Reduction of Small Arms and Light Weapons in the Great Lakes Region and the Horn of Africa).*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha maoni na ushauri ya Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia itifaki ya Kuzuia, Kudhibiti na Kupunguza silaha ndogo ndogo na nyepesi katika Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika *(The Nairobi Protocol on Prevention, Control and Reduction of Small Arms and Light Weapons in the Great Lakes and the Horn of Africa).*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kutoa pole kwa familia ya Marehemu Frank Michael Mussati na wakazi wa Jimbo la Kasulu Mashariki kwa kufiwa na aliyekuwa Mbunge wao kutokana na ajali ya gari iliyotokea huko Morogoro tarehe 15 Novemba, 2004, Mungu ailaze Roho ya Marehemu Mahali Pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kanuni 98 kifungu kidogo cha 2 ya kanuni za Bunge toleo la mwaka 2003 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Azimio la Bunge la kuridhia itifaki ya Kuzuia, Kudhibiti na Kupunguza silaha ndogo ndogo na nyepesi katika Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha maoni na ushauri wa itifaki hii napenda kumpongeza Mheshimiwa Capt. Mstaafu John Z. Chiligati, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ambaye alishiriki kwa niaba ya Serikali ya Tanzania kutia saini ya kuridhia itifaki hii katika mkutano wa nchi 11 uliyofanyika huko Nairobi tarehe 21 Aprili mwaka 2004. Vile vile nampongeza kwa kuwasilisha kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kina Azimio hili mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru na kuwapongeza wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama kwa kuichambua itifaki hii kwa makini. Kamati imeelewa, kuridhika na kuona umuhimu na ulazima wa kuridhia itifaki hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliangalia nchi ambazo zimeridhia itifaki hii na kuona kwamba kati ya nchi kumi na moja ni nchi nne tu ambazo kwa kiwango kikubwa zinautulivu. Nchi hizo ni Tanzania, Kenya, Seychells na Djibouti, nchi zilizobaki zimekuwa na hali ya kivita kwa miaka mingi nazo ni Ethiopia, Eritrea, Sudan, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burundi na Rwanda.

Aidha Somalia ambayo iko katika ukanda huu kwa muda mrefu haikuwa na Serikali na vyombo vya ulinzi wa Kitaifa. Hivi karibuni ndipo imeundwa Serikali na Bunge nchi hiyo lakini viongozi husika bado wanafanyakazi zao wakiwa nchini Kenya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo ya kivita silaha ndogo ndogo na nyepesi zimezagaa na kuwa mikononi mwa watu kinyume cha sheria kupitia wakimbizi, biashara huria ya silaha hizo na viwanda vidogo haramu vya silaha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imekuwa ikijitahidi kudhibiti kuzagaa kwa silaha hizo ambazo zimekuwa zikitumiwa kwa ujambazi lakini kazi imekuwa nzito kutokana na wimbi la wakimbizi ambao baadhi yao huingia nchini mwetu wakiwa na silaha. Waingiapo huzificha na pindi wapatapo nafasi kuzitumia kwa kufanya uhalifu pamoja na kuziuza kimagendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia itifaki hii Kamati inashauri Serikali kuwa iongeze juhudi za ushauriano za kushauriana na nchi zote wanachama kutafuta suluhu kwa njia ya mazungumzo na kukomesha matumizi ya nguvu katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo ndani ya nchi au kati ya nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, vita na mafarakano katika nchi wanachama kwa kiwango kikubwa vinatokana na viongozi wa vikundi vya kisiasa kutokukubaliana kwa njia ya mazungumzo. Ili kuondokana na hali hiyo Kamati inashauri kuwa Serikali ya Tanzania iwe mfano katika kusimamia kwa ukamilifu sheria na kanuni zinazotawala demokrasia ya vyama vingi vya siasa. Aidha Serikali itumie uwezo wake wote kuzishauri nchi zote wanachama kukutana mara kwa mara kwa lengo la kuzoea kutumia mikutano katika kushughulikia matatizo na kufikia muafaka kwa njia ya kidemokrasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili utekelezaji wa itifaki hii ufanikiwe hatua moja wapo muhimu ni kukomesha mapigano katika nchi wanachama pamoja na kujenga demokrasia inayozingatia utawala bora na utawala wa sheria. Hatua nyingine ni kwa kila nchi mwanachama kutumia elimu kwa jamii, sheria na kuunda vyombo vya kudhibiti kuzagaa kwa silaha hizo na kushirikiana na wanachama wenzake katika kuitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa vyombo vyetu vya habari, radio, televisheni na magazeti ni muhimu katika kuelimisha umma ni vema Serikali wanachama wa itifaki hii zikubaliane na zisimamie kuona kuwa kuna uwiano mzuri katika vipindi vyao. Vipunguze maonyesho ya kivita, ukatili na starehe na badala yake viongozi vipindi vya kuelimisha kuhusu maendeleo ya kiuchumi na jamii.  Kamati inaishukuru Serikali kwa kuleta Bungeni itifaki hii kwa wakati huu ambako inahitajika kweli kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono itifaki hii ya kuzuia, kudhibiti na kupunguza silaha ndogo ndogo na nyepesi, na naomba Bunge lako Tukufu lilidhie ili kuruhusu utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. *MAJOR* JESSE J. MAKUNDI - MSEMAJI WA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kwa ruhusa yako na kwa vile nimesimama hapa kwa mara ya kwanza kwa mwaka huu, naomba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Vunjo na kwa niaba yangu mimi mwenyewe nitoe salaamu za rambirambi kwa ndugu zangu wote waliyopatwa na msiba kati ya mkutano wa 17 wa Bunge na mkutano huu wa 18. Mwenyezi Mungu azilaze Mahali Pema Peponi Roho za hawa Marehemu, Mwenyezi Mungu ndiye anayetoa na ndiye anatwaa.  Jina lake lihimidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nitoe maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu kuridhia itifaki ya kuzuia, kudhibiti na kupunguza silaha ndogo ndogo na nyepesi katika nchi za ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika *(The Nairobi Protocol on Prevention, Control and Reduction of Small Arms and Light Weapons in the Great Lakes and the Horn of Africa).*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kwa mujibu wa kanuni ya Bunge kifungu cha 43 kifungu kidogo cha 5 (b) na kifungu cha 81 toleo la 2004 kuhusu Azimio tajwa hapo huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kabisa kwa niaba ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuunga mkono Azimio hili la Bunge la kuridhia itifaki ya kushirikiana katika ya kuzuia, kudhibiti na kupunguza silaha ndogo ndogo na nyepesi katika ukanda wa Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono Azimio hili tunapenda kushauri Serikali kutilia mkazo katika kudhibiti uingiaji wa wakimbizi kutoka nchi za jirani na kwa kufanya hivyo haitavunja makubaliano ya Kimataifa kuhusu wakimbizi. Pili kuchunguza uhusiano wa wakimbizi na vikundi vinavyopingana na Serikali husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 3 kifungu (c) IV ya mkataba huu kambi ya Upinzani inashauri Serikali kuenzi ujuzi wa wananchi wanaotengeneza silaha ndogo ndogo badala ya kuwachukulia kama waharifu. Watu hao watambuliwe na Serikali kwa kupewa ajira katika vitengo vya Serikali ili kuinua vipaji vyao ambavyo vinaweza kuwa changamoto hata kwa wale wengine wenye ujuzi huo ambao hutengeneza kuuzia wahalifu kwa lengo la kukidhi mahitaji ya familia zao ikiwa sehemu ya kujipatia kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kulipitia Azimio hili linaloridhiwa na Bunge lako Tukufu inaonekana mchango mkubwa ni jinsi ya kudhibiti na kupunguza silaha ndogo ndogo tu. Lakini nchi wanachama zimeshindwa baini ukweli wa chanzo cha uingiaji na matumizi ya silaha hizo katika jamii za nchi wanachama wa mkataba huu. Kambi ya Upinzani inaona ni ukweli usiyo pingika kuwa Azimio hili la Nairobi limeshindwa kubaini ukweli jinsi Tawala zilizomo madarakani zinavyoshindwa kuelezana ukweli jinsi zinavyojenga matabaka katika jamii kwa kuwa na kundi la watawala na kundi la watawaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kundi linaloona halitendewi haki kwani nchi na rasilimali zake ni haki ya wananchi wote na siyo la jamii au kundi fulani, hapo ndipo matumizi ya silaha ndogo ndogo yanapoanza. *(Makofi)*

Hivyo basi kambi ya Upinzani inashauri Serikali ijaribu kuangalia suala zima la political manipulation kwa wananchi wetu lisije likasababisha matatizo makubwa kwani ndiyo chanzo kikubwa katika suala zima la uingizaji na utumiaji wa silaha ndogo ndogo na hata silaha kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kambi ya Upinzani inaona kuwa kutoshirikishwa kwa kundi la vijana ambalo ndilo nguvu kazi muhimu katika ujenzi na uzalishaji *(productive force)* katika sekta rasmi ni sababu nyingine inayosababisha kuenea kwa matumizi makubwa ya silaha ndogo ndogo kama inavyoonekana katika nchi nyingi zilizo wanachama wa Azimio hili.

Hivyo basi tunashauri kuwepo na mipango endelevu kwa kundi hili ambalo linadhaniwa kuwa ni zaidi ya asilimia 45 ya wakazi wa kila taifa husika na mkataba huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo yote marefu kiasi hicho ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge wasemaje wa kila upande wamemaliza, nilitaka kuwataarifu kwamba tayari nina wasemaji nane kwa hili.

Sasa kama wote mnavyojua nia ya bunge tumalize kesi, baada ya hili tuna Azimio la Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni na kesho kuna shughuli nyingine tena. Kwa hiyo, mpaka kesho inatakiwa Bunge tumalize, kwa hiyo nitawaomba wale ambao nitawapa nafasi ya kuchangia wachangie *as brief as possible ili* tuweze kumaliza.

Lakini pia ningependa kuwataarifa kuwa Azimio hili nadhani orodha niifunge hapo watu wanane wanatosha. Wachangiaji ni Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Anatory K. Choya, Mheshimiwa Benito Malangalila, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Gwassa Sebabili na Mheshimiwa Stephen Kazi. Sasa namwita Mheshimiwa Jackson Makwetta, atafuatiwa na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesimama kuunga mkono itifaki hii kuhusu uzuiaji na udhibiti wa silaha ndogo ndogo katika nchi zetu. Nimesikiliza maelezo kutoka kwa Waziri muhusika na kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama na vile vile kutoka kwa Mwakilishi wa Upinzani na nimeelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati Bara la Afrika liliitwa Bara la giza kutokana na Bara hili kutojulikana nchi za ulaya, kutokana na biashara ya kuuza na kununua binadamu, kutokana na maendeleo duni na hali ya usindilela wa Bara la Afrika. Hali hiyo ya kuwa Bara la Giza ilisababishwa kuhararisha vitendo vya ukoloni na ndiyo maana wakoloni wakaingia kutawala Bara la Afrika.

Ni katika karne hii tu Bara la Afrika limepata uhuru wa bendera lakini tabia ile ya ugiza inaendelea, bado kuna dalili za utumwa katika Bara la Afrika, umaskini unazidi kukua, vita baina ya Mataifa vinazidi kuendelea na ndani ya Mataifa, magonjwa ya hatari kama Ukimwi yamezidi kulielemea Bara la Afrika na ndiyo linaloongoza katika dunia, njaa, umaskini na vikundi kama vya janja widi ni vikundi vinavyohararisha ubaguzi wa rangi na kumaliza watu wa kundi moja.

Ndiyo linaloongoza vile vile kwa ukimbizi kwa wakimbizi kuwa wengi katika dunia mpaka tunalia kwamba kuna upendeleo kwamba wale wakimbizi wa rangi nyepesi kule ulaya wanapewa msaada mkubwa zaidi kuliko sisi lakini jibu ni kwamba acheni kupigana vita. Hivi sasa suala la kuingiza silaha ndogo ndogo ni kama ukimwi.

Kwa suala la kuingiza silaha ndogo ndogo ni kama UKIMWI tu au kama vile kuuza madawa ya kulevya, linafanywa kisirisiri. Lakini silaha hizi vile vile zinazalishwa kutoka Ulaya na baadhi ya waathirika ndio wanaonunua silaha kutoka Ulaya na ninajua nchi gani inafanya hivyo. Wananunua kutoka Ulaya na wanauza kwenye nchi hizo ambako tunasema kuna vita na wale wakishaingia kwenye hali mbaya ndio wanauza kama maharage ndani ya nchi kama hizi Tanzania na kufanya tatizo hilo liwe sugu na kubwa na kuhatarisha usalama wa watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimesimama hapa kusema kwamba jawabu la silaha ndogo ndogo katika Bara la Afrika ni Waafrika wenyewe. Unaingiaje kuweka Mkataba wa Kuzuia Silaha Ndogo Ndogo huku unaendelea kuagiza silaha na unaendeleza vita? Kwa hiyo, hatua ya kwanza ni kuzuia vita ndani ya nchi huru ndani ya Afrika, vinginevyo tunapoteza muda tu.

La pili ni aibu ya Bara la Afrika. Vijana wetu, watoto wadogo badala ya kwenda Shule na kuchukua daftari na kalamu unaona wamechukua bunduki wanawinda wenzao kama sungura na ndio mafunzo ya Mwaafrika. Ukiangalia luninga, magazeti hasa ukiwa huko Ulaya ukiangalia Bara la Afrika unaona ni Bara la njaa na mapigano ya vita, umwagaji damu, magonjwa, UKIMWI na ubabe. Ndio Bara la Afrika! Hakuna mambo mazuri katika Bara la Afrika. Kuna wakati niliwahi kusema hapa kwamba Bara la Afrika ni Bara la Balaa *(A Dying Continent),* Bara lisilo na matumaini. Watu wake wanatumika tu katika mambo yote kwa sababu hata hii biashara ya silaha ndogo ndogo kuna wanaofaidika, lakini mtu wa katikati ni mtu mweusi, anachukua kutoka Ulaya anapeleka Congo mpaka Wakongo wenzake wanamalizika hivyo hivyo.

Sasa kuna watu ambao wamegeuza kumwaga damu za watu kama ni kazi ni ajira. *We have professional killers,* wanaua binadamu wenzao na wanasomea kuua binadamu wenzao *in the name of humanity or democracy.* Katika mazingira ya namna hii ukishakuwa na *moral decay* katika jamii ambayo maadili yameoza, inakuwa ni kazi ngumu sana. Kuondoa silaha ni kazi ngumu kama UKIMWI. Maana silaha zinauzwa kwa bei kama ya Bic au kalamu tu. Anauza bunduki ili apate riziki, anapata riziki kwa kuuza silaha kama anauza pipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimesimama hapa kupendekeza kwamba walio na madaraka kwanza wadumishe misingi ya kidemokrasia kwa sababu baadhi ya sababu ni hizo kwamba hakuna haki na kwa kuwa hakuna haki, mtu anaamua kutafuta haki kwa njia ya mabavu. Kwa hiyo tudumishe misingi ya demokrasia.

Pili, tuwaelimishe watu wetu thamani ya binadamu. Mwaafrika hana thamani, sasa anauawa kama kisungura tu. Wadumishie misingi ya demokrasi na tuwaelimishe

watu wetu kuhusu thamani ya binadamu ili kujiepusha na tatizo hili. Tatu, kuwe na operesheni ambayo itaanzia ngazi ya Balozi wa Nyumba Kumi Kumi na kuwekwe utaratibu ambao watu wanaomiliki silaha visivyo halali waweze kupeleka habari hizo kusudi tuweze kuondoa hizi silaha mikononi mwa watu wasiostahili, vinginevyo utakuwa ni ugonjwa usio na tiba na watoto wetu badala ya kufundishwa kushika bunduki wafundishwe kushika daftari na kalamu, Quran na Biblia na kujenga upendo kuliko hii hisia ambayo sasa imejengeka.

Katika *preamble* ya *UNESCO* inasema hivi "Kwa kuwa silika ya vita inastawi katika vichwa vya binadamu, basi silika ya amani ni lazima ijengeke katika vichwa vya binadamu. Ni kwa njia hiyo tu! Bila ya kuwa na elimu iliyo sawa sawa, tutakuwa hatufanyi kazi yoyote ile. Kwa hiyo nasema jawabu la tatizo hili liko kwa waathirika wenyewe bila ya kuchukua hatua. Sasa Bara la Afrika lote litakuwa la janja *weed*. Huu umaskini na njaa, magonjwa na elimu potofu, ukabila na udini utazaa na kustawisha kuwa mbolea ya silaha ndogo ndogo kuzagaa katika Bara la Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**MHE. AZIZA S. ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kwanza nitamke kwamba naunga mkono hoja. Pili, nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuweza kuweka Mkataba katika kuridhia itifaki hii. Hongera sana kwa kuweka saini katika nchi 11 na wewe ukiwa ni mmojawapo kwa kuwakilisha Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu kutoa pole za rambirambi kwa wale wote waliokuwa wamepata matatizo ya kufiwa na wake zao. Mwenyezi Mungu aziweke roho za Marehemu mahali pema Peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia kwa kifupi zaidi kama ulivyotuelekeza. Moja kwa moja naomba nichangie kuhusu kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo katika nchi za Maziwa Makuu na hususan nazungumzia katika nchi yetu ya Tanzania. Nchi yetu ya Tanzania ni nchi ya amani na utulivu. Lakini tatizo kubwa la kuzagaa kwa silaha limeweza kuingia kutokana na nchi yetu kuwa ni nchi ya huruma sana. Maana ya kusema ni nchi ya huruma sana ni kwamba, ni nchi iliyoweza kukubali kukaa na Wakimbizi wanaotoka huko na baadaye wale wale Wakimbizi wanakuja na silaha kuziuza katika nchi yetu kwa bei rahisi zaidi na matokeo yake silaha zile kuweza kutumiwa na wahalifu na kuzagaa katika maeneo mengi zaidi. Kwa maana hiyo, ile huruma ya nchi yetu imetulazimu tukubali na Wabunge wenzangu naomba wakubali kuunga mkono hoja hii kusudi sasa hivi angalau huruma kidogo tuitoe na hii itifaki itakuwa imetusaidia zaidi tuweze kuepukana na janga hilo la kuenea kwa silaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini silaha hizo mpaka sasa bado zipo na kama zipo kuna utaratibu gani wa kuweza kuziondoa au kuweza kuzitafuta ili ziweze kupatikana? Kama tutaridhia tu bila kuzipata zile silaha zilizokuwa zimeshazagaa katika nchi yetu

itakuwa bado tatizo lipo au ni kama tumepanda mbegu ambayo itaendelea kukua. Kwa maana ya kwamba, hizi silaha ambazo zimeshazagaa maeneo yale wanayoishi Wakimbizi mfano Kigoma, Tabora, Rukwa na maeneo mengine, ni maeneo ambayo lazima Serikali yetu itupie macho kuweza kuangalia katika Makambi yao wanayoishi wale Wakimbizi.

Mfano Rukwa, tulikwenda Katumba tukakuta wale Wakimbizi wana madhehebu mengi sana ya Makanisa, lakini wana Kanisa moja kubwa sana ambalo wamelijenga wanaingia watu kama 7,000, lakini wana utaratibu kila mwezi mara moja madhehebu yale yote yanakwenda kukutana ndani ya Kanisa lile. Wanachokiongelea mle na wanachokifanya mle ni mikakati yao ambayo wanaijua wenyewe. Lakini kama sisi ndani ya Tanzania yetu kinafanyika kitu kama hicho lazima tujiulize nini ambacho wanakifanya na kwa nini walijenga Kanisa kubwa kama lile.

Kama kila mtu ana madhehebu yake na wanasali Jumamosi, Jumapili kwenye madhehebu yao tofauti, lakini wanatenga siku moja kwenda kule, hatuwezi kujua nini wanakifanya au mikakati gani wanayoifanya. Tunaweza tukakuta siku moja wanaweza wakatufanyia mikakati hasa sisi wenyewe, tumekaa, tumelala na hatujui silaha wanaziweka katika maeneo gani. Maeneo yale ziko silaha ambazo wanashtakiana na wengine wanakutwa kweli silaha wanazo na wanatoka Kambini wanakwenda kuvamia katika maeneo wanayoishi Watanzania, tuseme kwa sababu wao ni Wakimbizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba suala hili, Serikali iweze kuangalia silaha zile au maeneo yale kwanza yaweze kufuatilia nini wanachokifanya. Maana Mkimbizi toka mwaka 1970 yuko pale mpaka leo bado anajiita Mkimbizi tu na mimi hata kuzaliwa nilikuwa bado sijazaliwa wakati huo, lakini yeye mpaka leo ni Mkimbizi. Kwa hiyo naomba suala hilo liweze kufuatiliwa zaidi. Pia naomba kuwepo na sanduku la maoni katika kila Kata ili kama mtu anaelewa fulani anaweza kuwa na silaha, basi aweze kuandika barua na kutoa taarifa. Maana ya kusema sanduku la maoni ni kwamba, anaweza akatokea mtu akawa na imani ya kusema ngoja nikaeleze katika vyombo vyetu vya dola kuwa fulani ana silaha na ameificha maeneo fulani, matokeo yake akaja akaambiwa baada ya yule kufika kule akasema kuwa fulani ameniambia kwa hiyo inakuwa tayari umeshamhatarishia maisha yake. Kwa hiyo lile sanduku la maoni litasaidia zaidi kuweza kuficha siri na kuweza kumlinda yule mtu ambaye ametoa taarifa katika vyombo vyetu vya dola.

Lakini suala lingine ni suala la kujiuliza hivi hizi silaha zinatoka wapi na zinapatikana wapi? Hizi silaha zipo, maana yake zinatengenezwa na zinauzwa lakini uuzwaji wake unauzwa kwa njia ambayo si halali kama jinsi ambavyo tunavyojiuliza madawa ya kulevya yanatoka wapi na yanauzwa kwa kupitia wapi. Basi na silaha zenyewe nazo zinauzwa kwa utaratibu huo na ndio maana zinazagaa kwa wingi sana. Kwa hiyo ni muhimu zaidi kujua wapi zinapatikana. Bado nasema tunasaini Mkataba huu na tunaridhia hapa Bungeni lakini kule bado zitakuwa zimeingia kama yanavyoingia madawa ya kulevya, watu wanazidi kuathirika na sisi ndio itakuwa ni hivyo hivyo tunaridhia na silaha bado zitazidi kuingia na zitazagaa katika maeneo mengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo ningependa kuuliza ni kwamba: Je, nchi hizi ambazo zimeridhia hii Mikataba ni nchi ambazo zina amani. Tunaweza tukaridhia na wenzetu wakaridhia kama wanavyodai lakini wao wakawa hawana amani, kila muda kutakuwa na vita. Kwa hiyo ile vita itasababisha bado silaha zizidi kuzagaa. Silaha zinapozidi kuzagaa itakuwa hakuna maana ya wao kusaini Mkataba huu. Lazima na wao kwenye Mikataba yao wanaposaini kuwepo na kifungu kinachosema, lazima nchi zote ziwe na utaratibu wa kupunguza vita kusudi huu Mkataba uwe na maana thabiti kabisa. Kwa sababu kama tutakuwa bado tunasaini Mkataba wa kupunguza kuzagaa kwa silaha na bado nchi hizo zitakuwa zinapigana vita, itakuwa maana nzima ya Mkataba huu na kusaini wao na sisi itakuwa hakuna utaratibu kwa sababu wao watapigana, watakuja kwetu na sisi tutawalea. Maana utaratibu huu wa kukimbia, wenzetu wa maeneo fulani kule ya Pemba na Zanzibar walikimbilia Shimoni kule. Sasa wao walijua ni sawa na nchi yetu ya Tanzania ilivyo. Nchi yetu ina amani na utulivu, kwa hiyo na kule walivyokuwa, wakaenda wakajua na kule kuna amani, utulivu, watakula tu, watalala, lakini wamefika Shimoni maisha yakawa magumu zaidi wakaona hapana, wacha tu turudi nyumbani bila hata kuitwa. Kwa hiyo na sisi kama watakubali Mkataba huu kuusaini na kupunguza vita huko kwao, kwa hiyo itakuwa na maana nzima ya kuridhia Mkataba huu bila ya matatizo kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja ili niweze kukubali yale uliyosema tuchangie kwa ufupi. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ANATORY K. CHOYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hoja hii iliyopo mbele yetu ya kuridhia Azimio la Bunge la Kuridhia Itifaki ya Kuzuia na Kudhibiti na Kupunguza Silaha Ndogo Ndogo na Nyepesi.

Awali ya yote kabla sijachangia naomba kwa niaba ya wananchi wa Biharamulo Magharibi nitume salamu za rambirambi kwa familia, ndugu jamaa na wananchi wa Kasulu Mashariki kwa kifo cha mpendwa wetu Frank Mussati. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema Peponi. Amin.

Vile vile, kwa wale Waheshimiwa Wabunge waliofiwa na Wapendwa wao, hiyo ni mipango ya Mungu, tumetanguliana na aliyetangulia tunamwombea apokelewe na Mwenyezi Mungu. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo niunge mkono hoja asilimia zote. Katika kuridhia hili Azimio ili utekelezaji uwe na manufaa lazima kila nchi ambayo inahusika ihakikishe inawaambia na kuwalazimisha au kutunga sheria ambazo zitahakikisha wananchi wanamiliki silaha hizo ndogo ndogo kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi ile. Bila hivyo kama ilivyo Somalia, Somalia sasa hivi pamoja na kwamba ina Serikali lakini Serikali ambayo iko nje hiyo si kitu. Wale wananchi wa Somalia wanakaa tu kama hawana baba wala mama, kila mmoja anajifanyia mambo yake. Kwa hiyo yale yote yanayofanywa kule yanafanywa bila Kiongozi yeyote. Kinachotakiwa hapa ni lazima sasa utekelezaji wa Azimio hili uhakikiwe na utungaji wa sheria ambazo zitahakikisha wale wananchi wanazifuata ipasavyo.

Nilikuwa kule kwenye *internet* nimesoma ripoti moja ambayo imeandaliwa na *United Nations Conference on the illustration on small arms and light weapons in all aspects* ambayo ilifanyika *New York* tarehe 9 mpaka 20 Julai, 2001 ambayo inaonyesha kabisa mlolongo wa Mikutano yote, makongamano na warsha zaidi ya 40 ambayo yameshafanyika na hayo yote yametumia fedha. Lakini katika hizo nchi zinazohusika, hizi nchi za Maziwa Makuu na nchi za pembe ya Afrika sijajua kama wale wananchi wameshajua hata hilo Azimio kama lipo. Kwa hiyo unaweza ukashangaa kwamba inavyoonekana, watu wasiohusika na tatizo ndio wanakwenda kuzungumzia mahali ambapo hata kule mahali kunakotokea matatizo hayo hawapaelewi. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba ili wananchi wa pale nao waweze kusaidiwa kwa namna moja au nyingine, wanatakiwa wahusishwe kwa namna moja au nyingine.

Kwa mfano kuna suala la Wakimbizi, huwa mimi naziita hizi nchi ambazo zinazalisha Wakimbizi ni viwanda vya kuzalisha Wakimbizi. Hizi nchi ni pamoja na Rwanda, Burundi na Congo. Hivi ni viwanda vya kuzalisha Wakimbizi. Mara kwa mara huu huwa ni mradi wa *UNHCR*. Kama usingelikuwa ni mradi wa *UNHCR* ina maana hili suala lingekuwa limeshakwisha.

Mimi nafikiria kwamba ifike mahali sasa Shirika linalohudumia Wakimbizi liwatengee maeneo wale Wakimbizi ndani ya nchi zao kuliko kuwaruhusu mara wanapopigana tu wanakimbia na kwenda kutoa adha, kusababisha maafa katika nchi kama ya Tanzania ambayo ina amani, utulivu na mshikamano. Kwa hiyo watengewe huko huko wajengewe makambi ya kudumu kuliko sasa hivi, maana yake wale ndugu zetu Wanyarwanda na Warundi kama itatokea siku wakatulia, nafikiri labda itakuwa ni jambo la ajabu katika dunia hii namna walivyo.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa naomba kwamba watengewe maeneo ya kwao huko huko. Halafu Serikali za nchi zinazohusika lazima ziimarishe mipaka na Viongozi wanaohusika wakiwemo Viongozi wa ngazi za juu lazima waheshimu mipaka. Kama Uganda inaweza ikavuka mpaka ikaenda mpaka Congo, huo ni uvamizi. Kama Rwanda inaweza ikaenda mpaka Congo, huo ni uvamizi. Kwa hiyo Viongozi wa Afrika lazima tuheshimu mipaka. Tuheshimiane, tuthaminiane, vinginevyo bila kuheshimu hiyo mipaka tutaendelea kupigana, kuumizana sisi kwa sisi. Tutafanana kama alivyosema Mheshimiwa au kama mnavyofahamu sisi kwetu kuna senene. Senene kawaida unapokuwa unawashika unawaweka kama lambo hivi . Sasa badala ya kutafuta namna ya kutoka kwenye lambo, wao wanaanza kukatana matumbo na matokeo yake wanakufa. Ndilo Bara la Afrika ni senene tu! Hakuna ambaye hakusoma. Wote kama unataka kutafuta uongozi, wewe hujui kama unamuua ndugu yako wala rafiki yako, wala jamaa yako, ili mradi tu unatafuta Uongozi.

Kwa hiyo lazima tuheshimiane, tuthaminiane tupendane na lazima Viongozi ifike mahali tuheshimu mipaka, vinginevyo tutakuwa tunaonekana kwamba sisi ni kichwa cha mwendawazimu tu. Wale wanatengeneza silaha tunaletewa sisi, tunanunua tunaumizana na tunauana sisi kwa sisi na elimu tunayoipigania haitusaidii wala haionyeshi umaana wake.

Vile vile, nilikuwa napendekeza kwamba, kwa sasa Serikali ihakikishe inafanya tathmini ili kujua madhara yaliyosababishwa na uzagaaji wa hizi silaha. Ikiwezekana wale wananchi walioathirika kwa namna moja au nyingine wapate fidia. Chukulia mfano halisi katika maeneo ambayo yameshavamiwa na Wakimbizi Mkoa wa Kagera, Kigoma pamoja na Rukwa, nichukulie tu mfano mdogo katika Wilaya ya Biharamulo Kata moja inaitwa Nyakahura. Hiyo Kata nimekwishasema mara nyingi ni kwamba wananchi wote kwenye Vijiji mbalimbali kwa mfano Kijiji cha Mihongora, Nyabungombe, Kijiji cha Mji Mkongwe, wananchi wote wameshahama na wameshakimbia. Vijiji vyote vimebaki wazi kwa sababu wananchi wanavamiwa mara kwa mara.

Kuna Kijiji hicho cha Mji Mkongwe kinaitwa Nyakahura, juzi juzi nimepata simu kwamba wananchi wote wameshahama wamekiacha Kituo cha Afya mpaka kimehama na Kituo cha Polisi. Sasa wananchi wamebakia hewani. Ninamwomba Mheshimiwa Naibu Waziri katika kufanya majumuisho ahakikishe anatoa maagizo katika Wilaya, Kituo cha Polisi kiwe pale kwa ajili ya kuwanusuru wananchi wa Kata hiyo ya Nyakahura, vinginevyo wale wananchi sasa wataendelea kubaki maskini kwa sababu hawana muda wa kufanya kazi za kujitegemea.

Jambo lingine, Serikali kama alivyosema lazima iimarishe mipaka ya Tanzania ni kama debe ambalo lina matundu mengi. Ni mahali tu ambapo kuna Vituo vya Uhamiaji ambavyo mnaweza mkazuia *illegal immigrants.* Sasa ni lazima Serikali iimarishe mipaka yake. Iimarishe vyombo vyake vya Ulinzi na Usalama ikiwemo Idara ya Uhamiaji, Polisi wapewe nyenzo za kufanyia kazi. Sasa hivi nilikuwa najiuliza kwamba wakati mimi nasoma naambiwa kwamba Mkimbizi lazima akimbie kutoka mlango huu wa kulia aingilie mlango wa kushoto hapo hapo. Lakini kwa sasa nasikia wanasema kwamba na Wasomali ni Wakimbizi. Sasa Msomali atakuwaje awe Mkimbizi hawezi akavuka kutoka Somalia, akaja Kenya akavuka akaja hapa akaitwa hapa Mkimbizi. Kwa hiyo dhana na tafsiri sahihi ya ukimbizi lazima iendelee kuwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi ukienda pale Dar es Salaam katika kila Hoteli zile za kitalii utakuta wahamiaji haramu ndio wafanyakazi wa pale. Kila sehemu ya kazi utakuta wahamiaji haramu ndio wanaokwenda kufanya kazi pale. Sasa lazima Idara ya Uhamiaji iimarishwe, Polisi waimarishwe wapewe nyenzo za kufanyia kazi halafu na Polisi katika kufanya kazi zisifanye kazi kama Zimamoto. Kwa bahati mbaya Polisi wanafanyakazi baada ya maafa kutokea ndipo utawaona wanafanya kazi. Lazima i-*detect* mapema kabla ya makosa kutokea iwe imeshajua kwamba iwajibike kwa utaratibu upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa kumalizia niseme kwamba Itifaki hii utekelezaji wake ndio utakaosaidia nchi au Bara la Afrika au nchi za Maziwa Makuu ziwe na amani, utulivu na mshikamano, bila hivyo, tunafanya kazi bure. Naunga mkono hoja asilimia zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru kwa kuweza kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyoko mbele yetu ya

kuridhia Azimio hili la Bunge la Itifaki ya Kuzuia Kudhibiti na Kupunguza Silaha Ndogo Ndogo Nyepesi katika nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu na pembe ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa mimi naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. Ni Azimio jema ambalo lina lengo la kuleta usalama katika maeneo yetu. Lakini nilikuwa na wasiwasi, hivi tunapozungumzia silaha hizi zinazoitwa silaha ndogo ndogo na nyepesi kwa sisi raia ambao hatuna utaalamu wowote wa kiaskari, ni silaha za namna gani? Ninamaanisha *definition* ya hizi silaha ndogo ndogo na silaha nyepesi nyepesi maana tunaweza tukatoka nje ya uchangiaji kumbe tunachangia silaha kubwa. Maana mimi nadhani silaha ndogo ndogo labda ni rungu, fimbo au visu vidogo vile vya kukatia nyama. Kwa hiyo nadhani pia Mheshimiwa Waziri wakati akihitimisha Azimio hili atueleze silaha ndogo ndogo ni kitu gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu waliotangulia wamezungumza mambo ya msingi sana na mimi niseme, sisi sote tumeishi katika mazingira ya amani na tusingependa tukafika mahali ambapo yanajitokeza matukio ambayo yanatupa wasiwasi katika kudumisha amani tuliyonayo. Sasa mimi nilitaka kusema kwamba hiki kitu huenda watu wasiwe wanakifahamu, lakini tunawakaribisha Wawekezaji. Wawekezaji wanavyokuja kuwekeza kwenye nchi yetu tumewapa nafasi ya kuamua mambo mengi sana. Hawanunui vyakula kwenye masoko yetu, wanasema viwango vya ubora viko chini, hawapati huduma za msingi kutoka kwenye maeneo ambayo yanatoa huduma ambayo yanamilikiwa na Watanzania wakidai ubora wa huduma zetu au bidhaa zetu haukidhi viwango vyao wanavyohitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kitu cha ajabu sana, mimi nina mfano wa *Kahama Gold Mine,* wale wawekezaji wa *Kahama Gold Mine* waliagiza walinzi kuja kulinda ile *mine* pale na wale walinzi wakawa wanahitaji kuingia na silaha zao nchini. Sasa napatwa na wasiwasi kwamba tukifika mahali ambapo hata wawekezaji sasa wanashindwa kuamini kwamba kuna ulinzi wa kutosha kwenye nchi yetu, wanaanza kufikiria kwamba ni lazima walete walinzi kutoka kwenye nchi zao, walinzi hao wanapokuja kutoka huko wanakuja na silaha zao, nadhani tutafika mahali ambapo ni pa hatari sana. Nadhani suala hili linajulikana ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani, sijui kama hawa watu walishapewa vibali vya kuingiza hizo silaha au hawajapewa. Lakini nadhani kama vibali vilitolewa, basi hili Azimio halitusaidii sana. Lakini kama walizuia wale watu kuingiza silaha zile, nadhani walifanya kitu ambacho ni kizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ninachotaka kusema ni kwamba kwa namna moja au nyingine ni lazima tudhibiti uingizaji wa silaha. Maana yangu ni kwamba pia utoaji wa leseni za kumiliki silaha ni lazima uangaliwe kama sheria ya zamani ambayo inawezesha raia wa Kitanzania kumiliki silaha au raia wa kigeni ambaye yuko ndani ya Tanzania kumiliki silaha tuangalie upya sheria hii kama bado inakidhi mahitaji ambayo tunayo sasa hivi.

Kwa hiyo, nasema kwamba tuna umuhimu wa kutazama hilo kwa sababu hata sisi Watanzania wenyewe ambao tunapewa vibali vya kumiliki silaha, mtu anakwenda dukani ananunua silaha yake hajawahi kupewa mafunzo ya kutumia silaha yenyewe. Bahati

nzuri sisi wengine tumepitia *National Service* tuna nafuu na wale waliopitia mgambo wana nafuu. Lakini kuna watu wanamilikishwa silaha na hawajapata mafunzo sehemu yeyote. Sasa mimi nadhani ile silaha haimsaidii hata yule anayeimiliki, badala yake ndiyo wengi tunasikia wakikutana na majambazi au watu wenye nia mbaya tunasikia wamenyang'anywa silaha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilidhani kuna umuhimu wa kuangalia hii sheria. Ni vyema Serikali ikaweka sharti la hawa watu wanaotaka kumiliki silaha kwa kujilinda, wapitie mafunzo maalum ya kuwawezesha kutambua namna ya kuzitumia silaha zenyewe na ni mazingira gani ambayo watahitajika kutumia silaha maana kuwa na silaha haimaanishi kwamba ukishakutana na mtu, basi wewe utoe silaha uanze kuitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilidhani sheria hii ya kumiliki silaha ingebidi iangaliwe upya, maana silaha nyingi sasa ziko mikononi mwa watu ambao kwa kweli ukitazama katika hali ya kawaida hawakuwa na sababu ya kumilikishwa silaha na wakati mwingine hata kama wamemilikishwa silaha hawazitumii kwa makusudi yaliyokusudiwa. Wakati mwingine mtu akikamata mke wake ugoni anakwenda kumtishia mgoni wake nitakupiga na *pistol*. Sasa hayo siyo matumizi ya kumiliki silaha hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo nilitaka kuchangia hapa wenzangu wamezungumzia kuhusu uzagaaji wa silaha kwenye maeneo ya mipaka. Hili ni suala ambalo ni la msingi sana. Nadhani tungedhibiti uingiaji wa Wakimbizi kwenye mipata yetu. *(Makofi)*

Ukifika Kigoma nadhani silaha sijui kama ndiyo kubwa, sijui *sub machine gun* zile ni kubwa, silaha zimezagaa sana kwenye Mikoa ya mipakani na Mkoa mmojawapo ni Kigoma. Tuseme kwamba kama tunapata matatizo ya matumizi mabaya ya silaha, siku moja Mikoa itakayoathirika mmojawapo ni Kigoma.

Nimemsikia rafiki yangu Choya hapa amezungumza vizuri tu maana yeye alikuwa Afisa Uhamiaji anajua matatizo ya mipakani watu wanavyoingia na kadhalika. Kwa hiyo, nadhani kuna umuhimu wa kudhibiti sana mipaka yetu. Kwa sababu chanzo kikubwa cha silaha hizi zinaingizwa na Wakimbizi hasa kwenye maeneo mipaka ambayo tunapakana na Rwanda na Burundi kuna tatizo kubwa pale. Kwa hiyo, nadhani Serikali ingeongeza kidogo uangalizi wa maeneo haya ya mipaka ili tuweze kuwa na Wakimbizi wanaoingia bila silaha, kama wataendelea kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimehudhuria Vikao vya mambo ya upunguzaji wa silaha ndogo hapa Tanzania na nje ya nchi, kuna suala hili la hawa Watanzania ambao wana ubunifu wa kutengeneza haya yanayoitwa magobole: Hivi, kwa nini huu ubunifu sisi tunauacha tu badala yake tunatunga sheria tu za kuwadhibiti? Kwa nini tusitumie huu ubunifu tukawaendeleza hawa Watanzania wakapatiwa leseni na wakaruhusiwa kushirikishwa katika Sekta iliyo rasmi kwa maana kwamba, uandaliwe utaratibu ambao wanaweza wakakuza hivyo vipaji?

Uuzaji wa silaha ndiyo biashara kubwa kwenye nchi ambazo zinajiita nchi zilizoendelea. Sasa leo sisi tumeweka sheria ambayo tukikuta mtu ana gobole tunaanza kumkamata. Sawa ni sheria ipo, lakini inakidhi mahitaji? Kwa nini hawa watu tusiweze kuwaendeleza kupitia kwenye Taasisi zetu? Kwa mfano, tuna Kiwanda kile cha Jeshi cha Mzinga, watu wa namna hiyo wakapelekwa kule wakaendelezwa ili waweze kutengeneza silaha ambazo zinaweza kuwa pia ni bidhaa tukauza kwa nchi nyingine ambazo zina matatizo ya vita sehemu zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ulituomba tuzungumze kwa kifupi sana na nisingependa kutokufuata mwongozo wako kwa sababu ni wa msingi ili tuweze kukamilisha kazi nyingine. Kwa hiyo, haya ndiyo ya msingi niliyokuwa nayo.

Lakini kubwa zaidi ni suala la umilikaji wa silaha ambao kwa kweli tunadhani kuna umuhimu wa sheria kuangaliwa upya na watu wanaomilikishwa hizi silaha wawe ni watu ambao kwa kweli wamepewa mafunzo na ni watu waaminifu na waadilifu. Matukio ambayo yanatokea sasa hivi kwenye nchi hii ya ujambazi, uhalifu wa kutumia silaha yameongezeka na hii ni dalili kwamba silaha hizi ndogo ndogo na nyepesi ziko mikononi mwa watu wasio waadilifu kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, nadhani hili litapewa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kwa jioni ya leo. Kwanza, napenda nitoe salamu za rambirambi kutokana na kifo cha ndugu yetu, mwenzetu Marehemu Frank Mussati. Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi. Amin.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, napenda nikubali kwa ukamilifu wote kuungana mkono na wenzangu katika kuunga mkono Itifaki hii. Hivyo naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli leo nitazungumza kwa ufupi sana na Mungu anisaidie. Nina maswali matatu. Swali langu la kwanza ambalo limenifanya nisimame kuzungumza kwenye Itafaki hii, ni tafsiri ya silaha ndogo ndogo, bado ni msamiati hasa kwa Wapigakura wetu. Kuna rafiki zetu ambao ukishazungumza silaha ni moja ya vazi lake, kwa mfano Mmasai hawezi akakamilika bila kuwa na mkuki, bila kuwa na rungu.

Sisi kule nyumbani ni wafugaji, huwezi kwenda kuchunga ng'ombe huna rungu, fimbo, panga, manati au shoka, ni vitu vya kawaida ambavyo vyote hivyo ni silaha. Sasa unapozungumza kwamba tunapunguza silaha ndogo ndogo, kwa mtu wa kawaida kwa mfano kwa rafiki zangu Wamasai na Wasukuma, basi wasiendelee na mikuki, wasiwe na mishale, wasiwe na panga, wasiwe na fimbo. Sasa mimi ningedhani labda kwa sababu Kiswahili bado kinakua, tusingetumia neno silaha ndogo ndogo. Ningedhani Waziri

atumie silaha za kiwandani au silaha za kisasa au silaha za moto au silaha zinazoua haraka. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo, swali langu la kwanza ni tafsiri ya neno hili, silaha ndogo ndogo anatafsiri vipi. Anaunganisha na hizi silaha zetu za kienyeji kama mapanga, mikuki, manati na kadhalika? Ndiyo swali langu la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili katika kujadili Itifaki, anasema kwamba uzuaji kudhibiti na kupunguza, lakini Serikali haijafafanua ni namna gani inashiriki katika kuzuia, kudhibiti na kupunguza; wenzangu wametangulia kusema na sipendi nirudie sana, vyanzo vya upatikanaji wa silaha hizi ni pamoja na vita ambavyo vinatokea kwa majirani zetu, pamoja na vurugu mbalimbali ambazo wanafanya majirani zetu wa Maziwa Makuu na pembe ya Afrika. Lakini mimi nadhani Serikali yetu na yenyewe inashiriki kwa sababu tumekuwa wapole mno wa kukaribisha kila namna ya Wakimbizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kule kwetu, kuna makambi yapo tangu miaka ya 1970 na wale watu hawarudi. Lakini upo msemo unaosema kwamba usiku wanarudi wanakwenda kule katika nchi yao, usiku kwa usiku wanasafiri wanarudi kuonana na jamaa zao na wao ndiyo chanzo kingine cha kuleta silaha katika nchi yetu. Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza kwamba Serikali iseme bila kuwa na kigugumizi kwamba sasa Wakimbizi waende kwao wote, hata hao waliokuwepo miaka ya 1970, hata hao waliokuja juzi wote waende kwao. *(Makofi)*

Kule kwao iwe marufuku kukimbia, wamalizane huko huko kama wanavyofanya Wapalestina na Waisraeli. Mbona Waisraeli na Wapalestina hawakimbii, wabaki huko huko? Pengine katika hilo watajifunza, watakaa kwa amani. Kwa hiyo, pendekezo langu la kuzuia, kudhibiti na kupunguza nilikuwa natoa hoja Serikali isiwe na kigugumizi, isione wasiwasi, itamke wazi wakimbizi sasa basi! Wanapigana kwa sababu wanajua watakimbilia wapi. Lakini tukifika mahali ambapo wanakosa pa kwenda, basi itasaidia kuzuia na hatutaona silaha nyingi namna hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu na mwisho katika Azimio hili la Nairobi, mimi nadhani niamini kwamba hata nchi za Uganda na Rwanda zilikuwepo. Lakini mimi sijawahi kusikia hata siku moja Serikali au nchi za Afrika Mashariki au Jumuiya za Maziwa Makuu zimeikemea Uganda au Rwanda. Nchi hizi mbili ndiyo wachokozi wakuu hasa kwenye vita hizi za Congo pamoja na Burundi. Kwa nini tunaogopa kusema ukweli kuwakemea Uganda na kuwakemea Rwanda kwamba waache uchokozi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema nitazungumza kwa kifupi. Nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa machache niliyonayo kuhusu Azimio hili.

Kwanza, naomba nitoe shukrani kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Kasulu, niwashukuru wale wote walioshiriki katika msiba wa ndugu yangu Marehemu Frank M. Mussati. Nawashukuru kwa hali na mali walizozitoa, hatuna la kuwalipa lakini tunamuomba Mwenyezi Mungu awaongezee zaidi. Lakini pia naomba nitoa pole kwa ndugu yangu Mheshimiwa Arcado Ntagazwa ambaye amefiwa na mke wake pamoja na ndugu zetu wengine Mheshimiwa Parmukh Hoogan, pamoja na ndugu yetu Mheshimiwa Benito Malangalila.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja kama ilivyotolewa kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vita baina ya nchi na nchi vimezidi kuwa nyingi katika Afrika. Silaha za kivita pamoja na silaha ndogo ndogo zimekuwa nyingi sana. Silaha hizi hazitengenezwi Afrika, zinatengenezwa Ulaya. Kwenye Mikataba mingi ya Kimataifa ambayo inajumuisha ile ya *Weapons of Mass Destruction* yote inatuomba sisi tukubali yafuatayo; nitanukuu kwa Kingereza. Wanasema tuyakubali haya kama *an essential element* ya mashirikiano yetu sisi na nchi za Ulaya. Naomba ninukuu *"Both manufacturing, proliferation and stockpiling of weapons and their means of delivery represents one of the most serious threats to international peace, security and stability"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno haya ni sahihi kabisa. Sisi tumekuwa tukiyasikia lakini hatuyafanyii kazi. Maana athari zake ni kubwa sana. Athari hizi zinafanya sasa hali ya amani na utulivu kwa nchi maskini, nchi ambayo ilikuwa ina msimamo mzuri kama Tanzania, amani na utulivu uonekane kwamba sasa imeanza kupotea. Azimio hili ni mwanzo wa kushughulikia matatizo ya amani, yanaweza kuvuruga amani yetu na utulivu katika nchi yetu. Ni mwanzo wa kushughulikia matatizo ya kuleta amani na utulivu katika Afrika. Masuala muhimu ya amani na utulivu lazima tuyaangalie. Amani ya Afrika iko mikononi mwa Waafrika wenyewe. Chuki ndani ya Waafrika imekuwa ni kubwa sana. Chuki hii imejengeka ndani ya ubinafsi. Ukitaka kitu ukikikosa unakimbilia kuomba msaada wa silaha wa kivita huko Ulaya. Ukipata silaha hizo unakuja kuwamaliza ndugu zako kisha unataka madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawapa mfano. Mimi kwa ridhaa yenu nilichaguliwa kuwakilisha *ACP Countries* katika Kamati Maalum ya Kushughulikia amani katika nchi ya *Cote d'Ivoire.* Tulipokwenda Cote d'Ivoire tulielezwa habari ya mtu mmoja ambaye kwa miaka 20 alikuwa anaua watu. Walipoomba wasuluhishwe, wakaenda Ulaya kupata usuluhishi kule, wakaingia kitu kinaitwa *The Lenus Marcus agreement. In that agreement one of those individuals* aliyechaguliwa kwamba awe ndiye *Minister of Defense and security* ndani *ya Cote d'Ivoire* alikuwa ni huyo bwana aliyekuwa anaua watu kwa miaka mingi. Wakamlazimisha kwamba lazima ukamuite. Mwingine alikuwa mtoto wa miaka 30, lakini anazungumza Kifaransa kizuri. Tuliingia Ofisini kwake tukakuta anazungumza na Wazungu nje analindwa Maaskari wa Kifaransa. Tukasema *what is this? Is it all about?* Lakini kwa sababu kwenye ule Mkataba wameweka kipengele kwamba lazima yeye apewe nafasi ya Uwaziri katika Serikali ile, L. Balbo *President* wa *Cote d'Ivoire* akasema: "Nitakubali masharti mengine lakini hili la kumpa huyu ambaye najua ni muuaji mkubwa sitakubali *over my dead body.*" Akakataa. Kamati

ya *European Union* ilipoingia Ikulu, Laura Bagbo alizungumza kwa nguvu zake zote, Wazungu wakamwelewa kwa nini msimamo wake ulikuwa huu aliokuwa anausema. *(Makofi)*

Lakini chuki hizi ambazo tunazo ni kwamba zinaendelea habari hizi. *Cote d'Ivoire* siwezi kuziendeleza maana ni hadithi ndefu. Chuki zetu ndani ya Afrika hazitatufikisha kokote, ndiyo hii mnazungumza mtu anaondoka anakwenda kupigana na nchi nyingine, anachotafuta ni kwa sababu kaambiwa na mtu waUlaya nenda kaniletee hiki. Leo hii tunapozungumza niwaambieni dhahabu ya *Congo, Antiwerp* ni *the cheapest*. Ukienda Burundi kuna dhahabu nyingi na bei yake ni rahisi. Kama unataka unafanya biashara hiyo, nipitie nitakuonyesha jinsi ya kuipata. *It is very cheap! Why?* Kwa sababu lile ni eneo ambalo limetawala na hawa Waganda na Wanyarwanda na ndiyo wanachopigania.

Ile dhahabu inayotolewa Burundi, kupata leseni yake ni Dola 5,000. Ukishapata leseni dhahabu yenyewe ni *cheap*. Soko lake kubwa liko Antwerp kule Belgium. Kule imeshusha hata bei ya dhahabu duniani, maana watu wengi wanakwenda kuinunua kule. Lakini ni mali yetu ya Afrika ambayo inapelekwa, sisi tunasahau kwamba *this is our property* na watu wanapigania mali yetu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoendelea hivi sasa ni kwamba tunalo Azimio hili, lakini kinachofuata *we shall soon be required to sign an agreement on weapons of mass destruction.* Katika mazungumzo na *European Commission already we have been asked to include weapons of mass destruction* kama *article* maalum na *an essential element of the Cotonou agreement,* hufanyi hivyo, hakuna msaada.

Lakini mambo matatu ambayo ni muhimu katika hili, moja ni *manufacturing,* lakini ya pili ni *proliferation* na ya tatu ni *stock piling*. *Who does all these*? Ni Afrika? Ni Caribbean? Ni Pacific? Hapana! Yote haya yanafanywa na hawa. Hizi *small arms* nani anazo? Ndiyo maana nasema hii ni hatua ya kwanza ya kushughulikia amani na utulivu wa Afrika. *Now we are being forced* katika hii. Hivi sasa *statement* ya *ACP countries* wamesema hivi: *"The ACP group of countries cannot accept weapons of mass destruction as an essential element of the Cotonou agreement. The parties considered that both manufacturing proliferation and stock piling of weapons of mass destruction and their means of delivery both to state and none state actors represent one of the most serious threats to international peace."* Lakini *who does this?*

Naomba niseme: *More recently* Tanzania ilishitakiwa kwenye Mikutano ya huko Ulaya kwamba Tanzania ime-*import* Kiwanda cha Kutengeneza Silaha hapa nchini. Sasa mimi katika Mikutano ya *ACP* na *EU* ndiyo Msemaji wenu Mkuu tulileta taarifa kueleza hii hali ilipotokea na mimi nilipata nafasi ya kujibu. Sasa nilitaka kuwasomea *statement* niliyotoa bahati mbaya ile *statement* niliyotoa pale sina. Lakini nilichokisema pale na *feedback* iliyokuwepo ya utaalam wa ndani ya nchi ni kwamba ziko nchi kule Ukraine (Urusi) zilikwenda zikanunua kiwanda hicho lakini zile leseni na *documents* nyingine ziko kwenye jina la Tanzania. Sisi wakati huo tukafanya mpango kuwasiliana na wale

tukawaambia haya ndiyo yamekuwa yanatokea, tunaomba mwulize, bahati nzuri walipowauliza wakakuta na Serikali yetu imeshafanya hivyo. Lakini ndiyo *proliferation of weapons* ambayo imekuwa katika dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda nizungumze mengi lakini nafikiri haya yanatosha kwa muda wako uliosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kasulu na Wakimbizi wa Burundi, mimi naomba Serikali ilichukue *seriously* hili nitakalolisema. Ninaomba Serikali ifanye msako, silaha zimezagaa sana Mkoa wa Kigoma na Kagera watu wanakufa ovyo na kunyang'anywa mali zao. Baada ya mimi kuwasilisha hoja binafsi ile ya kuomba Serikali ifanye utaratibu na ikafanya kazi nzuri katika Wilaya ya Kasulu, hivi sasa tuna matatizo ya watu kununua silaha mpakani. Silaha aina ya *SMG* ni Sh. 200,000/=, watu wanapata mpakani pale na wanashirikiana na Warundi; kwa nini hatuwafuatilii hawa Warundi walioko kwenye Makambi? Lakini wanavuka wanakwenda Burundi wananunua hizi silaha wanakuja nazo. Amani yetu iko mashakani kama tutaendelea kuachiachia mambo tu na watu wetu wataendelea kula rushwa tu, wanawaachia hawa watu wanaofanya mambo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naunga mkono hoja ya Azimio hili. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nilishatoa rambirambi zangu wakati nilipokuwa nikichangia katika Miswada ya nyuma. Kwa hiyo, naomba niendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuwa akitoa maelezo kuhusu Itifaki hii nilitegemea atatuambia chanzo hasa cha silaha kuzagaa katika eneo la Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika, lakini hakufanya hivyo. Lakini naomba niseme machache kuhusu kitu hicho. Silaha zimezagaa kutokana na Wakimbizi, umaskini, ukosefu wa ajira na uroho wa baadhi ya Viongozi wa nchi za Afrika kung'ang'ania madaraka. Sasa sijui Itafiki hii ilipokuwa inawekewa sahihi kule Nairobi ni utaratibu gani uliofanyika kujaribu kupunguza matatizo haya ambayo yanalikabili Bara la Afrika kwa uzito mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hauwezi hata siku moja ukazuia mtu kuiba. Kama ana njaa ataiba tu hata kama ni kupigwa risasi, atakuwa tayari kupata hiyo aibu ya kupigwa risasi na akifa atakuwa ameondokana na aibu, lakini ataendelea hivyo. Masuala haya, Viongozi wetu wa Kiafrika wanayashughulikia sasa na hasa baada ya Afrika kuungana. Lakini yanahitaji kwa upande huu msimamo mzito kulingana na maeneo ya Maziwa Makuu, hali ya hewa ya kisiasa ilivyo, hali ya hewa ya uchumi ilivyo na hali ya mila na desturi za makabila zilivyo katika Mataifa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumzie Wakimbizi. Tanzania ina Wakimbizi kuanzia mwaka 1959, ndiyo hao wanaozungumzwa. wako Katumba, Ngara, Mkoa wa Kagera, Karagwe na Kigoma. Hawa wameiingiza nchi hii katika umaskini

ambao hauna kipimo na ulimwengu unajua hivyo. Ujangili katika mapori yetu ya wanyama, misitu, wizi, ujambazi, utekaji wa magari, vinafanywa na watu hawa. Mwaka 1959 mpaka leo ni miaka karibu 45. Msemaji pale nyuma amezungumzia yanavyojengwa Makanisa, watu wanatembea wanavyotaka, leo tuna Wakimbizi wanaosoma Vyuo Vikuu vya Tanzania wakati Mtanzania mzaliwa anakosa nafasi ya kusoma, lakini haya tunayaona katika hali kama hii. Kwenye vita ya juzi ya Rwanda alipouwawa Habyaremana, *RPF* ilipopata nafasi Wanyarwanda wote waliokuwa wamekimbia ule mwaka wa 1959 mpaka 1963 wote walikwenda vitani na wote wameondoka na mali za Tanzania. Leo wanatumia *passport* za Tanzania kwa matumizi yao na wana marafiki wengi hapa. Wakimbizi waliokuwepo mwaka 1996 wamerudi kwa mamilioni. Lakini wale walioua wako msituni wana silaha nyingi mno. Serikali inafahamu hayo lakini imefumba macho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utakuja Mkoa wa Kagera usitegemee kwamba utaweza kusafiri utoke Biharamulo kwenda Ngara bila kuwa na *escort* na bunduki kubwa kubwa. Anapokuja Kiongozi wa namna yoyote, anapokuwa anatoka kwenye Mikutano kwa mfano Mkoani, pamoja na huyu anayezungumza hapa ni lazima awe na *escort*. Ukilitazama hili, kama Mheshimiwa Naibu Waziri hawezi kutuambia namna ya kumaliza mzigo huu namna ya kuudhibiti, hata kama naunga mkono Itifaki hii, nazidi kufikiri ni kupoteza muda. Wakimbizi waondoke warudi kwao. *(Makofi)*

Atakapokuwa anajumuisha, atuambie kwa tatizo tu la juzi mwaka wa 1993 kwa sababu ya Burundi na 1994 kwa sababu ya Rwanda. Nchi hii imetumia gharama gani wakati kwa wakimbizi Watanzania wanapata taabu katika umaskini mzito? Lakini tunawasimamia hawa tunao. Aniambie jinsi walivyozungumzia Wakimbizi walioko Tanzania. Tanzania imejitwika mzigo mzito ulimwenguni kote. Leo tunakwenda kutia sahihi Itifaki hiyo, leo Bunge lako Tukufu linaridhia kitu hicho, ilitusaidiaje? Lakini juzi tu juma lililopita, Kata moja ya Muleba, Mkoani Kagera kwa usiku mmoja tu majambazi walipo-*strike* Polisi wakaingia katika Kata ile kusaka, walipata zaidi ya bunduki 118 na risasi zaidi ya 2,000, kwa siku mbili peke yake. Inasikitisha na Serikali lazima iwe macho, vinginevyo raia wa Tanzania wako katika hali ngumu na wataendelea kuteseka.

Leo Wilaya za mpakani tunapata matatizo, zina Polisi wachache sana. Vyombo vya kusafiria havitoshi kwa sababu ya hali ya uchumi wa nchi yetu. Lakini hiyo sio tofauti na Kenya ambako Wasomali kila wakati wanauana na Wakenya wakiiba ng'ombe na ngamia. Tunayasikia yaliyoko Uganda na Sudan. Sasa tusizungumze ya Uganda na Rwanda, Rwanda na Congo, Burundi na Congo, ni hao hao ambao tuko katika Itifaki hii. Sikusikia jinsi ambavyo Jumuiya ya Kimataifa imekuwa *involved* katika suala hili zito ambalo linaikabili Afrika kama Afrika, siyo hizi nchi 11 tu zikose amani. Afrika nzima lazima iingilie kati ili kuleta amani.

Wenzangu wametamka kwamba Mwafrika hana uwezo wa kutengeneza silaha nzito kama hizo na kweli ndivyo ilivyo, ishara moja nzuri ya kwamba hizi zinatoka huko nje. Hivi karibuni miaka miwili mitatu Rais wa Marekani amekuja Afrika, nchi ambayo iko katika amani kama Tanzania hakuitembelea. Lakini aliweza kutembelea Rwanda

ambako watu wameuawa kwa mamia. Lakini aliweza kutembelea Uganda. Sasa si vibaya kusema alikuwa anakagua masoko ya silaha. Si vibaya hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaridhia hii kutokea wapi? Ujambazi huu unakuja kwa sababu ya tatizo la ajira. Atuambie nchi hizi maskini ambazo leo Tony Blair analalamikia zile *G7* kwa wakati huu kwamba wafute madeni ya nchi hizi. Lakini sasa anafika mahali pa kukata tamaa. Vijana wengi sasa wanasoma kutoka kila nchi, wanajifunza sayansi ya uchumi na sayansi ya kushindana. Wako katika soko la utandawazi. Hawa vijana wasipoiva, wasipopora, wasipokuwa na silaha, watakula wapi? Watavaa nini? Watalala wapi? Serikali zilizotilia saini Itifaki hii ni budi zijipange vizuri kuwapatia ajira vijana na wale wote wenye sifa za kutumi.

Kuna njia yoyote atatuambia Mheshimiwa Naibu Waziri ya kumaliza matatizo haya! Sijui kama ni kitu kidogo sana tunachokizungumza hapa hata kama tunaweza tukaridhia. Lakini nafikiri kuna matatizo makubwa sana na pengine niseme Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iendelee kufuatilia Itifaki hii na ijue itawaokoaje Watanzania na pengine inaweza kuwa ndiyo *pioneer* wa kuweza kufanya udhibiti huu ukafanikiwa. Kwa sababu ni nchi ambayo ina amani na kila Taifa katika matatizo yao wanakimbilia sehemu yetu, basi sasa ionyeshe mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie majambazi na pengine namna ya kuwasaidia. Juzi nilipokuwa nachangia, nilisema kwamba ni vizuri ile Sheria ya Uhujumu, ya Uhaini na mauaji, sasa ipanuke zaidi kuhusu majambazi. Majambazi wanapopatikana wasipewe dhamana. Majambazi wapewe adhabu zilizo kubwa kusudi labda wengine wajifunze kutokana na hayo. Itatusaidia zaidi kama Mheshimiwa Naibu Waziri atatuambia kwamba nchi ambazo zimeingia katika Itifaki hii zinakubali kutunga Sheria zinazofanana kwa sababu ya kushindana na wimbi la kuenea kwa silaha. Pengine hii itatusaidia kuliko kila nchi kuwa na Sheria zake, kuruhusu kitu hiki, lakini wote tumeridhia Itifaki moja; kumbe kama ni Mkenya amekuja Tanzania akafanya madhambi akapatikana na silaha, atakapokamatwa Kenya watatetea kwamba mlete tutamhukumu huku kwetu. Somalia watasema hivyo, pengine Ethiopia watasema hivyo. Congo hawawezi kusema kwa sababu hakuna Serikali inayojulikana kwa wakati huu, maana vita haitegemewi kwisha hivi karibuni.

Lakini miaka itakwisha na watu watakuwa wanamalizika wakati Itifaki kama hii ipo. Pamoja na yote haya, naomba niunge mkono hoja hii. Lakini naomba Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie anachotegemea kukifanya kwa haya kinafananaje. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi nichangie kwenye hoja hii yenye msisimko mkubwa. Kwanza kabla sijatoa maoni yangu, naomba niungane na wenzangu kutoa pole kwa Jimbo la Kasulu Magharibi kutokana na kifo cha Mheshimiwa Mussati. Pia, niwape pole wenzetu ambao wamefiwa na ndugu zao katika kipindi hiki ambacho tunakizungumzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja iliyo mbele yetu ni kuhusiana na kuangalia hali ya usalama na kuweka usalama uwe endelevu. Pamoja na hayo, ningependa kwanza kuiuliza Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa uzoefu wake pamoja na maoni ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge, hizi silaha hasa zinapitia maeneo yapi mpaka zinaingia nchini kwetu Tanzania? Sisi Tanzania hatuna vita. Nakubali kwamba tumezungukwa na matatizo na jirani wenye vita. Lakini sasa Wizara au Serikali inaweza ikatuambia nini ili tuweze kuweka nguvu zetu pale kuzuia suala hili zima na kuweka hali ya amani ndani ya nchi yetu izidi kwenda mbele?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda kikubwa ambacho napenda nikiseme hapa ni kwamba, naishukuru sana Serikali kwa juhudi ambazo imezifanya katika *operations* mbalimbali za kutafuta silaha. Inapofanya operesheni hizi, kwa kweli panatokea utulivu kwa muda, baada ya muda tatizo tena linaanza. Sura ya hali hii ya matumizi ya silaha au kuonekana kwa silaha au kuwa na silaha katika maeneo kunaachana, watu wa mipakani sura yao ni tofauti na sisi watu ambao hatuko mipakani sura yetu ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo letu hasa linakuwa kwamba majambazi wanasumbua raia kwa silaha katika maeneo yetu. Nakumbuka miaka ya19 70 huko, 1980 pia, Mwanza hapakuwa na matatizo ya majambazi wa kutumia silaha. Ilikuwa ikitokea mara moja. Tatizo hili halikuwepo kabisa. Lakini kwa sasa miaka hii ya 90 linazidi kuongezeka siku hadi siku. Watu wanatumia silaha kuvamia wenzao mchana. Kuna matukio mawili yametokea Mwanza Mjini katikati; kuna moja lilitokea maeneo ya Benki Kuu pale mchana, watu wakafika pale kwenye duka la mtu wakazuia watu wasipite na wakafanya uharibifu wa aina hiyo mchana na Kituo cha Polisi kiko karibu pale.

Tukio lingine lilitokea sehemu ya eneo karibu na soko, kuna Kituo cha Mafuta pale, kama miezi miwili iliyopita. Kwa hali hiyo hiyo kwa sura hiyo hiyo mchana majambazi wamefika pale wakafanya mambo haya, lakini kitu ambacho kinawapa nguvu kufanya yote kwa hali hiyo ya kutisha, ni silaha ambazo zinapatikana pale. Sasa katika juhudi hizi ambazo Serikali inazifanya, imezifanya hizi katika maeneo ya Dar es Salaam, pia Mwanza, Arusha, kwa misako mikubwa. Mimi ningeomba sana sana na niombe Wizara ichukue hatua hiyo kwa Mwanza, wafanye operesheni tena nzito kwa sababu hali imezidi kuwa mbaya kule tena ili kwamba silaha zipungue tena na raia waweze kuishi kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kikubwa ambacho ningependa pia nikieleze hapa kwa uwazi ni kwamba tulipitisha Sheria ya namna gani raia wetu wamiliki silaha na maduka ya silaha yanaruhusiwa kuuza katika nchi yetu? Taratibu hizi nina imani sasa zinaendelea na kuna raia mbalimbali wananunua silaha hizi. Sasa ningeiomba Wizara itueleze kwamba imeona nini katika utaratibu huu? Je, uko salama? Unakwenda vizuri? Watu wanapata yote vizuri na kwamba hali ilivyo ni kwamba utaratibu huu unahitaji labda marekebisho! Ningependa hili jambo waliangalie sasa kwa karibu. Kama walikuwa hawajaanza kuliangalia ningeomba waanze kuliangalie kwa karibu waweze kuona ni nini kifanyike ili tuweze kutekeleza hili Azimio letu au Sheria yetu vizuri bila kuwa sehemu moja ya matatizo ya kuingiza silaha bila utaratibu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa niseme kwamba katika zoezi zima hili la silaha, nina imani wananchi kwa kweli vurugu na fujo, kupigwapigwa kwa bunduki hawataki. Wangependa kukaa kama walivyozoea miaka yote. Nina imani wananchi na raia wanajua maeneo gani matatizo haya na hasa silaha hizi ziko. Ningeomba Serikali itafute namna ya kuwahusisha wananchi kwa karibu katika kutafuta na kusaka hizi silaha kutoka kwa majambazi na watu wenye tabia mbaya ili kwamba kwa pamoja sasa tushirikiane tupunguze matatizo ya silaha katika nchi yetu.

Azimio hili ni zuri, linataka tuweke utaratibu mzuri tuweze kuishi salama na tuwe na amani kama tulivyozoea kuishi hapa Tanzania. Kwa kutoa taarifa ni kwamba Mwanza mwezi jana, madhehebu ya Kikristo walikutana kwa pamoja ili wafanye maombi kwa kuutakia mwaka huu amani na utulivu, jambo ambalo kwa kweli mimi lilinifurahisha na mimi pia nilihudhuria jumuisho hilo. Lakini sasa kitu tunachohitaji hapa ni kwamba juhudi kama hizi ambazo zinatolewa na zinafanywa na madhehebu au watu kwa ajili ya kutafuta amani yanaonyesha kwamba watu wamezoea kuishi kwa utaratibu wa amani na utulivu katika nchi yetu.

Serikali sasa hapa inapewa *challenge* kubwa kwamba inachukua hatua zipi katika kushiriki kwetu katika Azimio hili, kushiriki kwetu katika Itifaki hii ambayo ilihusisha nchi 11 na Tanzania ikiwemo. Ilikuwa kwa kweli ni nia kubwa ya Serikali na sisi wenyewe kama Watanzania kujieleza kwa wenzetu na pia ulimwengu kwa pamoja kwamba sisi tungependa mambo kama haya ambayo yanakwenda nje ya utaratibu, kuwa na silaha ambazo siyo halali, silaha ambazo zinatishia amani na utulivu wa raia, kwa kweli ni jambo ambalo tumelisema wazi kwamba tusingelipenda litokee nchini kwetu na liachwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika haya ningependa niishie hapo lakini kikubwa ni kwamba hayo matatu ambayo nimeyauliza kwa Serikali ningefurahi kama ningepata ufanunuzi ili tuweze kuelewa na tufahamu hali hii inakwenda namna gani. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza ninapenda nitoe pongezi kwa Serikali kwa kuleta Azimio hili na pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kulielezea vizuri katika Bunge lako hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Azimio hili ndiyo tatizo kidogo kwamba kupunguza silaha ndogo, nia lazima iwe ni kuhakikisha kwamba hakuna silaha ya haramu ndogo ambayo inazagaa, hii ndiyo iwe dhana, si kupunguza. Hatuna watu wa kuua na hizo zilizobaki. Kwa hiyo, nia yetu ni kuanzia sifuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi ambazo zinatuzunguka, kuna silaha kedekede ambazo zimezagaa kwenye nchi hizo na zinaletwa kwetu. Kwa mfano Burundi, haina haja ya kueleza kwamba kuna makundi mengi na yote yana silaha. Mfano Somalia, wamempindua Siad Bare na Jeshi limepotea, kila askari amekwenda na silaha

zake. Congo, wamempindua Mobutu na kila mwanajeshi aliyekuwa huko amepotea na silaha zake na kuna vikundi vingi vina silaha vikitumia dhahabu kama tulivyoelezwa. Uganda, Serikali zimebadilisha mikondo, Iddi Amin alipoondolewa na majeshi shujaa ya Tanzania, askari wa Iddi Amin walizagaa na silaha zao wakapotea. Vile vile, Jenerali Okello naye alipokuja na jeshi lake naye alipigwa na Museleni, akapotea na silaha zake. Rwanda, Intarahamwe wamefanya hivyo hivyo. Kwa hiyo Wakimbizi wote hawa wamehamia Tanzania na Tanzania kwa kweli tuiombee Mwenyezi Mungu ni nchi ambayo ni pole mno, kwa nini tunakuwa wapole hivi jamani? Kila mtu mwenye shida zake anakwenda Tanzania. Hivi sisi baba wa kila mtu? Kila mtu mwenye matatizo yake anahamia Tanzania! *(Makofi)*

Mimi naiomba Serikali vitu viwili, kwa sababu pia kuna Wakimbizi wa kiuchumi hapa Tanzania wameanza kuja, ukienda Dar es Salaam, watu wengi sana wana watoto wa nyumbani, wafanyakazi wa nyumbani kutoka Malawi, wengi na pale Kawe kuna Kambi yao kabisa iko pale. Ukitaka mtoto unakwenda pale unauziwa mmoja. *(Kicheko)*

Wakimbizi hawa wote walioko sasa hakuna *group* hata moja ambalo lina haki ya kubaki. Burundi kuna maeneo yana amani, wale Warundi wote walioko Tanzania warudishwe kwao. Warudi kwao! Hatuna sababu ya kuwa na Wakimbizi wa Burundi Tanzania kama ni lazima. Tuwasifu sana wenzetu kwenye Wizara ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na kwa kweli tumpongeze Rais, kwamba sasa tuna Mjumbe kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Tunaiomba Serikali ipeleke Azimio kwenye Baraza la Usalama kwamba Wakimbizi wote wa Rwanda hawana sababu ya kuwa Tanzania, warudi kwao. Wakimbizi wa Burundi warudi kwao, Wakimbizi wa Congo watafutiwe maeneo Congo warudishwe kwao. Tumechoka jamani kuwa nchi ya Wakimbizi. *(Makofi)*

Pili, Jeshi la Wananchi wa Tanzania lifanye operesheni kuanzia Rukwa mpaka Kagera waondoe Wakimbizi wenye silaha wote warudishwe makwao na silaha zote zikusanywe. Hatuwezi kuwa na nchi ambayo watu hatuwezi kuwa na amani kwa sababu ya matatizo ya watu wengine huko. Jirani yako akipigana na mke wake wanahamia kwako? Haiwezekani! Lazima tuwarudishe makwao. Nasema hali ya silaha ndogo ndogo hizi na majambazi ni ya kutisha sana. Kwa mara ya kwanza katika Vijiji vyangu kule Mwanga silaha zimetumika kuiba kule Vijijini. Silaha zimetumika, Kifaru, wamevamia Kituo cha Mafuta, wameua watu. Silaha zimetumika Usangi kule Kijijini milimani, Mzee mmoja ameuawa. Silaha zimetumika Nyumba ya Mungu na hii nina ugomvi kidogo na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mwaka 2002 mwezi wa Pili kama sasa hivi ni mwaka wa tatu wananchi wa pale Nyumba ya Mungu wamejenga Kituo cha Polisi. Tumemwomba Waziri pale wananchi walipofika watusaidie kukamilisha kile Kituo, akaandika barua na nakala ikaenda kwa Mwenyekiti wa Kijiji kuwapongeza kwa kazi nzuri waliyoifanya kujenga Kituo cha Polisi, mwaka 2002 hakusaidia na barua ile ilimwambia Mwenyekiti wa Kijiji, Serikali itakikamilisha Kituo hiki mara moja, mwaka 2002 mwezi Februari.

Bajeti ya 2002 Kituo hakikufanywa, mara moja. Mwaka 2003 bajeti imetolewa hapa, nimesema hapa, nimeambiwa mara tu baada ya bajeti, mara moja Kituo hiki kitakamilishwa. Mpaka leo hamna kitu. Shilingi milioni moja! Siamini kabisa kwamba kweli Serikali inakosa Shilingi milioni moja na imeandika barua ikawaambia wananchi itawasaidia kukamilisha Kituo hiki mara moja. Siamini kabisa! Sasa katika eneo lile, zaidi ya watu sita wameuawa na majambazi kwa sababu hamna ulinzi wa aina yoyote kule na kule kuna watu wa aina nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kijiji kimoja pale Nyabinda kule Nyumba ya Mungu kuna makabila 54. Ni watu aina tofauti tofauti, kuna Mataifa tisa yanayozunguka Tanzania yote yako pale. Watu wanauawa hovyo hovyo, hakuna amani na Serikali inaahidi tutakamilisha Kituo mara moja, Shilingi milioini moja mwaka wa tatu, haifanyi. Kitu gani hiki jamani?

**MBUNGE FULANI:** Maana yake nini?

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mpaka watu wanasema hii Serikali ina nini? Napenda wakati Waziri anajumuisha atupe maelezo tumekosa nini? Au ni siasa? Maana nimeambiwa Siasa inatoka kwenye maneno, “Sio” na “Hasa”. Unaondoa ‘o’, unaondoa na ‘h’, unaunganisha siasa. Hivi siasa kweli na maisha ya watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Mwanga kuna Kituo kimoja tu cha Polisi na Mheshimiwa Naibu Waziri amefanya kazi kule miaka mingi anajua. Kule katika Tarafa Jipendea hakuna Kituo cha Polisi. Wananchi wamejenga Kituo, wanaomba Polisi mwaka mzima sasa, hakuna Polisi amepelekwa kule. Kwa kweli tunaomba sana Serikali ishirikiane na sisi, tukamilishe hiki Kituo cha Lang’a Tabora kama ilivyoomba na ifanye katika mwaka huu wa fedha, isiseme tena mara moja, huko mbele. Serikali itusaidie kukamilisha Kituo cha Kisangara kama tulivyoahidiwa hapa kwenye mwaka wa fedha wa 2003/2004 na Kituo cha Msangeni. Kwa nini msitusaidie? Tumepiga bati, tumekamilisha karibu kila kitu, lakini uwezo ni mdogo na mmesema tumefanya kazi nzuri, tutawasaidia mara moja,. Fanyeni basi!

Mheshimiwa Naibu Spika, yangu kwa kweli makubwa yalikuwa ni hayo. Nimeambiwa mara moja, lakini mwaka wa tatu huu. Ninakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda nitoe shukrani kwa wote ambao wamechangia hoja hii ama kwa kuzungumza ama kwa maandishi. Tatizo hili la silaha ndogo ndogo linazaa maovu mengi katika jamii yetu, ujambazi na kadhalika. Kwa hiyo, linagusa maisha yetu na usalama wa nchi yetu. Ndiyo maana Wajumbe wana haki kabisa kulizungumza jambo hili kwa jazba kubwa kabisa kwa sababu ya unyeti wa jambo lenyewe.

Kwanza kama ilivyo ada nianze kuwatambua wale waliochangia hoja hii. Waliochangia kwa maandishi kwa upande wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, ni Mheshimiwa Ireneus N. Ngwatura, Mheshimiwa Major Jesse J. Makundi, kwa upande wa Upinzani; Mheshimiwa Jackson M. Makwetta, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ali, Mheshimiwa Anatory K. Choya, Mheshimiwa Ibrahim W. Marwa, Mheshimiwa Gwassa A. Sebabili, Mheshimiwa Stephen M. Kazi, Mheshimiwa Kilontsi M.M. Mporogomyi, Mheshimiwa Lucas L. Selelii na Mheshimiwa Prof. Jumanne A. Maghembe.

Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mheshimiwa Cynthia H. Ngoye, Mheshimiwa George M. Lubeleje, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ni nyingi kweli kweli. Niseme tu tumezipokea kama ushauri. Siwezi katika muda huu kuzijibu zote kabisa, haiwezekani, mtanisamehe. Lakini zote zimepokelewa na zote tutazifanyia kazi kwa sababu ni mashauri mazuri yanayotuelekeza katika kutekeleza huu Mkataba ambao baada ya muda mrefu tutauridhia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na hoja za Kamati ya Ulinzi na Usalama, wametushauri kwamba tufanye juhudi kubwa katika kushauriana na nchi wanachama kupunguza matatizo yaliyomo kule ndani, vurugu na utumiaji wa nguvu na chuki na ghasia ili matatizo hayo tuyamalize kwa mazungumzo na tupunguze habari ya vita. Hili ndilo tunalolifanya katika Ukanda huu wa Maziwa Makuu. Juhudi kubwa kabisa zinafanyika sasa hivi katika nchi ambazo zina migogoro. Burundi sasa hivi wamefikia katika hali nzuri. Nchi ile sasa hivi karibu asilimia 95 sasa ni shwari, kasehemu kadogo tu ambako *NFL* wanafanya vurugu pale. Lakini kwa taarifa tulizonazo kwamba kile kikundi kidogo kimeshaanza kuonyesha ishara kwamba wanataka na wenyewe wazungumze, wajiunge na wenzao.

Kwa upande wa *Congo DRC* vile vile nadhani mpaka mwezi Juni, wanaweza wakafanya uchaguzi wao ili wapate Serikali ya muafaka waliochagua wenyewe. Kwa upande wa Sudan, nyinyi wote ni mashahidi kwamba makubaliano kati ya Kusini na Serikali kule, wametia saini Mkataba wa amani pale Nairobi juzi, bado kule Darfur ndiko kuna vurugu, lakini nako itakwisha. Somalia, ambako muda mrefu kabisa wamekuwa hawana Serikali, juzi juzi wamepata Serikali yao na baadhi ya Wabunge sasa wameshaanza kuingia ndani ya Somalia ili Serikali irudi kule.

Kwa hiyo, kwa kweli juhudi zinazofanywa sasa hivi, matunda yameanza kuonekana na ndiyo ombi letu kwamba wakitulia kule, suala la mapigano litatulia na kuzagaa kwa silaha vile vile kutapungua. Ndiyo lengo letu. Hata mwaka 2004 mwezi Novemba, tulifanya Mkutano mkubwa kabisa pale Dar es Salaam wa nchi za Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika na Msemaji mmoja akasema hawa mbona hawakemewi hasa Uganda na Burundi, pale watu walikemewa na wataendelea kukemewa kwa sababu kwa kweli tumechoka mapigano, tumechoka vita, tunataka na sisi Ukanda wetu tupate muda wa kutekeleza masuala ya maendeleo.

Kamati imetushauri habari ya elimu kwa umma ili kusaidia katika mapambano hayo na hata Mkataba wenyewe ndivyo unavyosema, tumekubaliana na nchi zote kwamba mapambano haya lazima tushirikishe umma. Ni moja ya vipengele katika Mkataba; ndivyo unavyotutaka tufanye na sisi Tanzania ndivyo tutakavyofanya. Baadaye nikipata nafasi nitafafanua kidogo. Hoja za Upinzani, wamesema tudhibiti wakimbizi na hili limesemwa na wengi kabisa, kwa sababu moja ya chanzo cha kuzagaa silaha nchini mwetu ni Wakimbizi. Sasa hili la kudhibiti wakimbizi tunalifanya. Katika kila Kambi ya Wakimbizi tumeweka Vikosi Maalum vya Polisi kulinda nyendo za wakimbizi. Lakini kubwa ni lile ambalo mmelisemea wengi pamoja na Mheshimiwa Sebabili kwamba wakimbizi kurudi makwao. Hili ndilo kubwa kabisa na ndilo sasa hivi Serikali inalifanyia kazi kwa nguvu zetu zote.

Wakimbizi wa Burundi wanarejea na juzi alikuja kututembelea Balozi wa Burundi tukazungumza naye. Anasema kwamba, ni kweli *speed* ya kurudi sasa hivi imepungua kidogo, lakini Wakimbizi walio wengi wanasubiri uchaguzi. Tarehe 28 Februari, 2005, watafanya *referendum,* wanapiga kura za maoni kuhusu Katiba *(referendum)*. Wakishamaliza *referendum*, hatua zinazofuata ni uchaguzi. Uchaguzi kwa Serikali za Mitaa, kwenye Vijiji huku chini na baadaye uchaguzi wa Wabunge na Rais. Balozi anasema Wakimbizi walio wengi wa Burundi wanangoja uchaguzi. Wanasema kama uchaguzi utakwenda vizuri kwa amani yeye anaamini kabisa Wakimbizi wote wa Burundi watarejea. Kwa hiyo amesema Burundi ipo tayari kuwapokea Wakimbizi wote watakaokuja, wameshajiandaa vizuri kuwapa makazi, chakula cha kuanzia kwa miezi mitatu mpaka minne wakati wanangoja watakacholima kikomae. Tuko tayari kuwapokea.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, suala la Wakimbizi kurudi ndio agenda kubwa ya Serikali zote mbili, Serikali ya Tanzania na Serikali ya Burundi. Mwezi uliopita, tulifanya mazungumzo kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya *DRC* na *UNHCR* na agenda ilikuwa ni kuwarudisha Wakimbizi wa *DRC*. Tumeshakubaliana kimsingi kwamba sasa wakati umefika *DRC* nako kumetulia waanze kurudi. Kwa hiyo Kikao cha juzi tumekubaliana kimsingi kwamba mwezi ujao sasa, wanakaa Kikao cha Wataalamu kuzungumzia taratibu za kuwarudisha (*logistics)* watatumia kama ni meli gani, utaratibu utakuwaje na kadhalika. Sasa watafanya uchambuzi wa utaratibu wa kuwarudisha.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, nataka kusema kwamba hili la Wakimbizi kurudi makwao, wale wa Burundi na wale wa *DRC*, ndio kazi ambayo Serikali sasa hivi tunaifanya. Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa na wengi wameuliza nini maana ya silaha nyepesi, silaha ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, silaha ndogo ndogo ni zile silaha mtu mmoja anabeba, kwa mfano *pistol, shortgun, SAR,* mtu mmoja anaweza akabeba tu ndio tafsiri ya silaha ndogo ndogo. Silaha nyepesi ni zile silaha ambazo anaweza akabeba mtu mmoja hadi watu watano. Kwa wale waliopitia Jeshini mnajua ile bunduki inaitwa *light machinegun.* Ile *machinegun* ni nyepesi na vitu kama hivyo. Kuna silaha nyingine ambazo watu wawili au wanne mnaweza mkabeba pamoja, hizo ndizo zinaitwa silaha nyepesi. Vile vile, kuna maswali nimeulizwa kuzuia, kudhibiti na kupunguza maana yake nini. Maana

Azimio linazungumzia habari ya Kuzuia, Kudhibiti na Kupunguza. Sasa kuzuia kwa mujibu wa Mkataba wetu, ni kuzuia kwanza utengenezaji wa silaha haramu ili kuzuia biashara ya silaha haramu. Kudhibiti; kuna silaha ambazo ziko nchini kihalali, ziko silaha kwenye Majeshi zile ambazo raia wanaomba kwa utaratibu uliopo kumilikishwa awe anaimiliki kihalali kwa mujibu wa Sheria. Lakini pia hizo nazo tumekubaliana kwenye Mkataba kwamba lazima vile vile tuzidhibiti ili zisitoke katika mikono halali zikaingia kwenye mikono haramu zikafanya vitendo haramu.

Kuhusu kupunguza, Mheshimiwa Prof. Maghembe amesema, sisi hatutaki habari ya kupunguza, tunataka kusikia zero. Sasa katika nchi, huwezi ukawa huna silaha kabisa (*zero*) kwa sababu katika nchi unahitaji na wewe silaha za kujilinda. Kwa hiyo hata tukipunguza zile ambazo ni haramu, lakini zibaki zile halali kwa ajili ya ulinzi wa nchi au wa mtu binafsi *(self protection)*. Kwa hiyo hatuwezi tukaondoa nchi yote ikawa *Arms free,* hakuna silaha hata moja maana hata nchi itakosa ulinzi wa kujilinda au mtu binafsi akakosa namna ya kujilinda, ndio maana ya kupunguza.

Mheshimiwa Makwetta amezungumza habari za Bara letu la Afrika kujaa umaskini, ugonjwa, njaa na kadhalika kwamba haya ndio yanayosababisha matatizo haya. Llakini sasa hivi Bara la Afrika tunajitahidi tusiendelee kuwa Bara la mapigano, giza, njaa na kuzalisha Wakimbizi. Juhudi nyingi zimefanywa, tumejiunda upya katika *AU,* tumeanzisha miradi kama hii ya *NEPAD, Regional Groups,* Makundi ya Ushirikiano ya *ECOWAS* kule Afrika ya Magharibi, *SADC,* zote hizi ni juhudi za pamoja za kujiondoa hapa tulipo. Ndio tumeingia katika Mikataba hii ili tuweze kuachana na mapigano, vurugu na vita, tushughulikie habari ya miradi ya *NEPAD* na *SADC*. Hata jana kulikuwa na Mkutano mkubwa hapa wa *Mtwara Corridor,* haya ndio mambo sasa ambayo tunataka tuyafanye tujiondoe hapo tulipo na ndio *spirit* ya Azimio lenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Aziza amekuwa na mengi ya kusema. Habari ya kwamba tumekuwa wapole mno, kila mkimbizi anakuja kwetu, Mikataba ya Kimataifa ndivyo ilivyo. Tumesaini Mikataba ya Kimataifa na Tanzania sio Kisiwa ndio maana wakiwa na shida kule kwao wanakuja kwetu. Lakini kama nilivyosema, sasa hivi tuko katika *gear* ya kuwarudisha wakimbizi kwao na hii *gear* haina *reverse*. Hata Balozi juzi tumemwambia kabisa kwamba Watanzania sasa wamechoka na huu mzigo, umebebwa karibu miaka arobaini, ni mzigo mzito, wameelemewa, wamechoka. Nimemwambia hivyo hivyo. Kwa hiyo *gear* sasa ni kwenda mbele kwamba Wakimbizi warudi. Tukamwambia kabisa *reverse gear* ya kurudi nyuma katika hilo haipo.

Mheshimiwa Aziza vile vile amesema habari kwamba je, kuna utaratibu gani wa kuzitafuta hizi silaha? Katika kutekeleza Mkataba huu, tunaanzisha mradi maalum wa kuzisaka hizi silaha na kuziteketeza. Jeshi la Polisi tumeunda Kitengo maalum. Ziko nchi marafiki ambazo wametusaidia fedha za kutekeleza mpango huu. Tutashirikisha wananchi katika kutekeleza mpango huu, tutaunda Kamati za kupambana na tatizo la kuzagaa silaha ndogo ndogo kuanzia kwenye Mitaa, Vijiji, Kata, Wilaya, Mkoa mpaka Taifa. Kwa hiyo, ni jambo ambalo tutalifanya. Ni mradi mkubwa kabisa ambao tutaufanya katika kutekeleza huu Mkataba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Aziza, utaratibu wa

kutafuta hizi silaha upo na wakati muafaka ukifika utangazwa utaratibu mzima wa jinsi ya kushirikisha wananchi katika suala hili.

Mheshimiwa Choya ameshauri kila nchi itunge Sheria katika kudhibiti suala hili na Mkataba ndivyo unavyotuagiza. Lakini vile vile tutazame na Sheria zilizopo. Kwenye Mkataba kule nyuma tumeambatisha zile Sheria ambazo tunatakiwa kuzitazama ili zifananefanane na mwelekeo wa Mkataba wenyewe. Mheshimiwa Choya amezungumza habari za elimu ya umma kuhusu tatizo hili kwamba: Je, watu watashirikishwa? Nimeshasema watu watashirikishwa. Tutaunda hizi Kamati ili zitusaidie katika misako tutakayoifanya. Amesema tufanye tathmini kuhusu athari za Wakimbizi hasa silaha walizozileta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo tathmini tunaifanya kwa lengo la kutaka Jumuiya ya Kimataifa watusaidie fedha za kufanya ukarabati wa maeneo yale ambayo yameharibiwa na Wakimbizi kwa namna moja au nyingine. Amesema Mheshimiwa Choya kwamba kuna Vijiji ambavyo vimehamwa kutokana na athari ya ujambazi, Kituo cha Polisi nacho kimehama! Amesema leo hii nitoe agizo Kituo kirudi. Tumesikia hiyo habari na tutaifuatilia kwa sababu nia ya Kituo cha Polisi ni kusogeza ulinzi kwa raia. Sasa Polisi kama inaacha raia inakwenda kwingine tutafuatilia. Napenda kumwambia Mheshimiwa Choya kwamba tutafuatilia hii taarifa aliyotupatia kwamba Kituo kimehama mahali walipo wananchi, wanahamia kwingine na hatua zitachukuliwa ili wananchi wapate ulinzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Marwa, aliuliza silaha ndogo ndogo ni zipi na nadhani nimeshajibu. Vile vile amezungumza habari za mgodi wa Kahama kwamba ulitaka kuleta silaha. Alitaka kujua inakuwaje mgodi wa hawa wageni waingize silaha na Serikali imekubali? Ukweli ni kwamba wali-*apply* kuingiza silaha, lakini Serikali iliwakatalia kwa sababu aina ya silaha walizotaka kuingiza ni silaha za *AK. 47.* Sasa *AK. 47* ni silaha za Kijeshi ambazo kwa mujibu wa Sheria zetu silaha za Kijeshi zinamilikiwa na Majeshi tu. Kwa hiyo kwa msingi huo tuliwakatalia tukawaambia, kama mnataka kuingiza silaha kwa kulinda kiwanda chao, basi waagize zile silaha ambazo zinakubalika kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo Mheshimiwa Marwa, kile kibali hakikutolewa kwa sababu aina ya silaha walizotaka kuagiza hazikubaliki kwa mujibu wa Sheria.

Vile vile Mheshimiwa Choya amesema kuhusu ununuzi wa silaha bila mafunzo kwamba wapate mafunzo kabla ya kutumia. Ni kweli mtu kama ananunua gari halafu hujui kuendesha, halina maana. Kwa hiyo ni kweli hawa ambao wananunua silaha, wanaomba Polisi wanawaelekeza jinsi ya kuitumia ile silaha, kuitunza kwa mujibu wa Sheria, kwa sababu ziko Sheria zake jinsi ya kutunza silaha. Watu wengi hawajui jinsi ya kutunza silaha na ukiiweka hovyo hovyo ikapotea, utaingia katika matata makubwa sana. Ndio maana unatakiwa kama unasafiri na huna haja nayo, basi iweke kwenye Kituo cha Polisi, *(safe custody),* ukimaliza safari yako unakwenda kuichukua unairudi nyumbani. Ukiiacha inazagaa pale nyumbani mtu akaichukua, utaingia kwenye matata makubwa sana. Haya yote wanafundishwa kabla ya kumilikishwa silaha.

Mheshimiwa Marwa amezungumzia suala la magobore. Hili la Magobore pia limeelezwa na Kambi ya Upinzani kwamba hawa namna gani, mbona hawatambuliwi wakaendelezwa? Tumeshajibu swali hili hapa Bungeni kwamba sisi Serikali hatuna tatizo na watu hawa iwapo wangejitokeza. Hata siku moja Waziri wa Ulinzi akasema, mimi ninawatafuta niwapeleke kwenye kiwanda cha Jeshi kule Morogoro. Lakini watu hawa wanapenda kufanya hii shughuli kwa kificho ndio shida kubwa. Lakini kama wakijitokeza sisi Serikali hatuna ugomvi nao, na Waziri wa Ulinzi alishawakaribisha na kuwapa changamoto kwamba wajitokeze awachukue. Kama wanasikia wale wataalam wanaotengeneza silaha huko waliko, basi wajitokeze, Serikali tuko tayari kuwapokea na kuendeleza vipaji vyao kwa sababu hawa ni *scientists* ila shida sasa hivi wanafanya kwa kificho. Sasa kwa kujificha hivyo, siku tukimgundua huyo, ana kosa la jinai. Anageuka kutoka kwenye mtaalam mwanasayansi wa kutengeneza silaha na kuwa na kosa la jinai. Ndio hasa tatizo lilipo katika magobore.

Mheshimiwa Selelii, tafsiri ya silaha ndogo ndogo katika Uzuiaji, Kudhibiti na Kupunguza, nimeshajibu. Ila alikuwa na lile la Wakimbizi wa miaka ya nyuma kwamba kule Bulyanhulu Urambo pamoja na Mpanda kuna Wakimbizi wamekaa tangu miaka ya sabini. Hawa nao uko utaratibu na wenyewe kurudi. Tumesema tunakwenda awamu ya kwanza tunarudisha wale waliyoko Makambini na ndivyo tulivyokubaliana kwenye Mkataba wetu na Serikali ya Burundi. Kwa mfano, kule Kagera na Kigoma.*Phase I.* Tukishawamaliza hao, awamu ya pili, tunakwenda kwa wale waliyoko katika makazi waliyokuwepo kule Katumba, Mishamo na Bulyanhulu tangu miaka ya sabini, *Phase II* na wenyewe itawakumba kwa sababu hawa bado ni wakimbizi hata kama wameshaishi miaka thelathini hapa Tanzania, lakini *status* yao bado ni Wakimbizi. Kwa hiyo nao zama yao vile vile itafika.

Mheshimiwa Mporogomyi, tunamshukuru kwa yale yote aliyotueleza. Mengi kwa kusema kweli yalikuwa ni ya ushauri tu na lile suala la kwamba Tanzania tuna mpango wa ku-*import* Kiwanda cha Kutengeneza Silaha, hili jambo si kweli. Sasa hivi sisi Tanzania kama nilivyojibu swali juzi, bado hatuna Kiwanda cha kutengeneza silaha. Tulichonacho ni Kiwanda cha Kutengeneza Risasi kule Morogoro ambacho kinamilikiwa na Wizara ya Ulinzi. Kwa hiyo ule mpango aliosema Mheshimiwa Mporogomyi, hilo gazeti lilituzulia tu sisi wala hatuna mpango wa sasa hivi wa kununua Kiwanda cha Kutengeneza Silaha. Serikali ifanye msako Kigoma na Kagera

Kwa sasa hivi ipo *operation* inayoendelea kule Kigoma inaitwa Operesheni Saidia Kufichua Silaha. Katika Operesheni hiyo, Wahisani wetu wametupatia Sh.243,000,000/= katika kusaidia kuendesha gharama za Operesheni hiyo. Kwa hiyo, hilo alilolisema Mheshimiwa Mporogomyi, limeanza kutekelezwa kwa Mkoa wa Kigoma. Baada ya hapo tutakwenda Mikoa mingine yenye matatizo makubwa ,hatutaki kuitaja sasa hivi, lakini kwa Kigoma Operesheni inaendelea hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Stephen Kazi na baadhi ya watu wamesema, lakini hizi silaha zinapitia maeneo gani? Zinatoka wapi? Kama nilivyoeleza kwenye maelezo yangu ya awali, chanzo kikubwa cha silaha hasa katika Mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa ni silaha zinazotoka *DRC*, Burundi na Rwanda kwa sababu ya

mapigano. Silaha nyingi tunazikamata katika Mikoa ile ni za kijeshi na zote zina alama za Majeshi ama *DRC*, Rwanda au Uganda. Lakini vile vile, baadhi ya raia ambao tumewapa silaha kihalali, baadhi yao wanawahazima au kukodisha watu wengi ambao wanakwenda kuzifanyia ujambazi. Nataka nitoe onyo kwa wale ambao tumewapa silaha kihalali kwamba, tumewapa masharti ya zile silaha. Kwa sababu hairuhusiwi wakati wowote kumuazima mtu mwingine. Lakini kuna watu ama anamwazima au wanakodisha. Sasa nataka nitoe ilani kabisa kwamba ni kosa kubwa la jinai na tutamkamata yule uliyemuazima na wewe uliyeazimisha silaha yako, wote mtaunganishwa katika ujambazi.

Kwa hiyo, napenda kutoa onyo kwa wale watu ambao tumewapa silaha kihalali wasiwaazimishe kwa sababu kuna baadhi ya kesi ambazo wamekamatwa watu ambao wameazimana silaha zikaenda kufanya ujambazi. Chanzo kingine ni haya magobore ambayo nilikuwa nayasema, kuna baadhi ya watanzania wanayatengeneza kwa siri na kuiuza kwa siri. Lakini na mimi vile vile misako niliyoifanya ni pamoja na haya migobole.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Kazi amesema kule Mwanza tufanye operesheni nyingine na tumesikia hilo ombi na sasa hivi tuko Kigoma na baada ya Kigoma kuna Mikoa tutaendelea na nina hakika Mwanza tutafika. Kuhusu maduka ya kuuza silaha, Mheshimiwa Kazi anauliza: Je, kuna usalama? Huo utaratibu hauna matatizo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tuna maduka mawili tu ya kuuza silaha hapa nchini. Tuna duka linaitwa *Tanganyika Arms* linalomilikiwa na Mtanzania mwenzetu ambaye hatuna wasiwasi naye. La pili, linamilikiwa na Jeshi la Wananchi, vile vile hatuna mashaka nao. Utaratibu wa kumiliki ni kwamba huwezi kununua silaha pale mpaka kwanza uwe umepata kibali cha kumiliki silaha. Kibali cha kumiliki silaha unaanza kukiomba kwenye Mtaa au Kijiji unachokaa, wakujadili: Je, huyu ni raia sawasawa? Ni jambazi au ni mtu mwema? Mlevi au siyo? Hasira zake ziko mbali au karibu? Wanakuchambua jinsi wanavyokujua pale. Wakiridhika, ndio unapatiwa silaha, na wengi wananyimwa. Wengine pale wanaishi Kijiji lakini ni mkorofi kila siku akinywa pombe anagombana na watu, wanamjua tabia yake, hawawezi wakam-*recommend* ili apate silaha. Kwa hiyo baada ya pale ndio inakwenda kwenye Kata yako, Wilaya, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, wote huko wanakuchambua. Kwa silaha za kawaida kama bunduki, maombi yanaishia kwenye Mkoa, wakisharidhika na wewe ndio unakwenda sasa kwenye hilo duka. Kwa *pistol* umilikishaji wake ni kutoka Mkoa inakwenda mpaka Makao Makuu ya Wizara kule *DSA* ndio nayo inakuchambua na kila kitu ikiridhika ndio unapata kibali.

Kwa hiyo, uko utaratibu tu mzuri wa nani amiliki silaha na nani asimiliki, ukishapata hicho kibali ndio unakwenda dukani. Napenda kumwambia Mheshimiwa Kazi kwamba, utaratibu huu mpaka sasa unafanya kazi vizuri wala hauna matatizo yoyote na hatujapata kesi ya mtu hata mmoja ambaye hajapata kibali akaenda kuuziwa bunduki katika haya maduka mawili niliyoyasema. Kuhusu kushirikisha Umma nilishasema kwamba utaratibu unaokuja, tunaunda Kamati kuanzia za Kijiji au Mtaa, Kata, Wilaya

mpaka Mkoa ambazo Kamati hizi ndizo zitakazofanya kazi zikishiriana na vyombo vya dola katika kufanya misako ya silaha ndogo ndogo na kuzikamata.

Mheshimiwa Maghembe, amekuwa mkali kidogo kuhusu Vituo vya Polisi ili kupambana na ujambazi. Lakini Mheshimiwa Maghembe ambacho hakusema ni kwamba kuna baadhi ya shughuli zimefanywa kule Mwanga. Askari wake walikuwa na shida sana ya nyumba. Tumejenga nyumba nzuri za ghorofa, lakini angalau Mheshimiwa angetupongeza kidogo kwamba hilo mmefanya, fanyeni na hili pia. Hakupongeza hata kidogo! Sasa tukifanya mambo mazuri, angalau na nyinyi mseme hapa mmefanya hili na sasa fanyeni na hili. Tumejenga nyumba za kisasa pale kwa gharama kubwa sana. Siku nyingine angalau pongezi basi ili na sisi tupate moyo kwamba tuko pamoja. *(Kicheko/Makofi)*

Lakini kuhusu Vituo, napenda kumwambia Mheshimiwa Maghembe kwamba tumechelewa kutekeleza ahadi yetu kwa sababu tu kwamba hivi Vituo vinavyojengwa na wananchi ni vingi nchi nzima na pesa tunazopata kwa mwaka mmoja hazitoshi kusaidia wananchi kila mahali wanapojenga Kituo. Ndio maana tunachelewa. Siyo kwake tu, wako wengi wanajenga Vituo tumewaahidi kuunga mkono, hatujawaunga mkono. Nia ipo, lakini uwezo ni mdogo ndio maana tumechelewa, siyo kwa sababu ya ujeuri, ufedhuli, hapana. Ni kwa sababu tu ya matatizo ya Bajeti. Hata hivyo, kwa Vituo ambavyo tuliahidi hivi juzi Lang'ata Bora, pale tayari Serikali imepeleka Sh.2,400,000/= katika kusaidia kumalizia ujenzi. Kisangara, Sh.2,000,000/= kuunga mkono na Ugweno Msangeni Sh. 1,800,000/=. Kwa hiyo, Mheshimiwa Maghembe asikasirike sana kwa sababu tuko naye kama tulivyo na baadhi ya Wabunge wengi ambao tumewaahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu waliochangia kwa maandishi. Lakini nataka tu niseme kwamba Mheshimiwa George Lubeleje, yeye amesisitiza habari za udhibiti, uingiaji na uzagaaji wa silaha na ndilo hasa lengo la Mkataba huu. Vile vile, amesema tudhibiti Makampuni ya Ulinzi Binafsi. Makampuni haya ni mapya, huko nyuma tulikuwa hatuna Sheria ya kuwadhibiti, sasa hivi tunaandaa Sheria ya kudhibiti Makampuni binafsi. Wakati Sheria hiyo tunaisubiri, tunawabana kwa Sheria zilizopo kwa mfano, lazima walinzi wao kabla hawajawaajiri kwenye Kampuni zao za ulinzi, lazima waende Makao Makuu ya Polisi wachukuliwe alama za vidole ili wachunguzwe na kuwa *vetted*. Silaha wanazozitumia kwenye Kampuni zao lazima ziorodheshwe kwa *OCDs* ili zijulikane. Na wale maaskari ambao wanawaajiri tunataka tuone Mikataba yao ya Ajira na kama wanawalipa kweli mishahara kulingana na kima cha chini. Kwa hiyo tunawabana kwa Sheria zilizopo wakati tunaandaa Sheria mpya ya kuwadhibiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Ngoye yeye ametueleza habari za elimu kwa umma ili wananchi washirikishwe watuunge mkono katika hili. Vile vile na hili tunalifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo ni mengi sana mtanisamehe ambao sikuwajibu, lakini yote ambayo mmetuambia tumeyapokea na tutayafanyia kazi. La mwisho ni kwamba, tarehe 15 Machi, 2005, ni siku ambayo tutakubaliana katika Nchi Wanachama juu ya kuanza kutekeleza hili Tamko la Nairobi. Katika siku hiyo

tumeambiwa kila nchi, moja ya shughuli ya kufanya ni kuchoma moto zile silaha haramu zilizokamatwa. Sisi siku hiyo tutateketeza silaha 1,000 katika kuunga mkono hili Tamko la Nairobi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Itifaki ya Kuzuia, Kudhibiti na Kupunguza Silaha Ndogondogo na Nyepesi liliridhiwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Azimio hilo limeafikiwa na Bunge na limepitishwa rasmi. Waheshimiwa Wabunge hapa ndio tumefikia mwisho wa shughuli za leo. Kwa hiyo naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho Saa Tatu Asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 01.29 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Ijumaa Tarehe 11 Februari, 2005 Saa Tatu Asubuhi)*